**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**2020 - 2025**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Zubeir Ali Maulid | - | SPIKA |
| 2. | Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/Nafasi za Wanawake |
| 3. | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | - | Jimbo la Dimani |
| 4. | Mhe. Shaaban Ali Othman | - | Jimbo la Mpendae |
| 5. | Mhe. Hemed Suleiman Abdulla | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Uteuzi wa Rais |
| 6. | Mhe. Mudrik Ramadhan Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji/ Jimbo la Bububu. |
| 7. | Mhe. Masoud Ali Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Ole. |
| 8. | Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora/Jimbo la Makunduchi. |
| 9. | Mhe. Jamal Kassim Ali | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Fedha na Mipango/Jimbo la Magomeni. |
| 10. | Mhe. Dkt Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi/Jimbo la Donge. |
| 11. | Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan | - | MBM/Waziri wa Kilimo, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo/Jimbo la Paje |
| 12. Mhe. | Simai Mohammed Said | - | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Tunguu |
| 13. Mhe. | Tabia Maulid Mwita | - | MBM/Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo/ Uteuzi wa Rais |
| 14. Mhe. | Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi/ Nafasi za Wanawake |
| 15. Mhe. | Rahma Kassim Ali | - | MBM/Waziri Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi/Nafasi za Wanawake |
| 16. Mhe. | Suleiman Masoud Makame | - | MBM/Waziri wa Maji, Nishati na Madini/Jimbo la Chonga |
| 17. Mhe. | Abdulla Hussein Kombo | - | MBM/Waziri wa Uchumi wa Bluuu na Uvuvi /Jimbo la Mkoani |
| 18. Mhe. | Lela Muhamed Mussa | - | MBM/Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale/Nafasi za Wanawake |
| 19. Mhe. | Abdalla Abasi Wadi | - | Jimbo la Nungwi |
| 20. Mhe. | Ali Abdulgulam Hussein | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 21. Mhe. | Ali Suleiman Ameir | - | Jimbo la Pangawe |
| 22. Mhe. | Ameir Abdalla Ameir | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 23. Mhe. | Anna Athanas Paul | - | Uteuzi wa Rais |
| 24. Mhe. | Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Mahonda |
| 25. Mhe. | Azza Januar Joseph | - | Nafasi za Wanawake |
| 26. Mhe. | Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 27. Mhe. | Bakar Hamad Bakar | - | Jimbo la Wawi |
| 28. Mhe. | Bihindi Hamad Khamis | - | Nafas iza Wanawake |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **29. Mhe.** | **Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba)** | | **Nafasi za Wanawake** |
| **30. Mhe.** | **Habibu Ali Muhamed** | **-** | **Jimbo la Mtambwe** |
| **31. Mhe.** | **Haji Omar Kheri** | **-** | **Jimbo la Tumbatu** |
| **32. Mhe.** | **Haji Shaaban Waziri** | **-** | **Jimbo la Uzini** |
| **33. Mhe.** | **Hamza Hassan Juma** | **-** | **Jimbo la Kwamtipura** |
| **34. Mhe.** | **Harusi Said Suleiman** | **-** | **Jimbo la Wete** |
| **35. Mhe.** | **Hassan Hamad Omar** | **-** | **Jimbo la Kojani** |
| **36. Mhe.** | **Hassan Khamis Hafidh** | **-** | **Jimbo la Welezo** |
| **37. Mhe.** | **Hudhaima Mbarak Tahir** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **38. Mhe.** | **Hussein Ibrahim Makungu** | **-** | **Jimbo la Mtoni** |
| **39. Mhe.** | **Juma Makungu Juma** | **-** | **Jimbo la Kijini** |
| **40. Mhe.** | **Juma Ali Khatib** | **-** | **Uteuzi wa Rais** |
| **41. Mhe.** | **Issa Haji Ussi Gavu** | **-** | **Jimbo la Chwaka** |
| **42. Mhe.** | **Kombo Mwinyi Shehe** | **-** | **Jimbo la Wingwi** |
| **43. Mhe.** | **Machano Othman Said** | **-** | **Jimbo la Mfenesini** |
| **44. Mhe.** | **Maryam Thani Juma** | **-** | **Jimbo la Gando** |
| **45. Mhe.** | **Mihayo Juma Suleiman** | **-** | **Jimbo la Mwera** |
| **46. Mhe.** | **Miraji Khamis Mussa** | **-** | **Jimbo la Chumbuni** |
| **47. Mhe.** | **Mohamed Mgaza Jecha** | **-** | **Jimbo la Mtambile** |
| **48. Mhe.** | **Mohamed Ahmada Salum** | **-** | **Jimbo la Malindi** |
| **49. Mhe.** | **Mtumwa Peya Yussuf** | **-** | **Jimbo la Bumbwini** |
| **50. Mhe.** | **Mussa Foum Mussa** | **-** | **Jimbo la Kiwani** |
| **51. Mhe.** | **Mwanaidi Kassim Mussa** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **52. Mhe.** | **Mwantatu Mbarak Khamis** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **53. Mhe.** | **Mwanajuma Kassim Makame** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **54. Mhe.** | **Dkt. Mwinyi Talib Haji** | **-** | **Mwanasheria Mkuu** |
| **55. Mhe.** | **Nadir Abdullatif Yussuf** | **-** | **Jimbo la Chaani** |
| **56. Mhe.** | **Nassor Salim Ali** | **-** | **Jimbo la Kikwajuni** |
| **57. Mhe.** | **Nassor Ahmed Mazrui** | **-** | **Uteuzi wa Rais** |
| **58. Mhe.** | **Omar Said Shaaban** | **-** | **Uteuzi wa Rais** |
| **59. Mhe.** | **Panya Ali Abdalla** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **60. Mhe.** | **Rukia Omar Ramadhan** | **-** | **Jimbo la Amani** |
| **61. Mhe.** | **Saada Ramadhan Mwendwa** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **62. Mhe.** | **Dkt. Saada Mkuya Salum** | **-** | **Uteuzi wa Rais** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **63. Mhe.** | **Saidi Saleh Salim** | **-** | **Jimbo la Tumbe** |
| **64. 5Mhe.** | **Sabiha Filfil Thani** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **65. Mhe.** | **Salha Mohamed Mwinjuma** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **66. Mhe.** | **Salma Mussa Bilal** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **67. Mhe.** | **Suleiman Makame Ali** | **-** | **Jimbo la Ziwani** |
| **68. Mhe.** | **Suleiman Haroub Suleiman** | **-** | **Jimbo la Kiembe Samaki** |
| **69. Mhe.** | **Sulubu Kidongo Amour** | **-** | **Jimbo la Mkwajuni** |
| **70. Mhe.** | **Shadya Mohamed Suleiman** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **71. Mhe.** | **Shamata Shaame Khamis** | **-** | **Jimbo la Micheweni** |
| **72. Mhe.** | **Shaib Hassan Kaduara** | **-** | **Jimbo la Chake Chake** |
| **73. Mhe.** | **Yahya Rashid Abdulla** | **-** | **Jimbo la Kwahani** |
| **74. Mhe.** | **Yussuf Hassan Iddi** | **-** | **Jimbo la Fuoni** |
| **75. Mhe.** | **Zaina Abdalla Salum** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **76. Mhe.** | **Zawadi Amour Nassor** | **-** | **Jimbo la Konde** |

**Ndg. Raya Issa Msellem - Katibu**

**Kikao cha Tatu - Tarehe 12 Februari, 2021**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua*

## MASWALI NA MAJIBU

**Nam. 69**

**Ukosefu wa Miundombinu Bora kwa Madrasa**

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum -** Aliuliza:-

Walimu wa Madrasa ni kundi ambalo limekuwa likisaidia sana kuijenga jamii ya wananchi ambao wana maadili na imani kubwa. Lakini ni kundi ambalo limekuwa likikabiliwa na changamoto kubwa za kukosa uwezo wa kuziendesha madrasa hizo kutokana na miundombinu isiyobora ambayo inawakosesha kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Je, lini serikali itawazingatia walimu wa madrasa kuwawekea mazingira bora ya kufanyia kazi zao.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora -** Alijibu:-

Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama na tukaendelea na vikao vyetu. Sasa mheshimiwa kwa heshima naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 kama ifuatavyo:-

Ni kweli walimu wa madrasa wamekuwa wakisaidia kujenga jamii yenye maadili mema na kukuza imani zao. Kadhalika walimu hawa wanakabiliwa na changamoto kubwa zinazowakosesha uwezo wa kuziendesha madrasa hizo kwa ufanisi.

Kwa kutambua hilo, serikali kupitia Ofisi ya Mufti ya Zanzibar imeanza kushughulikia suala hili kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

i. Kufanya ukaguzi maalumu ili kutambua idadi ya misikiti na madrasa zilizopo Unguja na Pemba ambapo tayari ukaguzi huo umefanyika na jumla ya madrasa 4,947 na misikiti 2,870 imepatikana. Aidha, idadi ya walimu 15,573 imethibitishwa kwa madrasa hizo za Unguja na Pemba.
ii. Serikali imepanga kutoa mafunzo ya Ualimu kwa Walimu wa Madrasa kwa lengo la:

    a) Kuwajengea uwezo mzuri wa kufundisha
    b) Kuwapa vyeti na kuwasajili wahitimu wa mafunzo hayo

c) Kuwapa vibali wale wenye uwezo na sifa za kufundisha
d) Kuwaombea ruzuku inapopatikana fursa.
e) Kuziunganisha madrasa zinazokosa usimamizi mzuri na zile zenye usimamizi mzuri ili kuboresha ufanisi wa madrasa hizo.
f) Kutumia mtaala mmoja kwa madrasa zote mara tu itapozinduliwa.

Aidha, suala la miundombinu ni jambo la muhimu lakini ni pana sana kwani suala hili linahusisha posho na mitaala mpaka majengo ya kusomea. Kwa upande wa posho ya walimu ambapo ikipatikana kwa wakati itasaidia sana kuwatuliza walimu na kuepuka tatizo la kuwashikiza mabarobaro ambao kwa kawaida hubaki ndani ya madrasa hizo na kusababisha vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto wengine.

Mhe. Spika, ili kufanikisha suala hili kupitia Baraza lako tukufu kwa kuanzia nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge wa majimbo yote ya Zanzibar tushirikiane katika kuwapatia ufumbuzi suala hili ili kila mmoja wetu ajitahidi kuwapa angalau kiasi fulani cha sabuni walimu wa madrasa ndani ya majimbo yao kwa kadri hali ya fedha itakavyokuwa inaruhusu. Pia na serikali itaendelea kutafuta mbinu mbali mbali za kusaidia kwa kutafuta mfadhili ambao wapo katika jitihada za kuweza kusaidia katika maeneo kama hayo.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Ahsante sana Mhe. Spika, na nachukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla kutokana na utaratibu mzuri ambao wameuandaa kwa madrasa zetu za Unguja na Pemba. Mhe. Spika, mimi nina swali moja la nyongeza, swali langu lilikuwa lini serikali itazingatia kuwawekea mazingira bora ya kufanyia kazi. Sasa mpango uliokuwepo ni mpango mzuri namuuliza Mhe. Waziri sasa mpango huu lini utaanza *particularly* kuwajengea uwezo, kuwapa vyeti na kuwapa vibali na kuwaombea ruzuku. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum swali lake la nyongeza. Hakika serikali ingetamani hata kesho ifanyike jambo hili, lakini pale hali itaporuhusu tutafanya hivyo lakini kwa sasa hivi serikali inafanya jitihada ya kutafuta taasisi zile yapo mashirika ambayo yanatoa misaada ya Kiislamu kwa ajili ya madrasa na misikiti na wafadhili kama hawa wapo wengi. Sio lazima kwenye taasisi hata watu binafsi waliokuwa tayari wakati mwengine wanasaidia, ndio pale tulipoesema sisi kwa kuanzia hatua hii ya mwanzo basi ni vyema sisi wawakilishi, wabunge wa majimbo tusaidiane angalau kuwagaia sabuni wale vijana wetu wanatusaidia sana katika maeneo yetu kutuliza hali na amani kwa vijana wetu.

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf:** Bismilah Rahman Rahim. Mhe. Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza yenye (a) na (b).

Mhe. Spika, kwa kuwa serikali imesema kwamba itajitahidi na sisi tuna Ofisi ya Mufti chini ya wizara yake.

a) Je, Ofisi ya Mufti imekaa na Mufti wenzake labda nchi ya Oman, Saudia Arabia, UAE ambao Mufti wa kule huwa na package ya fedha na fedha wanaweza wakasema wao wakati wowote watachangia kiasi gani, wamewahi kukaa au kupeleka maombi jinsi ya kuweza kuwasaidia walimu ambao hawana uwezo.

b) Kwa kuwa kuna *NGO's* nyingi za kidini zinaweza kusaidia walimu ambao hawajiwezi kwa sababu sisi wenye majimbo, mimi nina madrasa 67 na nina walimu zaidi ya 450 nitaweza kuwalipa vipi pesa ya sabuni kama serikali pamoja na Ofisi ya Mufti haijatusaidia, sisi tuko tayari kuchangia lakini lazima tupate nguvu ya serikali na Ofisi ya Mufti kusaidiwa kupitia *NGO's* na Ofisi za Mufti wengine ambao wa nchi za Kiislamu tuweze kuona vipi tutawasaidia walimu wetu. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, jitihada ya Ofisi ya Mufti ziko wazi wanajitahidi sana na ana mashirikiano mazuri na ma-Mufti wenzake hasa wa Oman na nchi za Kiarabu na maeneo mengine. Wamefanya jitihada kubwa ya kutafuta mbinu mbali mbali lakini kuomba nako kuna njia zake vile vile, unajua huwezi kufika mahali ukajidhalilisha kiasi hicho unakwenda kumtafuta Mufti mwenzako akugaie pesa kwa kusaidia. Nadhani sisi Wazanzibari wenyewe tungejipanga vizuri kuna watu wana uwezo mkubwa sana hapa ambao wanasaidia shughuli za Kiislamu kuliko kwenda kuomba mataifa ya nje.

Mhe. Spika, mashirikiano ni mazuri tutamuomba Mufti wakati atakapopata fursa ya kwenda nje, sasa hivi ndio nje hakwendeki kutokana na hali ya maradhi yalivyo, lakini hali itakapotulia inshaallah watashirikiana hata kwa njia ya mitandao kuona kiasi gani tunaweza kusaidia kwa sababu misikiti inajengwa na tunaishuhudia, kuna mahali panajengwa msikiti kila hatua tano msikiti, hatua tano msikiti. Sasa watu wale ambao wanajenga misikiti ni vizuri sasa hivi wangefanya utaratibu wa kuwasaidia hawa walimu wa madrasa ambao wapo tayari katika maeneo yetu ingependeza zaidi.

Mhe. Spika, kuhusu suala la *NGO's* serikali iko makini kidogo kuziangalia hizi *NGO's*, unaweza kuwa *NGO's* badala ya kuleta faraja ikaleta dhiki na *NGO's* hizi zinakuja na madhumuni yake, tusije tukazikaribisha katika maeneo ambayo kama haya ya kidini tukaja tukaharibikiwa huko baadae. Kwa hiyo, serikali itakuwa makini hatukatazi lakini kwanza *NGO* hiyo ipitie katika mikondo inayohusika kisheria, ije katika Ofisi ya Mufti ifanyiwe *vetting* tukiridhika tutaziruhusu hatuna matatizo.

**Nam. 39**

**Changamoto za Upatikanaji wa Vyeti vya Kuzaliwa**

**Mhe. Hassan Hamad Omar –** Aliuliza:-

Ulipofanya ziara ya kushtukiza ofisi ya kutoa vyeti vya kuzaliwa uligundua madudu mengi yanayokwamisha upatikanaji wa huduma hiyo na ukatoa muongozo ili kuondoa urasimu katika upatikanaji wa haki ya msingi.

(a) Je, ni wajibu mtu anapofuatilia cheti cha mtoto, lazima alete cheti cha kuzaliwa cha baba na mama na cheti cha ndoa.

(b) Je, kitambulisho cha wazazi hakitoshi kuwa ni ushahidi.

(c) Je, wizara inafahamu kwamba kuna wazee wengi wameoa pasi na kupewa vyeti vya ndoa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - **Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.39 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, usajili wa kizazi hai kwa ajili ya cheti cha kuzaliwa cha mtoto hakuna ulazima wa moja kwa moja kwa wazazi kuleta vyeti vyao vya kuzaliwa au vya ndoa isipokuwa pale tu inapohitajika kwa mujibu wa mazingira husika. Kwa mfano, cheti cha kuzaliwa huhitajika pale tu mzazi baba/mama anapokuwa hana kitambulisho rasmi kama cha Mzanzibari Mkaazi, cha Taifa au *Passport*. Kwa upande wa cheti cha ndoa huhitajika kuthibitisha iwapo mtoto aliyezaliwa ni wa ndani ya ndoa au la. Aidha, iwapo wazazi hawana hata kimoja kati ya vyeti hivyo, mtoto anaweza kusajiliwa na itatosheleza iwapo mzazi ataeleza tu kwamba mtoto huyo ni wa ndani ya ndoa na kutaja tarehe/mwaka wa ndoa hiyo ili taarifa hiyo iingizwe katika mfumo wa usajili. Vile vile iwapo mtoto ni wa nje ya ndoa ataweza kusajiliwa isipokuwa ni lazima ielezwe hivyo ili taarifa hiyo iingizwe katika mfumo. Taarifa hizi za ndoa na nyengine kama za kiafya zinahitajika kwa kuzingatia kwamba mfumo wa usajili wa vizazi, vifo, ndoa na talaka mbali ya kusajili na kutoa vyeti vya matukio hayo pia unatumika kwa ajili ya kutoa taarifa mbali mbali za kitakwimu.

(b) Mhe. Spika, vitambulisho vya wazazi vinatosha kuwa ni ushahidi katika usajili wa mtoto. Aidha, mbali ya kuwa ni ushahidi vitambulisho hivyo vinahitajika katika kupata usahihi wa majina ya wazee yanapoandikwa katika cheti cha kuzaliwa cha mtoto kwa lengo la kuepusha makosa ya kiuandishi ndani ya cheti hicho. Kuwepo kwa makosa kama hayo jambo ambalo hupelekea usumbufu mkubwa na gharama kwa watoto wanapoanza kusoma au kufanya kazi kwa kuomba kufanyiwa marekebisho mara kwa mara.

(c) Mhe. Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ inafahamu kwamba ndoa yoyote lazima ifungishwe na mfungishaji ndoa maalum aliyekabidhiwa daftari la kufungisha ndoa na Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii. Wafungishaji ndoa hawa huwa aidha ni Masheikh, Mapadri au Viongozi wa dini nyengine zinazotambulika kiserikali na watalazimika baada ya kufungisha ndoa kuwapatia wana ndoa vyeti vya awali ambavyo wana ndoa hao wanawajibika kuviwasilisha katika Ofisi za Wakala kwa ajili ya kusajiliwa na kupatiwa vyeti rasmi. Kwa hivyo, ofisi inafahamu kwamba watu wote waliooa ni lazima wawe na vyeti hivi vya awali vinavyotolewa na wafungishaji ndoa. Hata hivyo, wizara pia inafahamu kwamba watu wengi waliooa hawana vyeti rasmi vya ndoa vinavyotolewa na wakala kutokana na kutozisajili ndoa zao na ndio maana ofisi yetu ya wakala inaendelea kufanya kampeni ya kuwashajiisha wananchi kusajili matukio yote ya kijamii yakiwemo vifo, ndoa na talaka. Kwani cheti cha ndoa ndio uthibitisho rasmi wa uwepo wa ndoa hiyo pale utakapohitajika katika masuala mbali mbali.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Mheshimiwa kwanza nikupongeze kwa majibu yako mazuri na sahihi, lakini pamoja na ufuatiliaji wako mzuri nina swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa wananchi wetu tumeshuhudia wakipata usumbufu mkubwa ukienda pale utafikiria watu wanasubiri vyeti kama waliofugwa lakini tunakushukuru kwa ufuatiliaji wako. Hili suala la kuwa mpaka mtu awe na cheti cha ndoa ndio apate cheti cha mtoto wake limekuwa linawasumbua wananchi wetu. Kwa hivyo, mheshimiwa ni lini usumbufu huu utaondoka kwa kuwafahamisha watendaji wako.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu swali la nyongeza Mhe. Hassan Hamad Omar ni kwamba sheria Nam. 3 ya 2018 ya kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Matukio ya Kijamii imeelezea taratibu za upatikanaji wa cheti cha ndoa, kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi na vyeti vya kuzaliwa. Kwa hiyo, jambo hili si kwamba ni jambo tulilolianzisha kama ofisi, ni jambo ambalo limeanishwa ndani ya sheria hiyo. Kwa hiyo, lini tunaweza kusema kwamba hilo litaondoka labda tuseme tufanye mabadiliko ya sheria hiyo, lakini jambo ambalo hatulioni kwa sasa kama lina ulazima wa kufanya hivi. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Zawadi Amour Nassor:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko mengi juu ya vyeti feki vya kuzaliwa. Je, wizara yako inathibitisha hili kwa baadhi ya ofisi zako za vyeti vya kuzaliwa inapotoa huduma hii. Kama ndio ni hatua gani zilizochukuliwa kwa vile waliotoa huduma hii ni watendaji wa serikali yako ili kuhakikisha kwamba hili tatizo halitokei tena na wao wamewekwa kwenye fungu gani mpaka sasa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Zawadi Amour Nassor swali lake la nyongeza. Kwanza nikubaliane nae ni kweli ipo changamot hiyo lakini kama ambavyo tumeshaanza kuchukua jitihada ya kuziondosha changamoto hizo, naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba pamoja na wawakilishi wengine tutaendelea kuchukua jitihada ili kuziondosha changamoto hizo na huduma hiyo kupatikana kwa mujibu wa sheria kwa wale wote wanaostahiki.

**Mhe. Aza Januar Joseph:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba upatikanaji wa vyeti vya ndoa unakuwa na gharama ambayo mara nyingi huwasababisha wana ndoa kukosa vyeti hivi, serikali itachukua hatua gani ya kuhakikisha kwamba suala hili linakuwa na gharama ndogo ili wote waweze kumudu kupata vyeti.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, naomba nimjibu swali la nyongeza Mhe. Aza Januar Joseph. Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe wengine gharama ambayo inatozwa kwa ajili ya upatikanaji wa cheti cha ndoa ni gharama ndogo sana. Kimsingi ni gharama ambayo tukisema hata serikali tukianzisha tukitazama ile *production cost* ya hicho cheti chenyewe na gharama anayotozwa mwananchi kwa kweli kusema gharama hiyo ni kubwa, sisemi kwamba labda si kubwa

kulingana pengine na hali ya maisha ya wananchi wetu. Lakini kimsingi gharama hiyo ni gharama ya kawaida kwa sababu gharama ya cheti hicho haifiki shilingi hata 10,000/=. Kwa hiyo, katika msingi huo tunaona kweli ni gharama ambayo kwa mtu aliyeamua kuingia kwenye ndoa ni gharama ambayo iko *affordable*. Nashukuru Mhe. Spika.

**Nam. 43**

**Ujenzi wa Soko katika Eneo la Mtambile**

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha –** Aliuliza:-

Katika Jimbo la Mtambile kuna wauza samaki wengi wanaofanya biashara zao kiholela kando kando ya barabara kutokana na kukosa soko la kuuzia samaki wao. Hali hiyo huwapa usumbufu hususan katika kipindi cha mvua na kuharibu haiba ya eneo hilo.

Je, serikali ina mpango gani wa kuwajengea soko wananchi wanaoishi katika maeneo hayo ili waweze kufanya biashara zao bila usumbufu wowote.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.43 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kupitia Baraza la Mji Mkoani lina mpango wa kujenga soko la samaki na mboga mboga katika Jimbo la Mtambile kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Utekelezaji wa azma hiyo utakwenda sambamba baada ya kupatikana uhakika wa eneo litakalopitiwa na ujenzi wa barabara kuu ya Chake Chake Mkoani kutokana na kuwa eneo linalopendekezwa sasa lipo kando kando na barabara hiyo.

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nataka kumuuliza maswali mawili madogo.

a) Mhe. Spika, ametwambia kwamba katika bajeti hii wameadhimia kulijenga soko hilo na kuingiza pesa, nataka nimuulize ni robo ipi.

b) Mpaka sasa hawajapata uhakika wa hiyo barabara kama itapita wapi mpaka wapi wakati barabara imeshapimwa zamani.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, samahani lile swali la kwanza naomba arudie, swali la pili nimelipata.

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha:** Umesema kwamba mnaingiza pesa kupitia awamu hii ambayo inaingia, nimekuuliza tu robo ya mwaka ipi.

**Mhe. Spika:** Robo ipi ya mwaka huu ambayo mtaingiza fedha au vipi?

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha:** Robo hiyo ya huo mfuko wa hizo pesa katika kuingiza wataingiza kwa kipindi hiki au kipindi gani. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yano naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza robo ipi ambayo tutaingiza fedha hili ni suala ambalo kama nilivyomuahidi kwenye jibu la msingi ni kuwa tutalifanya ndani ya mwaka wa fedha 2021/2022. Sasa suala la robo ipi tutaingiza fedha ni kutokana na hali ya fedha itakavyokuwa.

(b) Hatujapata uhakika au laa. Tunafahamu kwamba ujenzi wa barabara ya Chake Chake/Mkoani ni jambo ambalo pia linategemea mipango ya serikali. Kwa hivyo, tumhakikishie mheshimiwa kwamba serikali ikishakuamua kwamba lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza na sisi tutafanya maamuzi ya lini tutaanza kujenga soko hilo katika eneo ambalo litakuwa linafaa.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Mhe. Waziri wananchi wangu wa Ndagoni asilimia 90 ni wavuvi lakini wanapata shida wakati wa kwenda kuuza samaki wanafuata soko lilioko mbali kijiji cha Wesha, mara nyingi huwa hawaendi kuuza samaki katika soko la Wesha na pale Halmashauri au Baraza la Mji Chake Chake wanakosa mapato.

(a) Je, haoni ipo haja sasa ya kujenga soko Ndagoni ili kuwarahisishia wananchi wa Ndagoni kuuza samaki wao katika soko na Halmashauri ya Baraza la Mji Chake Chake kwa kupata faida au yale mapato yanayotakiwa.

(b) Shehia ya Ziwani walikuwa na soko lao la kudumu na sana wanapenda kula Pomboo watu wa Ziwani pale na soko lile limekufa kipindi kikubwa sana. Haoni sasa ipo haja ya wananchi wa Shehia ya Ziwani kuwarejeshea soko lile na kupata huduma hiyo ya soko katika maeneo yao.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri hili swali lilikuwa la Mtambile lakini sasa umepelekwa kwenye Soko la Ndagoni, kama unaweza kujibu nakuruhusu.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi wakati nikijibu swali la Mhe. Mohamed Mgaza Jecha kwamba serikali inao mpango wa kujenga masoko au maeneo ya kufanya biashara kwa wananchi au wajasiriamali katika maeneo yote ya Unguja na Pemba. Kwa hivyo, kwa vile sehemu anayoizungumza ya Ndagoni nayo ni sehemu ya Zanzibar ni sehemu ambayo inatumiwa na wananchi kwa ajili ya kufanya shughuli zao, tumhakikishie kwamba kadiri hali ya uchumi itakavyoruhusu basi na eneo hilo pia

tunaweza kujenga soko hilo. Hatutaki kumhakikishia kwamba tunaweza kufanya hivyo, lakini pale ambapo hali ya uchumi itaruhusu tutafanya hivyo.

(b) Soko la Ziwani ambalo lilikuwepo lakini sasa limehamishwa. Mimi nimuombe Mhe. Mwakilishi kuwa jambo hilo tushirikiane na Baraza la Mji la Chake Chake tuone sababu zilizosababisha za kuhamisha soko lile, sababu kwa vyovyote zilikuwa za msingi ikiwa kuna ulazima wa kulirejesha basi tutalirejesha. Nashukuru Mhe. Spika.

**Nam. 78**

**Athari ya Moshi Unaotokana na Kiwanda cha Makonyo**

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara (Kny. Mhe. Bakar Hamad Bakar)** - Aliuliza:-

Kiwanda cha Makonyo kilichopo Wawi ni kiwanda cha muda mrefu kinachotumika kuzalisha mafuta ya makonyo na arki za mimea mbali mbali. Kutokana na maendeleo ya jamii imepelekea kiwanda hicho kuwepo katikati ya makaazi ya wananchi.

Kwa kuwa uzalishaji wa mafuta katika kiwanda hicho hutegemea matumizi ya kuni na makapi ya makonyo ambayo husababisha utoaji wa moshi mwingi wa kati wa uzalishaji.

(a) Je, ni kwa kiasi gani serikali imefanya tathmini ya uwepo wa athari inayotokana na moshi wa kiwanda hicho.

(b) Je, serikali imeandaa njia gani mbadala ili kuweza kuzuia athari zinazojitokeza kutokana na moshi huo.

**Mhe. Kaimu Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda (Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Uchumi na Uwekezaji)** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 78 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imewahi kufanya tathmini ya uwepo wa athari inayotokana na kiwanda hicho kupitia Idara yake ya Mazingira mnamo mwaka 2012 na kuonyesha kwamba kiwanda hicho hakina haja ya kufanyiwa "*environmental auditing*" na badala yake ikatoa maelekezo kwa uongozi wa kiwanda hicho kutekeleza mapendekezo ambayo yaliwasilishwa kutokana na ripoti hiyo.

Mapendekezo hayo ni pamoja na:-

i. Kutumia kuni zenye kutoa kaboni chache
ii. Kuziba sehemu ambazo moshi unaweza kupenya kabla ya kufika katika bomba.
iii. Kubadilisha boila na kuweka lenye uwezo mdogo wa kutoa kaboni
iv. Kuwafunza wafanyakazi juu ya njia bora za kujikinga na madhara yatokanayo na moshi.

Baadhi ya mapendekezo hayo tayari yameshafanyiwa kazi na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa uwezekano wa moshi utokao kiwandani hapo kuleta athari za kiafya.

(b) Njia mbadala zilizoandaliwa na serikali ni pamoja na kuzidisha urefu wa bomba la moshi ili moshi unaotoka uweze kusafiri masafa ya mbali zaidi na hivyo kupunguza athari zinazoweza kupatikana kutokana na moshi huo pamoja na kutekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na Idara ya Mazingira katika ripoti yao ya utafiti waliofanya.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kupata fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda swali la nyongeza lenye alama (a) na (b).

(a) Mhe. Waziri je, serikali haioni kwa sasa kwa vile Kiwanda cha Makonyo kiko katikati ya makaazi ya wananchi kukitafutia sehemu nyengine na kikaweza kuboresha baadhi ya mambo kama ku-*process* karafuu zetu ili ziwe na tija zaidi.

(b) Kwa vile baadhi ya mahitaji ambayo yalihitajika kufanyiwa kazi hayakufanyiwa kazi. Je, serikali haioni kwamba bado athari ile kwa Kiwanda cha Makonyo kwa wakaazi wa Wawi, Msikiti Begi, Maabara, Kichangani, Kisunzi, Machomane wote watu hawa wanaendelea kupata kadhia ya kiwanda kile.

**Mhe. Kaimu Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda (Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Uchumi na Uwekezaji):** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Suala la kuhamisha kiwanda ni suala ambalo lina gharama kubwa sana na kuna vitu vingi ambavyo unatakiwa kuvizingatia. Hata hivyo, serikali kwa sasa hivi ipo katika mpango wa kuelekeza kila wilaya kutenga maeneo ya viwanda. Hivyo basi, mpango huo utakapokuwa umekamilika basi taratibu zitafanyika kwa ajili ya kufanya uhamisho huo, lakini naomba tuzingatie gharama kubwa ambazo zinaweza kutokezea kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

(b) Kwa yale maagizo ambayo yamebaki tutajitahidi kupitia watendaji wetu kuhakikisha kwamba yanatekelezwa.

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na nimshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake. Wakati anajibu Mhe. Waziri ameeleza kwamba kiwanda hiki kukiondoa ni gharama kubwa na ni kweli, lakini ukisikiliza swali la msingi linazungumzia suala la nishati kwa ajili ya ku-*heat* maji pamoja na makonyo kwa ajili ya kutengeneza mafuta.

Sasa swali langu lipo hapa, kuna ugumu gani kitaalamu pengine na gharama katika kuondosha mfumo wa nishati wa kuni ili tukenda katika mfumo wa nishati ya gesi kama vile ambavyo serikali imekuwa ikihimiza wananchi wetu kuachana na matumizi ya kuni twende katika matumizi ya gesi, ili kuokoa mazingira pamoja na kutafuta mambo mengine.

Swali langu hili naliuliza kwa sababu miongoni mwa majibu yake Mhe. Waziri amesema kuna aina ya kuni ambazo zina kaboni kidogo. Sasa hofu yangu wananchi wetu sio wengi ambao watakuwa na uwezo wa kubaini kuni ambazo zina kaboni kidogo. Kwa hivyo, swali langu ni kwamba je, serikali ina mpango gani wa kubadilisha mfumo wa nishati kutoka katika mfumo wa kuni kwenda katika mfumo wa gesi ambao una hakika athari za kimazingira zitakuwa ndogo na kiwanda kitaendelea kuleta tija na malengo ya serikali yataweza kufikiwa. Mhe. Spika, nakushukuru.

**Mhe. Kaimu Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda (Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Uchumi na Uwekezaji):** Mhe. Spika, ahsante naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Tunalichukua pendekezo hilo la matumizi ya gesi ni wazo zuri na tutawasilisha kwa wataalamu ili kuona namna gani tunaweza tukalitekeleza.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi na mimi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

(a) Kwanza Mhe. Spika, napenda nimuulize Mhe. Waziri yeye tayati ameshafanya ziara wakati alipokwenda Pemba aliwahi kukagua Kiwanda hiki cha Mafuta ya Makonyo wakati kinafanya kazi zake.

(b) Tumeshuhudia mara nyingi serikali kuzidisha urefu wa bomba, lakini ningependa kujua je, kwa mara hii serikali imejipangaje katika kuboresha bomba lile kwa sababu wananchi wa vijijini pale Wawi wanaathirika sana na moshi ule. Mimi mwenyewe Mhe. Spika, ni shahidi nilikwenda hivi juzi nikakaa pale nazungumza na watu nikaona ule moshi unavyokuja. Je, serikali au wizara yake imejipangaje mara hii katika kuboresha bomba hili ili wananchi wetu wasiathirike. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Kaimu Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda (Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Uchumi na Uwekezaji):** Ahsante Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo. Ziara ya kwenye kiwanda bado sijaifanya, ikumbukwe tu kwamba hii ni wizara ambayo ninaikaimu kwa hivyo nimekuwa nikifanya ziara nyingi zaidi katika wizara yangu mama ambayo ninaisimamia. Lakini hata hivyo, nitapanga muda makhsusi kabisa ili niweze kukitembelea hicho kiwanda na kwenda kujionea mwenyewe hali halisi ya hilo eneo.

Kuhusu suala la kuboresha bomba nafikiri linajijibu katika swali la msingi kipengele (a) kuanzia mapendekezo yaliyotolewa moja mpaka nne. Nashukuru Mhe. Spika.

**Nam. 57**

**Kukithiri kwa Wizi wa Mazao na Mifugo**

**Mhe. Habibu Ali Muhamed** - Aliuliza:-

Wananchi wengi hasa wa kipato cha chini hutumia rasilimali nguvu zao kwa shughuli za kilimo na mifugo, lakini hawafaidiki kutokana na tatizo la wizi na uharibifu unaofanywa na baadhi ya watu.

(a) Je, unawahakikishiaje wananchi juu ya uwepo wa sheria za kudhibiti wizi wa mifugo na mazao.

(b) Je, kuna utaratibu gani wa sheria ambao utawawezesha waathirika kupata haki ya fidia ukiachia mbali kuadhibiwa kwa mtendaji wa kosa hilo kijinai.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo** - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 57 lenye kifungu (a) na (b) naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo. Kwanza namshukuru kwa swali lake.

Mhe. Spika, ni kweli wananchi wengi hasa wa kipato cha chini hutumia rasilimali nguvu zao kwa shughuli za kilimo na mifugo, lakini hawafaidiki kutokana na tatizo la wizi na uharibifu unaofanywa na baadhi ya watu.

(a) Mhe. Spika, tunawahakikishia wananchi juu ya kuwepo kwa Sheria ya Makosa ya Adhabu *(Penalty Code)* Namba 6 ya mwaka 2018 ambapo katika kifungu 268 na vifungu vidogo (1), (2) na (3) vinafafanua makosa pamoja na aina ya mazao ya kilimo.

(b) Mhe. Spika, utaratibu wa sheria ambao utawawezesha waathirika kupata haki ya fidia ukiachia mbali na kuadhibiwa kwa mtendaji wa kosa hilo la kijinai umefafanuliwa katika kifungu kidogo (1) ambapo mkosa wa kosa la wizi wa mazao atahukumiwa kifungo kisichozidi miaka mitano na pia atatakiwa kulipa mara mbili ya bei ya soko la mazao husika.

Mhe. Spika, mapato yatakayopatikana yatagawanywa sawa sawa baina ya mmiliki wa mazao na serikali.

Mhe. Spika, tafsiri ya mazao ya kilimo katika sheria hii imejumuisha wanyama wa jamii ya ndege, haikujumuisha wanyama wenye miguu minne kama vile mbuzi na ng’ombe. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Habibu Ali Muhamed:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniruhusu niulize swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kuna mkulima mmoja katika Shehia ya Piki jimbo la Mtambwe alipata athari ya kuunguliwa mikarafuu yake pamoja na minazi yenye ukubwa wa eneo la ekari sita. Kwa bahati nzuri Makamu wa Pili wa Rais Mstaafu, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi pamoja na Waziri wa Kilimo walishiriki katika kazi ya kumuunga mkono kupanda miche katika shamba lile na alipelekwa Afisa wa Kilimo kufanya tathmini ilikuwa kama shilingi 14 milioni.

Je, nimuulize Mhe. Waziri mkulima huyu tutaweza kumsaidiaje ili shamba lake liweze kurudi katika hali ya kawaida, kwa vile yeye ni mkulima mzuri wa mikarafuu.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Mhe. Spika, naomba nimjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi. Kwa kweli hilo suala tutalifuatilia na tuone jinsi gani ya kuweza kumsaidia huyo mwananchi. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Said Saleh Salim:** Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Mhe. Spika, kunakuwa na mgongano kati ya wakulima na wafugaji wa mifugo jamii ya ndege aina ya kuku, mabata na wengine. Mara nyingi wakulima wanapoharibiwa vilimo vyao na jamii ya ndege kunakuwa hakuna hukumu, kuku anapoharibu kilimo kama viazi, mihogo na vitu vyengine hawapati hukumu inayoridhisha wakulima au majibu mazuri kwenye kesi hizi.

Je, Mhe. Waziri suala hili wizara yake inaliangalia vipi.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza la kwamba kuku na ndege ambao wanaharibu. Hili nafikiri ni kuweza kukaa wanajamii kwa pamoja na kuunda sheria ndogo ndogo ambazo zitaweza kuhakikisha kuwa wanyama hao wasiweze kuharibu. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa serikali ilishapitisha sheria mbali mbali ambazo zinaweza zikasaidia tatizo ama kupunguza wizi wa mazao na mifugo katika nchi yetu ambayo kila pembe ya nchi yetu naona kwamba ni kilio kikubwa juu ya kadhia hii.

Je, Mhe. Waziri watendaji wake watakaa na taasisi nyengine katika kuzijengea uelewa sheria hizi ili wananchi wetu waweze kuzitambua. Ni lini serikali itafanya kazi hiyo wakati sheria hizi zipo. Kwa mfano, sheria ile ya mifugo namna ya kusafirisha mfugo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine, lakini vile vile tukijua kwamba wezi au watu hao wanaojishughulisha na vitendo hivi mara nyingi hawatumii *document* za serikali na hawaulizwi chochote kwa sababu ni utaratibu ambao umeshazoeleka.

Je, kwa kuwa serikali imezitunga sheria hizo kwa gharama kubwa na watendaji wetu hawawajibiki wakiwemo wa wizara yake na wizara nyengine, ni lini serikali itawawajibisha watendaji hawa sambamba na kutoa taaluma.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi Shamata Shaame Khamis ambaye ni mwanafunzi wangu kwa taarifa zenu. Kwanza nimjibu kwamba tutawapatia mafunzo pale tu hali itakaporidhisha ya kifedha tutawapatia mafunzo, ili kuhakikisha kwamba sheria hizo wanazifuata na kama tukishakuwapatia mafunzo basi ambaye hatowajibika basi tutamuwajibisha ipasavyo ili ahakikishe kwamba kazi hii inafanyika kwa ufanisi na kuwapa moyo wananchi katika vipando vyao. Ahsante Mhe. Spika.

**Nam. 16**

**Mradi wa Maji kwa Wilaya ya Magharibi “A” na “B”**

**Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Kny. Mhe. Machano Othman Said)** - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa katika majadiliano na Serikali ya India kupitia Benki ya *EXIM* kuhusu Mradi wa Maji kwa Wilaya za Magharibi "A" na "B". Kwa kuwa ni muda mrefu sasa wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wakiusubiri mradi huo.

(a) Je, ni lini mradi huo unatarajiwa kuanza kutekelezwa.

(b) Mradi huo unatarajiwa kugharimu kiasi gani cha fedha.

**Mhe. Waziri wa Maji na Nishati** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali Nam. 16 lililoulizwa na Mhe. Machano Othman Said Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini

(a) Mradi wa uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji wa Maji Zanzibar kupitia *EXIM Bank*, ya India umetiwa saini mwezi Julai 2020, na unatarajiwa kuanza kazi ndani ya robo ya tatu (Januari- Machi 2021) na utekelezaji wake utachukua kipindi cha miezi 18.

(b) Mradi huu unagharamiwa kwa Mkopo kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya Uagizaji na Usafirishaji ya India *(EXIM Bank India)* na mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), ambapo jumla ya Dola za Kimarekani *(USD)* Milioni 92.18 zinatolewa kwa Serikali ya Tanzania na *EXIM Bank* ya India na Mchango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) utatolewa kupitia Wizara ya Nchi, Fedha za Mipango.

**Mhe. Yussuf Hassan Iddi:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza maswali ya nyongeza mawili kama ifuatavyo:

(a) Kwa kuwa amesema kwamba Mradi huu wa *EXIM Bank* unagharamiwa na wafadhili pamoja na SMZ. Je, ni kiasi gani cha SMZ cha fedha kitatoa katika mradi huo.
(b) Kwa kuwa miradi mingi ya maji iliyopita haikuwa na ufanisi mzuri. Je, Mhe. Waziri anahakikishia vipi wananchi wa Magharibi A na B ambapo mradi huu utapita kwamba mradi huu utakuwa na ufanisi na tija na malengo yaliyokusudiwa yatapatikana. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Maji na Nishati:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza. Mhe. Spika, kiasi cha fedha kilichotolewa na SMZ, naomba hili Mheshimiwa nililete kwa maandishi baada ya kupata ile *break down* kutoka kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Fedha na Mipango hilo nitalileta Mheshimiwa.

Mhe. Spika, la pili nikiri kwamba miradi mingi ya maji imekuwa na changamoto na tija yake imekuwa ndogo, lakini niwahakikishie kwamba Mradi wa *EXIM* ambao unagharimu dola milioni 92. Serikali kupitia Wizara ya Maji, Nishati na Madini, imejipanga kuhakikisha kwamba mradi huu utakuwa na tija, tunaufatilia mradi ngazi kwa ngazi tunau-*monitor* kuhakikisha kwamba, yale ambayo yalikuwa yanatokea katika miradi mengine ikiwemo kupata mashine zisizokuwa za uhakika halitokei tena katika mradi huu.

**Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma:** Ahsante Mhe. Spika na mimi kwa kuniona, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, nataka akubaliane na mimi Mhe. Waziri

kwamba kuna maeneo ya Jumbi, Tunguu, Kibele na Cheju wananchi wake hawajawahi kupata huduma ya maji safi na salama tangu zimeanzishwa huduma hizi, na ukizingatia Mhe. Rais amesema maneno yake naomba ninukuu "Sasa hivi wananchi wanataka Matunda ya Mapinduzi na sio simulizi za mapinduzi"

Je, ni ipi kauli ya serikali ili kuona wananchi hawa wanawatatulia tatizo hili na kuwatua wanawake na watoto ndoo ya maji kichwani.

**Mhe. Waziri wa Maji na Nishati:** Mhe Spika, kwa ruhusa yako naomba nijibu swali la nyongeza la Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma. Kwanza naomba nikiri kwamba, changamoto ya maji katika maeneo aliyoyataja ipo lakini serikali imejipanga kutatua changamoto hizo kwa sababu mradi ambao nimeueleza wa *EXIM Bank* unapita pia katika maeneo hayo, ambao utajumuisha ujenzi wa matangi, uondoaji wa mabomba chakavu pamoja na kuweka miundombinu mipya ya maji kuhakiksha kwamba huduma hii ya maji inapatikana vizuri.

**Mhe. Miraji Khamis Mussa**: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, lakini naiomba sana serikali kwenye mradi huu watupe majibu yaliyo sahihi kwa sababu kauli ya serikali ya mwanzo ni mradi ambao uko katika Mkoa wa Mjini na Magharibi. Kauli ya pili inakuja unaenda mpaka Cheju maana mwisho utafika Upenja na juzi ulifika Mahonda lakini naomba niulize swali la nyongeza,

(a) Katika utekelezaji wa Miradi ya Serikali mara zote huwa ina-*delay*. Mhe. Waziri, sisi tunajua mradi unataka kuanza lini na umalize lini, hebu tupe hasa *status* ya mradi huu.
(b) Kuna mchakato ulipoendeshwa mligawa *lot* kwa utaratibu maalum, hebu tupe zile kampuni zilizoshinda na utekelezaji wa zile *lot* katika mradi huu. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu maswali mawili ya Mhe**.** Miraji Khamis Mussa. Mhe. Spika, *status* ya mradi upo kwenye utekelezaji, na naomba nimwambie au nimueleze Mheshimiwa Mwakilishi kwamba tayari *contractors* wameanza kuleta vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Baadhi ya vifaa vimeshafika, kuna mambo mengine ambayo bado yapo njiani kuletwa. Kwa hiyo, mradi *status* yake kwamba utekelezaji umeanza na baadhi ya vifaa pamoja na kukabidhiwa maeneo ya kuanza kazi kwa wakandarasi.

Mheshimiwa ni kweli kwamba, mradi huu una *lot* tatu, kuna kampuni tatu anbazo zimeshinda katika mradi huu. Moja ni *Afcon Company* ya India, *Mega Company* pia ya India lakini nyengine ni *L&T* pia ya India.

**Nam. 49**

**Utekelezaji wa Ahadi ya Serikali katika Mradi wa Uwekaji wa Mabomba Mapya ya Maji**

**Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa** - Aliuliza:-

Katika kipindi cha miaka 10 kumekuwa na juhudi kubwa za uchimbaji wa visima na ujenzi wa matenki ya maji. Hata hivyo, pamoja na kufanyika kwa kazi hiyo, bado katika baadhi ya maeneo,

wananchi wa Mkoa wa Mjini Magharibi wanakabiliwa na upungufu wa maji safi na salama, hali ambayo inaleta shida kubwa kwa maendeleo yao.

(a) Je, kwanini pamoja na kuwepo juhudi ya uchimbaji wa visima na ujenzi wa matenki ya maji, bado kuna shida ya upatikanaji wa maji.

(b) Je, ahadi ya serikali kupitia Baraza la Wawakilishi imefikia hatua gani katika mradi wa kuweka mabomba mapya ya maji maeneo ya mjini.

**Mhe. Waziri wa Maji na Nishati** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali Nam. 49 lililoulizwa na Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa swali lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, juhudi za serikali katika kuondoa tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji Mkoa wa Mjini Magharibi umegawika katika maeneo matatu, eneo la mwanzo ni la utekelezaji wa mradi wa *AfDB* ambao tayari umekamilika kwa kuwahudumia wananchi wa Shehia za Mji Mkongwe na Ng’ambo ya zamani. Eneo la pili ni eneo la utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Usambazaji wa Maji wa *EXIM Bank* wa India ambao utekelezaji wake unatarajiwa kuanza ndani ya mwaka huu wa fedha ambao nao utawanufaisha wananchi wa maeneo ya Shehia za Kama, Mfenesini, Mwakaje, Chuini, Mbuzini, Kihinani, Dole, Kizimbani, Bububu, Mwanyanya, Kibweni, Sharifumsa, Masingini, Chaani, Kianga, Mwera, Ubago, Jumbi, Tunguu, Fuoni Kibondeni, Fuoni Kijitoupele, Pangawe, Kinuni, Magogoni, Mwanakwerekwe, Melinne, Tomondo, Maungani, Kisauni, Shakani, Chukwani, Nyamanzi, Kombeni, Dimani, Bweleo na Fumba. Eneo la tatu ni utekelezaji wa mradi wa maji wa *JICA* ambao huu bado upo katika makubaliano ya kimkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Japan.

Hivyo, kukamilika kwa miradi hiyo kutapunguza kwa kiwango kikubwa tatizo la upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi na maeneo mengine.

**Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi niseme nimesikia majibu ya Mhe. Waziri lakini kidogo bado hajaniweka sawa ndani ya Mkoa wangu. Mhe. Spika, Mhe. Waziri amesema tayari mradi wa kwanza umeshakamilika ndani ya Mkoa wa Magharibi lakini ambao kuwa eneo la mjini hasa Ng’ambo nataka kumwambia Mhe.Waziri.

(a) Je, anajua upande wa Ng’ambo Jimbo la Kwamtipura, Chumbuni, Mpendae na Amani ya kuwa mabomba yaliyokuwemo mkipiga maji, maji yote yanamwagika.
(b) Ni lini sasa fundi wako utawaleta kuja kutengeza bomba hili ili wanawake wafaidike na uwatue ndoo wanawake wa Wilaya ya Mjini.

**Mhe. Waziri wa Maji na Nishati:** Mhe. Spika, naomba kwanza kwa heshima na taadhima na unyeyekevu nikubaliane na hoja na swali la Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa, kwamba kweli kuna matatizo ya mabomba katika maeneo aliyoyataja lakini pamoja na maeneo mengine. Juhudi za serikali kupitia Mamlaka ya Maji *ZAWA* ni kuendelea kubadilisha miundombinu hiyo. Lakini

nimwambie kwamba niko tayari kuja na kuwaleta mafundi katika eneo hilo kwa ajili ya kuyashughulikia.

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Ahsante sana Mhe. Spika, nikushukuru kwa hekima na busara zako hao wengine wanafanya fitna. Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi ya kumuliza Mhe. Waziri swali moja lenye kifungu (a) na (b)

Swali langu la kwanza ni kwamba Mhe. Waziri nadhani ipo haja ya kufanya utaratibu na njia nyengine nzuri zaidi itakayotupa tija kwa wananchi wetu. Serikali mara zote ilikuwa ikihangaika na kuchukua twakimu za uzalishaji wa maji, lakini wawakilishi wote hapa hoja yetu sisi ni upatikani wa maji, inaonekana kuna jambo halijakaa vizuri. Takwimu za serikali mara nyingi zinakuwa ni uzalishaji wa maji lakini changamoto ya watu ni upatikanaji wa maji.

Sasa swali la mtangulizi wangu alichokuwa akikisema kwamba uzalishaji wa maji inawezekana ukawa unafanyika mkubwa, lakini upatikanaji wa maji kwa jamii ukawa uko mdogo na serikali ikawa inatumia jitihada na gharama kubwa katika kutafuta nguvu za uzalishaji wa maji. Lakini upatikanaji wa maji unakuwa mdogo na hasa kutokana na miundombinu kuwa imechoka ama dhaifu. Swali la kwanza kwamba:

(a) Je, serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba haya yanakamilika vizuri ili kutathmini kile ambacho kinatumika katika uzalishaji hivyo hivyo kiwe kinapatikana katika wale watumiaji.

(b) Katika mradi ambao umeutaja wa *EXIM Bank* umesema una *lot* tatu, na kwa mujibu wa vijiji ulivyovitaja uko *scattered* mradi wenyewe. Je, Mhe. Waziri anaweza kutusadia zile *lot* kwa maana kwamba zina uwezo ndizo ambazo zimegawanya kimaeneo au mtawanyiko wake uko jumla jamala. Mhe. Spika, nakushukuru.

**Mhe. Waziri wa Maji na Nishati:** Ahsante Mhe. Spika, kwanza naomba pia nikiri kwa yale ambayo yameelezwa na Mhe. Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Chwaka. Mheshimiwa serikali ina mpango wa kuhakikisha kwanza kufanya tathmini. Sasa hivi tunafanya tathmini ya nani anapata maji na nani hapati maji, lakini nani ameungiwa maji na nani hawajaungiwa ilin tuweze kujua *production.* Lakini kuhakikisha kwamba tunajua tunapata tathmini halisi ya maji.

Mhe. Spika, kwenye mradi ambao nimeueleza tuna mpango wa kufunga mita kwa wale wote ambao tutawaungia maji ili tuweze ku-*manage* ile *production* ya maji na ukosefu wa maji. Hivi sasa kupitia ngazi za mikoa wilaya na shehia tunafanya tathmini ya nyumba kwa nyumba kujua wapi kuna maji na wapi hakuna maji.

Mhe. Spika, eneo la *lot* hili kwa kweli naomba nililete sijalipata hasa ile *concept* naomba labda arudi kidogo anisaidie.

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Mhe. Spika, katika Mradi wa *EXIM Bank* wa India Mhe. Waziri ameeleza kwamba kuna *lot* tatu, lakini eneo la mradi ni eneo kubwa. Swali langu niliuliza kwamba katika zile *loti* tatu, kwa mfano *lot* A itashughulikia vijiji hivi, *lot* B itashughulikia vijiji hivi na *lot* C

itashughulikia vijiji hivi. Ule mgawanyo ukoje au *lot* hizi zote kwa ujumla zitakuwa zinashughulikia katika maeneo yote. Ndio swali langu mimi.

**Mhe. Waziri wa Maji na Nishati:** Ahsante, Mheshimiwa *lot* hizi tatu zimegawika katika utaratibu ufuatao. Kuna *lot* ambayo inajumuisha ujenzi wa matangi, kuna *lot* inayojumuisha ulazaji wa mabomba pamoja na ujenzi wa ofisi na nyengine ambayo inahusiana na, Mheshimiwa naomba kwa ruhusa yako hili bora nililete kwa maandishi kwa sababu linahitaji takwimu. Nitakuja kudanganya Mheshimiwa na sitaki kudanganya baraza lako. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa sababu upo kwenye visima vya maji.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh:** Mheshimiwa nikushukuru hata nilikuwa sitaki kuinuka lakini Mheshimiwa kwa sababu mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Welezo na Welezo maana yake ni eneo la visima vya maji. Lakini cha kusikitisha kwamba maji yote yapo Welezo lakini wana Welezo sisi hatupati maji yanakwenda mjini kwa Mheshimiwa hapa na anajisifu hapa maji yanatoka kama mvua.

Lakini kilichonifanya niinuke Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametaja huu Mradi wa India ametaja maeneo yote lakini nashangaa kwamba hapo Welezo haijatajwa ndio hayo maji yote yanakuja hapo halafu *dissseminated* kwa watu wengine. Sasa Mheshimiwa nataka nimwambie kwamba wana wa Welezo hilo hawalitaki na wananuna sana. Mna mkakati gani kwa kuhakikisha kwamba yale maji yanakuja Welezo lakini kwanza wafaidike wana wa Welezo wapate maji kwa sababu ndio hawapi maji hilo la kwanza.

Mhe. Spika, la pili, nataka kujua mkakati wa serikali dhidi ya kuyaziba haya mabomba ambayo yanavuja kwa sababu mabomba mengi ukitaka kuyaona njoo kule mtoni Welezo nikupitishe kunako mito uone jinsi maji ya mvua hayapo lakini sasa maji ya mbomba yaliyovuja ndio yamejaa na athari kubwa Mheshimiwa ni hatari kuja kupinduka maradhi ya Kipindupindu. Yanavuja sana na taarifa tushatoa sana lakini bado Mheshimiwa taarifa hazifanyiwi kazi. Sasa mkakati gani wa kuziba haya mabomba.

**Mhe. Waziri wa Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la Mhe. Hassan Khamis Hafidh swali (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa nikiri kwamba kumekuwa na kilio kikubwa kwa wana wa Welezo kwa kukosa huduma hii muhimu ya maji na hii nayo inachangia pia na hili swali lake la pili la uchakavu wa miuondombinu ile ya kizamani ambayo maji mengi yanapotea katikati. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mwakilishi kwamba tumejipanga kuhakikisha kwamba tunaondoa hii mivujo yote inayosababisha upotevu wa maji ikiwemo Welezo, lakini pia tuna mradi mdogo wa India ambao uta-*serve* katika yale maeneo mengine ambayo sikuyaainisha. Kwa hiyo eneo la Welezo litaingia katika mradi huo.

**Nam. 9**

**Utekelezaji wa Malengo ya Shirika la Meli kwa Safari za Ndani na Nje ya Zanzibar**

**Mhe. Mussa Foum Mussa -** Alijibu:-

Katika malengo yake ya Bajeti ya Mwaka 2020/2021, Shirika la Meli lilipanga kufanya safari 120 za ndani na safari 6 za nje ya nchi (Comoro na Msumbiji) kwa kutumia meli zake mbili za MV. Mapinduzi II na MV. Maendeleo.

(a) Je, Mhe. Waziri malengo hayo anayafahamu.

(b) Je, malengo hayo ya safari yamefikiwa vipi mpaka sasa.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 kama ifuatavyo. Lakini kabla sijenda kujibu swali lake kwanza naomba kutoa maelezo ya swali.

Itakumbukwa kwamba mnamo mwezi wa Disemba, 2015 Meli ya MV Mapinduzi II ilifika Zanzibar kutoka Nchini Korea ambako ndiko ilipotengenezwa. Mnamo tarehe 8 Januari, 2016 meli ya MV Mapinduzi II ilianza safari zake za kawaida za kusafirisha abiria kutoka Unguja kwenda Pemba na ilipofika tarehe 11 Oktoba meli ilijitokeza hitilafu katika *engine* zake zote mbili na kufanyiwa matengenezo.

Mhe. Spika, ilipofika tarehe 4 Septemba 2017 meli hiyo ilijitokeza hitilafu za kiufundi kwa mara nyengine. Hitilafu za mara kwa mara katika meli hiyo na kukosa kufanya kazi kikawaida. Hiyo ni kwa upande wa MV Mapinduzi II kwa sababu swali linaeleza Mapinduzi na Maendeleo.

Mhe. Spika, kwa upande wa MV Maendeleo, meli hiyo ilifika nchini mnamo mwaka 1980 ambapo kwa sasa meli hiyo ina miaka 40. Meli hii imefanya kazi zake kwa muda mrefu bila ya kujitokeza changamoto zozote isipokuwa tu inafanyiwa *service* za kawaida, lakini ilipofika 2017 ilionekana imekataa kufanya kazi. Ndipo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kuipeleka mchelezoni kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho makubwa kwa sababu ilikataa kabisa. Hayo ndio kwa upande wa maelezo.

Mhe. Spika, sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo, ilikuwa kitoto (a) na (b)

a) Mhe. Spika, malengo ya bajeti ya mwaka 2020/2021 ya Shirika la Meli nayafahamu.

b) Mhe. Spika, malengo ya bajeti ya mwaka 2020-2021 hayakufikiwa kwa kuwa mpaka sasa ikiwa ni nusu mwaka Meli ya MV Mapinduzi II imeweza kufanya safari moja tu ya ndani kutoka Unguja kwenda Pemba. Sababu iliyopelekea kutofikiwa malengo hayo ni kutokana na hitilafu za mara kwa mara zinazotokea katika injini za meli ya MV Mapinduzi II. Hitilafu hizo husababisha meli kutoweza kusafiri katika safari zake za kawaida ambazo zimepangwa.

   Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi sita kuanzia Julai – Disemba, 2020 meli ya MV Maendeleo ilitarajiwa kwamba matengenezo yake yatakamilika. Hata hivyo, meli hiyo haikuweza kufanya kazi kwa sababu matengenezo ya meli hiyo hayajakamilika kama ilivyotarajiwa. Ahsante nashukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Mussa Foum Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri kakiri kwamba meli hii tokea ilipokuja ina tatizo la *engine*, sasa nimuulize Mhe. Waziri.

a) Je, serikali ina mpango gani kabambe wa kuliondosha tatizo hili la *engine* ili kuona kwamba meli hii inafanya safari zake za kawaida.
b) Kwa kuwa Mhe. Waziri katueleza kwamba MV Maendeleo bado ipo kielezoni Mombasa na kwa kuwa tulitarajia baada ya miezi 6 meli ile itarudi. Je, tutegemee lini meli hii itafika hapa Zanzibar. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

a) Swali lake lilikuwa linahusiana na Mpango Mkuu wa Serikali ambao utatengeneza meli ya MV Mapinduzi II na kuanza safari zake za kama kawaida. Kwa upande wa serikali kwa sasa tumeamua kumleta mtaalamu kutoka nje ili aje aifanyie uchunguzi wa kina kabisa meli hiyo, tujue ina tatizo gani na baadae tutajua nini tufanye. Lakini hatua iliokuwepo sasa hivi ni kumtafuta huyo mtaalamu aje kuifanyia matengenezo hiyo meli.
b) Kwa upande wa MV Maendeleo iliyokuwepo chelezoni Mombasa, ilipopelekwa ilikuwa ina tatizo dogo, lakini baada ya kukaa pale imeonekana ina tatizo kubwa. Kwa hivyo, serikali inatatufa fedha ya kuifanyia matengenezo kutokana na hilo tatizo kubwa lililoonekana. Ahsante Mheshimiwa. *(Makofi)*

**Mhe. Nassor Salim Ali**: Ahsante Mhe. Spika kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika majibu yake Mhe. Waziri ameeleza kwamba meli ya MV Maendeleo ipo Mombasa na ipo katika matengenezo. Je, ni gharama ngapi za fedha ambazo zitatumika kwa serikali kutengeneza meli hii.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Nassor Salim Ali swali lake la nyongeza. Kwa upande wa gharama naomba nimletee kwa maandishi kwa sababu sizijui. *(Makofi)*

**Mhe. Juma Ali Khatib:** Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kwa kunipa nafasi. Mimi nataka kumuuliza Mhe. Waziri haoni kwamba tunaendelea kuitia hasara serikali kwa meli hii kwa kutumia *engine* ya *wartsila* ambapo *engine* hizi zina matatizo, na pendekezo ilikuwa kwamba meli hii iwe na engine ya *caterpillar*. Ana mpango gani sasa wa kwamba engine hii itolewa itiwe *engine* ya *caterpillar* ili kuepusha gharama kubwa tunazoibebesha serikali yetu.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhsa yako naomba kumjibu Mhe. Juma Ali Khatib swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kama nilivyosema mwanzo serikali hivi sasa imeagiza mtaalam kutoka nje ili kuja kufanya uchunguzi. Kwa hivyo, yeye atatuambia mashine gani itafa nya kazi, ikiwa *wartsila* au *caterpillar*. Mtaalam atatuambia. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa pamoja na umuhimu wa swali hili sitaki kutoa swali la upendeleo. Mheshimiwa nenda kapumzike.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Nashukuru.

**Nam. 81**

**Kuelimisha Kuhusu Uchumi wa Buluu Zanzibar**

**Mhe. Aza Januar Joseph -** Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya awamu ya nane imejielekeza sana katika kujiongezea kipato chake kupitia uchumi wa buluu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaelimisha wanafunzi kuhusu uchumi wa buluu ili kupata wataalamu watakaoweza kuendeleza uchumi huo.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 81 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ina mpango wa muda mfupi na muda mrefu wa kuwaelimisha wanafunzi na wananchi mbali mbali kwa kuwapatia mafunzo ya kinadharia na vitendo ili kuendeleza uchumi wa buluu. Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano (2020 – 2025) kupitia Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, unalenga kutoa mafunzo na nyenzo kwa wajasiriamali wa uvuvi na mazao mengine ya baharini. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa vyuo vya elimu ya amali huko Mtambwe Pemba na Makunduchi Unguja ambapo mbali na taaluma nyenginezo, vyuo hivyo vitakuwa na mtaala wa fani ya uvuvi .

Mhe. Spika, katika mpango wa muda mrefu, serikali ya awamu ya nane ina mpango wa kuanzisha au kujenga Chuo Kikuu kitakachotoa elimu ya uvuvi na ubaharia. Ahsante mheshimiwa.

**Mhe. Aza Januar Joseph:** Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu mazuri lakini naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa uchumi huu umeshaanza na tayari watu wameshajikita katika kuona kwamba hata kama tayari walikuwa wanafanya kazi zao lakini hii elimu ya uchumi wa buluu imeshaingia kwenye akili yao. Je, serikali itaanza lini mafunzo haya hususan kwa wajasiriamali na wavuvi.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Aza Januar Joseph swali lake la nyongeza. Ni kwamba masuala ya kuwaelimisha wavuvi yameanza. Tumeanza kuwaelimisha wavuvi katika masuala haya kwa kutumia *workshop* yaani makongamano na tunaendelea kwa sababu hili ni suala endelevu. Kwa hivyo, tunaendelea mheshimiwa.

**Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir:** Ahsante Mhe. Spika, hongera Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwasaidia taluuma wavuvi wadogo wadogo, ni upi mkakati wa serikali wa kuwasaidia ama kuwaongezea taaluma katika uvuvi wenye tija kupitia *fishing ground.*

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Hebu rudia kidogo huko mwisho.

**Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir:** Kwa kuwasaidia taaluma wavuvi wadogo wadogo ni upi mkakati wa serikali wa kuwaongezea taaluma wavuvi katika uvuvi wenye tija kupitia *fishing ground.*

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Mheshimiwa kama nilivyoeleza mwanzo kwamba suala la taaluma ni endelevu na tunaendelea na kila baada ya muda huwa tunatoa warsha, makongamano na tunawatembelea wavuvi wenyewe katika maeneo yao.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Ahsante sana Mhe. Spika, Taaluma hii ya uchumi wa buluu katika kipengele cha uvuvi, kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba wanaendelea kuitoa, lakini kutoa taluuma ni jambo jengine, jambo moja lakini kufanya kazi ni jambo tufauti. Hivi tunavyozungumza Mhe. Spika, ni kwamba kuna baadhi ya wavuvi hususan wanaokwenda kuvua baharini katika maji ya kati, lakini kunakuwa kuna *either boundary* au vipi na wenzetu wa Tanzania Bara, na mara nyingi wale wavuvi wanakamatwa na kuharibiwa vyombo vyao kwa kuambiwa kuwa tayari wamekiuka sheria katika maeneo hayo.

Je serikali imejiandaa vipi kukaa na wenzetu wa wizara inayohusiana na uvuvi kwa upande wa Tanzania Bara, kuona kwamba dhana nzima ya uchumi wa buluu kwa Zanzibar inafanikiwa kwa kuondoa hivi vikwazo ambavyo vinawapata wavuvi wanapokwenda kuvua na inavyosemekana wakiingia katika maji ya wenzetu Tanzania Bara.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante, naomba kumjibu Mhe. Saada Mkuya Salum swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa kwamba Wizara yangu pamoja na Wizara ya Uvuvi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tupo karibu sana, na kwa kila baada ya muda fulani huwa tunakutana. Mheshimiwa kwa taarifa tu ni kwamba tarehe 5 mwezi huu ilikuwa tuwe na kikao, lakini kwa bahati mbaya shughuli hazikuwa kuruhusu. Kwa hivyo, tumepanga mwisho wa mwezi huu tutakutana kuzungumzia masuala ambayo ni *common* baina ya sisi na wao.

**Nam. 35**

**Changamoto Zinazowakabili Wavuvi na Wachuuzi Kutokana na Kuchelewa kwa Ujenzi wa Soko la Malindi**

**Mhe. Hassan Hamad Omar** – Aliuliza:-

Serikali iliweka azma ya kujenga soko la kuuzia samaki Malindi kwa muda wa mwaka mmoja. Lakini hadi sasa imepita miaka mitatu hata msingi wa ujenzi haujaanza.

a) Je, ni lini ujenzi huo utaendelezwa na soko hilo litakamilika na kuanza kutumika.

b) Je, ni lini shida na usumbufu wanaopata wavuvi na wachuuzi utaondoka na kumalizika.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 lenye kifungu a) b) na c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali bado inaendelea na azma yake kwa kutekeleza ujenzi wa Diko na Soko la samaki Malindi. Aidha, mradi huo unatekelezwa kwa awamu (*Phase*) mbili ambazo ni *Phase 1:* Ujenzi wa Eneo la Kuegeshea vyombo vya uvuvi *(Architecture works)* ambayo inatekeleza kwa msaada wa Serikali ya Japan (*JICA*) na *Phase 2:* Ujenzi wa Jengo – Ofisi na sehemu za biashara na ukarabati wa soko la zamani *(Building works)* ambayo inatekelezwa kwa fedha kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa msaada wa Serikali ya Japani (*JICA*)

Hivyo, Awamu ya kwanza *(Phase 1)* imekamilika kwa asilimia 95 ambapo eneo la kuegeshea vyombo limeshajengwa na kazi iliyobakia ni kusafisha na kuondoa vitu vilivyokua vikitumika wakati wa ujenzi (*temporal piles).*

Kwa awamu ya pili *(Phase 2)*, utayarishaji wa ujenzi wa jengo la Afisi na maeneo ya kuuzia samaki umeanza kwa kujenga mashimo mawili ya kuhifadhia maji taka *(2 Septic Tank).* Aidha, jumla ya matofali 10,000 yameshatayarishwa kwa ujenzi wa jengo la Afisi na sehemu ya kuuzia samaki.

Kutokana na kuzuka kwa Janga la *COVID 19*, Tarehe 2 April, 2020, Ubalozi wa Japan kupitia *JICA* uliwataka wakandarasi pamoja na washauri elekezi (wataalamu) ambao ni raia wa Japani na wanaotekeleza miradi inayopata misaada ya Serikali ya Japani kurudi nchini mwao. Wajenzi hao hadi hivi sasa bado hawajapata ruhusa ya kurudi nchini Tanzania.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ujenzi huo wa diko na soko la samaki la Malindi unatarajiwa kuendelea kuanzia mwezi wa Machi 2021 na kukamilika mwezi wa Febuari 2022. Hatahivyo, hivi sasa taratibu za maandalizi ya kurudi watalaamu (wakandarasi na washauri elekezi) zinafanyika ili kuendelea na ujenzi huo. Aidha, utaratibu huu utategemea hali halisi ya maradhi ya *COVID 19* katika nchi zao.

b) Mhe. Spika, Usumbufu wanaopata wavuvi na wachuuzi utaondoka na kumalizika mara ya soko hili kuanza kufanya kazi. Hivyo, ninawashauri wananchi waendelee kutoa ushirkiano na kuwa wastahamilivu katika kipindi hiki hadi tutakapokamilisha ujenzi huo.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mheshimiwa nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Soko la Malindi limechelewa kujengwa kwa muda uliotarajiwa na linatarajiwa kujegwa tena mwaka huu mwezi wa Machi na kumalizika mezi wa February mwaka 2022 na wavuvi kwa muda huu wamehamia katika Diko la Kizingo, na Diko la Kizingo liko *open space*, wachuuzi pamoja na walaji wa

samaki, jua mvua linawapata pale. Wizara yake ina mpango gani kuwajengea alau banda la dharura katika kujihami na jua na mvua.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Mheshimiwa naomba kumjibu Mhe. Hassan Hamad Omar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mheshimiwa hilo tatizo tunalielewa na kwa sasa serikali imepanga wavuvi watumie sehemu ya Bwawani. Kwa hivyo, hilo suala tunalielewa na tunaomba tu wananchi wawe wavumilivu, tunaendelea na mikakati ya kujenga soko la uhakika.

**Mhe. Shaaban Ali Othman:** Ahsante Mhe. Spika, kwanza namshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nilikuwa nataka nimuulize swali moja la nyongeza kupitia majibu yake ya msingi. Ameeleza hapa kwamba kutokana na sababu ya *COVID 19* Serikali ya Japan imeondoa wakandarasi wake nchini na hadi sasa hajatupa maelezo ni lini wakandarasi hawa hasa wanatarajiwa kuja Zanzibar kuendelea na ujenzi wa soko lile. Lakini pia hatuna uhakika, *COVID* kwa upande Japan itaisha lini, soko lile kwa upande wa *phase 2* ndio inayowagusa wanachi wetu, hasa wale waliokuwepo pale na waliondolewa. Sasa swali langu ni kwamba je, serikali haioni haja sasa ya kubadilisha kandarasi hii tukawapa wazawa ili ujenzi wa soko lile ukaendelea.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwenyekiti swali lake la nyongeza kama ifuatavyo...

**Mhe. Spika:** Ni Mhe. Shaaban Ali Othman.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Mhe. Shaaban Ali Othman, jibu langu la msingi nilieleza kabisa kwamba tunategemea mwezi wa Machi wakandarasi wafike hapa.

Suala la pili lilikuwa nikumbushe kidogo.

Aa, ok nimeshalipata. Kwa nini tusiwape wakandarasi wadogo. Mimi nadhani tusubiri mpaka tutakapofikia mwezi wa Machi tuone hatua gani imefikia na wenzetu wa Japan, hapo tutakapofika mwezi wa Machi, ikiwa hali bado haijaridhisha, basi tutaangalia namna gani ya kuweza kulimaliza suala hilo.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini mimi nampongeza sana Mhe. Rais kwa jitihada hizi za kuja na hii *blue economy* ya kuweza kutufanya Zanzibar kuonekana kweli ni nchi iliyozungukwa na bahari.

Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri na kumkumbusha kitu. Serikali ya Awamu ya mwanzo ya Mzee Karume ilikuja na Azimio la Kuwathamini Wakwezi, Wakulima na Wavuvi, na ushahidi huo ukienda hapo Mazizini panapouzwa samaki, lile soko utakuta lilijengwa enzi hizo lakini lina msikiti, kuna pahali pa kupumzikia, kunako ile *landsite* yaani madiko. Lakini je, katika kuendeleza mbele hii *blue economy* yaani uchumi wa buluu, serikali ina mkakati gani wa kuwathamini kama alivyowathamini Mzee Abeid Amani Karume Wavuvi kwa kuwajengea madiko mazuri kama lile la Mazizini.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Hassan Khamis Hafidh swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mheshimiwa katika mipango yetu ya *blue economy* yamekwenda zaidi kuliko huko wanakofikiria. Tutajenga madiko, tutajenga masoko, tutajenga viwanda. Kwa hivyo, mambo yanakwenda kidogo kidogo mimi nadhani awe na subra tu, tutafikia huko anakokutaka.

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Waziri unaweza kwenda kukaa.

Waheshimiwa Wajumbe, maswali kwenye *order paper* yamemalizika japo muda umebaki kidogo. Naomba nitoe tangazo moja ambalo niwakumbushe Wajumbe kuhusu semina ambayo inahusu huduma za Maji na Nishati iliyoandaliwa na *ZURA* itafanyika kesho Jumamosi saa 3:00 asubuhi katika ukumbi wa mikutano wa *ZURA* uliopo Maisara. Kwa hivyo, naomba kuwajulisha tangazo hilo.

Baada ya hapo sasa naomba nimwite Katibu kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka 2018/2019

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kama mtakumbuka kwamba baada ya kuwasilishwa kwa hizi ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yalitoka maswali hapa pamoja na michango ya kutoka kwenye kamati zetu na Mhe. Waziri aliahidi kuja kutupa majibu leo. Kwa hiyo, kabla sijampa hiyo nafasi nitamkaribisha kwanza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango yeye azungumze hapa machache baadae nitamwita mtoa hoja ili aweze kuja kutoa majibu ya maswali. Mhe. Waziri karibu sana.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango:** Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuzungumza machache katika hoja ambayo iliyowasilishwa hapo juzi juu ya taarifa hizi za Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali na mimi nipende kumpongeza mtoa hoja pamoja na Mwenyekiti wa *PAC* na wa *LAAC* kwa uwasilishaji wao. Nitazungumzia maeneo machache na kwa kifupi sana.

Kwanza sote tunajua umuhimu wa ukaguzi na jambo hili lipo kikatiba na kwa mujibu wa katiba yetu ibara ya 112 naomba ninukuu ibara (iii) Mhe. Spika, inasema:

"Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa na majukumu ya mambo yafuatayo (a), (b) na (c)". Naomba nilisome jukumu (c):-

"Angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hesabu zinazosimamiwa na Watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi wa Zanzibar, Hesabu za Mahakama zote za Zanzibar, Hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na katiba hii na Hesabu zote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi".

Baada ya kusoma kipengele hicho naomba nijielekeze sasa kwenye Sheria yetu ya Fedha yaani *The Public Finance Management Act* ya mwaka 2012 pia nayo imeeleza majukumu ya mkaguzi. Ukisoma *section* ya *123 sub section one* naomba niinukuu.

> *"On receiving the financial statement describe by sections 121 and 122 of this Act. The Control and Auditor General shall calls them to be examined and audited in accordances international accepted auditing standard and shall within 5 months after the end of financial year to which the financial statement related prepare the audited report".*

Baada ya kusoma hayo, pia naomba sasa tujielekeze kwenye nini *International Accepted Standards* zinamtaka mkaguzi afanye. Hizi ni *standard* za kimataifa ambazo zinapitishwa na bodi inayosimamia na masuala ya Uhasibu na Ukaguzi yaani *IFAC* ukisoma *International Standard of Audit 200* naomba ninukuu:

> *"The roll of auditor, the objective of independent auditor is to enable auditor to express an opinion whether the financial statement are prepare in all material respect and accordance with applicable financial reporting frame".*

Sasa Mhe. Spika, baada ya kunukuu vifungu hivyo naomba pia ninukuu kanuni yetu ya Baraza. Kanuni namba 109 inaeleza utaratibu wa kamati na ukisoma kanuni ndogo ya saba na ya kumi na tano inaeleza namna gani kamati itafanya kazi.

Mhe. Spika, nishukuru wenyeviti kwa taarifa yao waliyoeleza, kuna mambo mawili ningesema nigusie. La kwanza ni jukumu la *CAG*. *CAG* ni chombo muhimu sana katika kila nchi na umuhimu wake unatokana na nini, yeye ndie anakuwa *responsible* na kusimamia au kutoa taarifa juu ya pesa zote za serikali zilivyotumika na yeye anawajibika moja kwa moja kwa chombo hichi na kwa wananchi wa Zanzibar na ukitizama hata *position* yake kikatiba imemlinda kufanya kazi zake bila ya kuingiliwa na mtu yeyote.

Sasa majukumu tuliyoipa ofisi hii ni kukagua hesabu, sasa hesabu zinakaguliwaje ndio nikasoma mlolongo wote huo mpaka hatua ya mwisho Hesabu za Ukaguzi zinavyokaguliwa na kuwasilishwa.

Kwa mujibu wa katiba yetu *CAG* tumempa *mandate* ya kukagua hesabu yaani *financial report*. Sasa kuna dhana imejengeka ya kwamba kila tunapoenda kukiwa na tatizo sasa *CAG* hakufanya kazi, hii si sawa. *CAG* anakagua hesabu kwa mujibu wa kanuni na taratibu ambazo zipo. Kwa hiyo, hata kama sehemu kuna wizi hesabu zimesema hapa kama kuna wizi na *CAG* akikagua katika taarifa ikionesha kuna wizi yeye atasema hati hii ni safi kwa sababu kweli kwenye ile hesabu imeripoti ule wizi kwa hiyo kazi yake ameifanya.

Lakini pia *CAG* ana *express opinion* sio kwamba ripoti yake inafanya kila kitu *it's just an opinion* zile hesabu zimeandaliwa kwa mujibu wa yale masharti na vigezo tulivyopewa. Kwa hiyo, naamini chombo chetu hichi kina wajibu wa kushirikiana na sisi, hata sisi serikali tumeona kuna maeneo ambayo sasa sisi wenyewe kwa vile tuna mkaguzi wetu wa ndani tumem-*task* kazi hizo. Lakini na chombo hichi ambacho mnafanya kazi kwa ukaribu na *CAG* pia mna uwezo wa kumpatia. Kuna taarifa muhimu za mazingatio ambazo hizi tunaweza tusizipate kwenye taarifa

za ukaguzi wa mwaka ambazo hizi ni *special assignment* ambazo *CAG* kwa mamlaka ya kikatiba hatukumpa kufanya *performance audit*.

Kuna dhana mbili tofauti, kuna *financial audit* na *performance audit*. Jukumu la kikatiba *CAG* tulilompa kufanya *financial audit* kukagua hesabu tu vitabu kama hapa shilingi ngapi, risiti zipo, hazipo hilo ndio jukumu tulilompa.

Sasa kama tunaona na mimi naungana na wajumbe wenzangu kwamba ipo haja kumuomba *CAG* kufanya *performance audit.* Naamini kupitia Kamati ya *PAC* na *LAAC* kwa sababu wao ndio wadau wa karibu na ofisi hii basi katika yale maeneo ya mazingatio tumtumie *CAG* kufanya ripoti au kufanya kaguzi hizi za *performance*, ili sasa kuleta taarifa ya kina ambayo inahusisha masuala ya *value for money* ambao Wajumbe wengi imekuwa *concerning* kwao. Hilo eneo la kwanza.

Lakini eneo la pili juzi yaliripotiwa mafungu mengi ya ajabu na hili ndio maana nikasema mpaka nikanukuu kanuni ile ya 109 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. *CAG* jukumu lake ni ukaguzi na ukipitia taarifa za hesabu zile za ukaguzi za *CAG* mafungu yale yote ambayo tulisema ya Bima, ya Benki, ya *ZRB* hayajakaguliwa *CAG* yote yana taarifa zake za ukaguzi. Niwaombe tu wajumbe kwenye sekta nyeti na muhimu katika nchi hii hamna kama sekta ya benki.

Kwa hiyo, sekta ya benki macho yote kwanza *regulator* mkubwa wa sekta hii ni *BoT.* Yaani kila kitu kinachofanywa ndani ya benki, yaani hata kuna mambo madogo tu sana basi yanahitaji *approval* za *chain* kubwa sana. Sasa seuze za suala la ukaguzi ambalo linasema takribani miaka mitano benki haijakaguliwa ndio maana nikasema kuna hii dhana ya kukaguliwa na dhana ya mafungu haya kwenda kuchambuliwa kwenye kamati zetu.

Mhe. Spika, utakubaliana na mimi mafungu ni mengi na kwa mujibu wa muda ambao kamati zetu tumeupa kamati zetu zifanye kazi ni muda mdogo. Kwa wiki mbili katika vikao vinne hawawezi kwenda kwenye mafungu yote ya ukaguzi. Nikubaliane na wajumbe na viongozi wa kamati hizi walikuwa wanalilia waongezewe muda wa kufanya kazi na mimi nakubali kwa sababu kazi ni kubwa kupitia fungu moja au mawili kwa siku inawachukuwa muda mrefu. Labda kutokana na ufinyu wa muda mafungu ambayo *CAG* aliweza kukagua na kuwasilisha ripoti za ukaguzi hayakupata bahati sasa ya kufika kwenye kamati zetu hizi za kudumu yaani ile ya *PAC* na ile ya *LAAC* kwa ajili ya uchambuzi.

Kwa hiyo, taarifa zao hazikuweza kupata mjadala katika kamati zetu na kuwasilishwa katika Baraza lako kwa ajili ya kujadiliwa. Lakini sio kwamba mafungu haya hayakukaguliwa. Mafungu haya yalikaguliwa na mimi niwaombe tu Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati zetu hizi mbili wazidi kushirikiana na *CAG*. *CAG* mhimili wao na ndio msingi mkuu wa kazi zao na sisi serikali tunajivunia *CAG* anatupa chachu na changamoto. Kwa sababu katika *the more than governance* pia wanasema *critics is a free consultation*. Kwa hiyo, kila *CAG* anavyotu-*criticize* sasa kwetu sisi tunaona ni nafasi ya kuona namna gani sasa tunaongeza ufanisi na ku-*improve* utendaji wetu ndani ya serikali.

Kwa hiyo, na mimi niwaombe sana kamati zetu ambazo zinafanya kazi kwa karibu na *CAG* kuona ipo haja ya kumtumia *CAG* kwa sababu ndio chombo pekee cha kikatiba kilichoweka kwa ajili ya kukagua au kusimamia serikali kwenye upande wa matumizi hamna chombo chengine. Kwa hiyo, nishukuru kamati zetu zimefanya kazi vizuri lakini nilikuwa na jambo hili nikasema kabla mtoa hoja hajazungumza na mimi nipate kuchangia ili kuona namna gani sasa huko mbele ya safari tunaboresha utendaji kazi na hususan na kamati zetu hizi mbili. Lakini pia kuona namna gani sasa chombo hichi cha Baraza kinashirikiana kwa karibu kabisa na Afisi yetu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa sababu ni mtu muhimu sana kwa Baraza letu na kwa wananchi wote. Lakini pia ndio ana ile *stewardship* yeye anaonesha kwamba usimamizi wa mali za umma matumizi yake na kila kitu ndani ya serikali yanafanyika kwa vile ambavyo sheria imeelekezwa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu na niendelee kukushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa wote asubuhi hii ya leo kwa kupata nafasi kuja kutekeleza ahadi yangu niliyoiweka juzi kwamba nitaleta majibu hapa Barazani.

Lakini kaba sijatoa majibu hayo naomba kwanza niwashukuru Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuniuliza mimi ni mwalimu nimezoea kuwauliza watu, sasa na mimi leo nimeulizwa, madhali nimeulizwa na mwalimu akiulizwa na mwanafunzi huona raha kumjibu vizuri. Sasa hawa si wanafunzi ni waheshimiwa wanahitajiwa kujibiwa vizuri ili wafahamu kile ambacho wamekiuliza.

Kwa hivyo, niwashukuru kwanza na niwatambue waliouliza maswala haya mbali mbali. Kwanza Wenyeviti wa Kamati Mhe. Mwanaasha Khamis Juma nakupongeza sana Mwenyekiti wa *LAAC*, Mhe. Juma Ali Khatib Mwenyekiti wa *PAC* nakushukuru vile vile kwa kuwasilisha ripoti yako na waliouliza maswala ni:-

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
Mhe. Shaib Hassan Kaduara
Mhe. Rukia Omar Ramadhan
Mhe. Hamza Hassan Juma
Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir
Mhe. Omar Said Shaaban
Mhe. Suleiman Makame Ali
Mhe. Yussuf Hassan Iddi
Mhe. Hassan Khamis Hafidh
Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango

Hao ndio waliopata nafasi wa kwanza niliowataja ukiondoa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango ambaye na yeye amenisaidia kutoa jawabu za baadhi ya masuala.

Mhe. Spika, nataka nitoe kidogo nasaha chombo hichi ni chombo kikubwa sana ni mhimili ambao umepata heshima kubwa duniani, kila mahali chombo hichi kinachotunga sheria kina

heshima kubwa na wakati mwengine tukishasema hapa tujue hayamaliziki hapa dunia yote inapata habari siku hizi mitandao inafanya kazi yake vizuri.

Juzi tulipokea taarifa za Mwenyekiti wa *LAAC* hazikulaumu zilikuwasha wajibu wa kazi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na ripoti ile au taarifa ile iliyoletwa na *LAAC* ilikuwa na maswala mengi ndani yake.

Mhe. Spika, ulipomaliza ukatoa *conclusion* ndogo tu na mimi nimekunuu kwa ruhusa yako naomba nikunukuu vile ulivyosema:

"Uliposema ripoti hii ya *LAAC* ni balaa ulisema hivyo"

Sasa kwa ilivyowasilishwa hakuna sababu nyengine yoyote usiseme vile lakini hapa leo nitatoa ukweli wa mambo yote yafahamike mchana kweupe.

Nataka nikuhakikishieni kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iko makini sana katika masuala yote yanayohusiana hasa na fedha za umma. Nataka nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha kwa kueleza haki na mamlaka aliyokuwa nayo *CAG* kifungu cha 112 na 113 cha Katiba ya Zanzibar kimeeleza wazi wazi majukumu yake wapi *CAG* anapeleka taarifa zake. Katika kifungu kile cha 112 na 113 waziri hakutajwa mle anaesimamia masuala ya *CAG* katajwa *CAG* na ripoti zake akimaliza anapeleka mamlaka iliyomteuwa ambaye ndie Mhe. Rais.

Kama hamjui nataka nikufahamisheni mimi kama waziri ninayesimamia masuala haya wakati mwengine *CAG* anapeleka ripoti zime mimi kama waziri sina taarifa kwa sababu sheria imempa mamlaka yeye sie waziri, halafu akeshapelekewa Mhe. Rais anachofanya katika kipindi cha siku 7 kabla kile kikao cha Baraza kinachoendelea kile awasilishe ripoti ile kwenye Baraza la Wawakilishi anampa mtu yoyote anaehisi anaefaa kuleta ripiti ile na mara nyingi hupewa yule waziri anaesimamia masuala la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kwa sasa hivi masuala ya Mdubiti yako katika wizara inayoshika na masuala ya Utawala Bora.

Kwa hiyo, kwa sababu masuala ya *CAG* ni masuala ya Utawala Bora yanajenga nidhamu ya matumizi katika afisi zetu, katika taasisi zetu na katika mashirika yetu na moja katika sifa kubwa ya Utawala Bora ni kutumia vizuri fedha za umma na kuzitumia kwa njia ambazo zimekubalika kwa mujibu wa sheria zilizotayarishwa au zilizowekwa na Baraza la Wawaklilishi.

Kwa hivyo, hapa juzi zilitoka taarifa nyingi kwamba *PBZ* haijakaguliwa, Bima haijakaguliwa sijui kuna taarifa za miradi Mhe. Omar Said Shaaban juzi alisema kama *CAG* hagusiki sisi mtu wetu waziri. Lakini waziri hajatajwa kwenye katiba lakini hawezi kuepuka jukumu hilo kwa sababu ile afisi iko chini yake. Kuna kazi ambazo waziri anajua anapopewa *CAG* kuna kazi ambazo kati ya mamlaka na *CAG* anapewa *CAG* kutokana na mamlaka iliyomteuwa.

Mhe. Spika, kuna mfano ukaguzi wa jengo la Treni imetajwa, mfano kuna suala zima la mradi wa *ZUSP* na mwengineo. Kazi zile zimefanyika na zimekaguliwa na kazi zile zimetolewa na mamlaka inayosika na kazi sio ikishatolewa na mamlaka tena siku ya pili ziletwe hadharani zinfanyiwa uchunguzi na utafiti. Kama vile jengo la Treni baada ya kufanyiwa utafiti ripoti imekwenda kwa mamlaka na *ZAECA* ndio waliopewa jukumu lile na *ZAECA* tayari walishiriki

mpaka taarifa zile kwa mamlaka na tulikuwa mashuhuda sote tumeona hata hicho kitabu cha *ZAECA* ndio tunacho ambacho ripoti yake hatujaiwasilisha sasa kuna picha hapo juu inaonesha Mhe. Rais kakamata *document* ambayo ile ndio ripoti ya jengo lile la tren ambayo amewasilisha *ZAECA* kwa uchunguzi sasa. Wao ndio watachunguza kuona kipi kimetenda ndivyo na kipi kimekosewa. Kwa hivyo, hakukuwa na mashaka.

Mhe. Spika, sasa baada ya hayo naomba uniruhusu nitoe ufafanuzi wa masuala haya ambayo ni machache kwa ufupi sana nitatoa kwa sababu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kishanisaidia mengi sana.

Hoja ilikuwa suala zima la ukaguzi wa ofisi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hii ndio iliyokuwa hoja msingi, mbona *CAG* hatujapata ripoti yake ya kukaguliwa yanakwenda kwendaje mambo haya je, tutajuaje ripoti zake. Nataka nikuhakikisheni kuna Taasisi inaitwa *TAC (Tanzania Associate Consultant)* ni taasisi fulani ambayo ipo Tanzania Bara pale hii ndio inayofanya ukaguzi wa ofisi ya *CAG* imefanya mara moja mara mbili, sasa baada ya ripoti zile kiwajibu inabidi *CAG* sasa ziwalishe kwenye mamalaka inayohuka na baadae ziwasilishwe hapa Barazani.

Tukubali kuna makosa yalikuwa yanatendeka na anaekubali kosa ni muungwana ofisi ya *CAG* ilikuwa suala lile mwenye mamlaka ya kuteua ile kampuni au taasisi kama alivyosema hapa Mhe. Waziri wa Fedha ikishamalizika ni waziri ndie anayeteua ile kampuni sio yeye mwenyewe *CAG* ateue yeye mwenyewe hilo haliwezekani. Kuanzia mwaka huu nimetoa maagizo na inshallah ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali italetwa Barazani kwa ajili ya kuipitia hapa. *(Makofi)*

Hilo limekaa sawa tumeshaliwekea msimamo na nimetoa maelekezo hivi sasa Katibu Mkuu analifanyia kazi kwa kushirikiana na Taasisi zinazohusika kupitia Wizara ya Fedha vile tushirikiane nao ili kuona njia gani tunatumia kupata mtu ambae anaweza kuja kufanya *Auditor* katika ofisi ya *CAG* yenyewe, hilo lilikuwa la kwanza. La pili sababu zilizopelekea kutokaguliwa kwa baadhi ya mashirika nimesema hapa zimekaguliwa nitatoa mfano Mhe. Spika, na ripoti zote hizi za ukaguzi zipo tayari zikihitajika zipo pake kwa afisa wetu kaja nazo zote.

**Benki ya Watu wa Zanzibar**

Benki ya Watu wa Zanzibar ambayo inasemekana haikukaguliwa lakini kama alivyosema Waziri wa fedha Benki hii ina utaratubu wake na kuna *regulator* wake ambaye ni *BOT*. Sasa kuna Taasisi ambayo imekwanda kuikagua hii nitaitaja hiyo taasisi yenyewe ili tupate uhakika zaidi na ukaguzi umefanyika lini tarehe 31 Desemba 2019 imekuguliwa *PBZ*. Kwa kushierikia na kampuni moja *Claritas International Zanzibar Limited* na r*egulator* wetu tunaambiwa ni *BOT* kwa hivyo, *PBZ* imekaguliwa sio kama haijakaguliwa hata siku moja. Banki ya watu wa Zanzibar zinafunga hesabu zake kwa kutumia mwaka wa fedha Januari hadi Disemba kwa mujibu ya sheria ya usimamizi wa fedha namba 12 ya mwaka 2016.

Taasisi za umma zinatakiwa kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka wa miezi mitatu kwa kukamilika kipindi cha mwaka. Aidha, kwa kipindi ambacho Benki ya Watu wa Zanzibar inawasilisha hesabu zake kwa ajili ya ukaguzi kwa kipindi hicho Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tayari ameshawasilisha kitabu chake cha ukaguzi cha mwaka 2018-

2019 na kuwasilisha katika mamlaka husika ya uteuzi. Yaani tarehe inabadilika badilika yaani kalenda ni tofauti tarehe ya kuwasilisha hapa na zile kalenda za *PBZ* ukaguzi wake. Kwa hivyo anapowasilisha zile ripoti wenyewe tayari *CAG* ishazipeleka kwa mamlaka iliyomteua au iliyompa mamlaka yake kama azipeleke kwa nani.

Kidogo panaingiliana mambo mawili matatu sasa hivi kazi iliyopo mbele yetu na sisi hata kalenda zetu za Baraza itabidi tuziangalie vizuri ili ripoti zile zipatikae kwa wakati hivi ninavyosema sasa hivi ripoti ya Mwaka 2019/2020 tayari iko hatua nzuri na tunatarajia kuiwasilisha wakati wowote ili iweze kujadiliwa hapa katika Baraza lako tukufu.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Mkuu wa Hesabu za Serikali ikikagua hesabu za mfuko wa hifadhi ya jamii kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa kushirikiana na kampuni hiyo hiyo *Claritas International Zanzibar Limited* Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekamilisha ukaguzi huo na kuwasilisha ripoti ya mahesabu yaliyokaguliwa kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya kuthibitishwa usahihi wa hesabu hizo na kusainiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ndio uratatibu ulivyo.

**Bodi ya Mapato Zanzibar *(ZRB)***

Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilikagua hesabu za bodi ya Mapato ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na 2017/2018 kwa kushirikana na kamupuni hiyo hiyo *Claritas International Zanzibar Limited.* Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekalisha ukaguzi huo na kuwasilisha ripoti ya mahesabu yaliyokaguliwa kwa bodi ya Mapato Zanzibar kwa ajili ya kuthibitisha usahihi wa hesabu hizo na kusainiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi. Baada ya *CAG* kwenda kukagua baadae zinapelekwa tena wathibitishe je, yale yaliyokaguliwa yalionekana ndio sahihi. Baadae Bodi inapelelekewa wanapitia wakiridhika inatiwa saini ikishtiwa saini sasa anatayarisha kwenye kitabu ndio manake baadae ndio zinaletwa hapa.

**Ukaguzi wa Shirika la Umeme Zanzibar**

Ukaguzi wa Shirika la Umeme Zanzibar, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilikagua hesabu za Shirika la Umeme kwa mwaka 2018/2019 kwa kushirikiana *TAC* kile chombo ambacho nimekitaja. Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali imekamilisha ukaguzi huu na kuwasilisha ripoti ya mahesabu yaliyokaguliwa kwa Shirika la Umeme Zanzibar kwan ajili ya kusainiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi lithibitishe na kutiwa saini hesabu hizo na limetiwa saini tayari 30 May 2019 na kuziwasilisha kwa afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo katika kipindi hicho afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tayari ilikwisha kuwasilisha taarifa hizo kwa mujibu wa sheria hivyo ripoti hiyo imekamilika nan iko tayari kuwasilishwa kwa mujibu wa sheria.

Vile vile ilipofika kwa hesabu zao kalenda zao ilichelewa kufika tayari *CAG* alikuwa tayari kashazipeleka kwa Mhe. Rais sasa tayari zishamilika hatua zake zote zimeshatiwa saini kazi iliyobakia sasa hivi ni *compile* pamoja na kuzileta kwa ajili ya kuja kuzijadili hapa.

**Shirika la Bima**

Shirika la Bima lilizungumziwa sana hili kama halijakuguliwa hata mara moja Mhe. Spika tumekagua afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilikagua hesabu za Shirika la Bima Zanzibar kwa wa Fedha 31 Decemba 2019 kwa kushirika na *TAC associate*. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekamilisha ukaguzi huo na kuwasilisha ripoti ya mahesabu yaliyokaguliwa na Shirika la Bima Zanzibar kwa ajili yan kusainia kwa Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi.

Shirika la Bima Zanzibar lilithibitisha na kusaini hesabu hizo tareje 17 Decemba 2020 na kuziwasilisha afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Lakini kama nilivyosema tarehe zilikuwa tayari zimepitana na imepelekwa tayari ishapelekwa Mhe. Rais lakini hivyo haina maana kwamba ripoti hizo hazitapatikana.

**Mradi wa *ZUSP***

Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekamilisha ukaguzi na inaendelea na kuwasilisha ripoti kwa taasisi husika kwa mujibu wa taratibu, miongoni mwa iliyokaguliwa ni mradi wa *ZUSP* ambapo ripoti ya ukaguzi mradi huo imetolewa kuwasilisha Wizara ya Fedha ambao ndio wasimizi wa kuu wa mradi huo. Ripoti hii imekalika na ipo tayari kuwasilishwa kwa mjibu wa sheria.

**Ukaguzi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar**

Ukaguzi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar, Mhe. Spika, afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inafanya ukaguzi wa hesabu za serikali kila mwaka wa fedha aidha, afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilifanya ukaguzi wa maalum wa hesabu wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kwa mwaka fedha 2016/2017 na 2017/2018 na kubaini dosari mbali mbali na ripoti yake imewasilishwa serikalini kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Vigezo vinavyotumika katika utoaji wa hati za ukaguzi Mhe.Spika, vigezo vinavyotumika katika hati na ukaguzi kitaifa na kimataifa hutolewa kulingana na mazingira tofauti yanaotokana na usahihi wa hesabu zinazokaguliwa hati zennyewe ni kama hizi zifuatazo:-

Hati inayoridhisha, hati isiyoridhisha, Hati yenye shaka na hati mbaya.

**Hati inayoridhisha**

Hati inayorodhisha ni hati aina hii inatolewa pale ambapo ukaguzi umeridhisha kutokana na kukidhi viwango vinavyotumika katika uandaaji wa hesabu, usahihi wa taarifa pamoja ushahidi uliopatikana wakati wa ukaguzi na kupelekea kutoa sura sahihi na halisi ya hesabu hizo.

**Hati isiyoridhisha**

Hati ya aina hii inatolewa pale ambapo ukaguzi umejiridhisha kwamba taarifa ya hesabu zilizoandaliwa imebainika kuwa zina dosari kubwa na za umuhimu, dosari ambazo inaweza kusababisha taarifa ya hesabu kupoteza uhalisia wake na hivyo kutoaminiwa na kuonyesha sura sahihi na halisi ya hesabu zao.

**Hati zenye Shaka**

Hati aina hii hutolewa baada ukaguzi kujiridhisha kulingana na ushahidi wa kiukaguzi mambo yafuatayo yamejitokeza. Taarifa ya fedha zilizoandaliwa zina dosari kubwa ambazo zinaweza kuathitri hesabu endapo zikichukuliwa aina moja tu baada moja au kwa ujumla wake kwenye taarifa hizo hazitoweza kuleta sura sahihi na halisi ya hesabu hizo. Pale ambapo ukaguzi umeshindwa kupata taarifa nyaraka na vielelezo vya kutosha vinavyosaidia kufanya ukaguzi na kuweza kutoa maoni ya ukaguzi wa hesabu hizo. Pia kuwepo kwa kiasi kikubwa cha mapato na matumizi yasiyokuwa na nyaraka muhimu na kufanya matumizi bila ya kuwa na kibali halali au matumizi ya mapato ambayo hayakuidhinishwa kutumika.

Pia kutozingatiwa kwa sheria na kanuni mbali mbali za matumizi ambapo kunapelekea madhara makubwa ambayo yanaweza kusababisha kutotoa sura sahihi na halisi ya hesabu hizo kwa mfano kwa vitu ambavyo vilitakiwa kuripotiwa kwenye taarifa ya hesabu na manunuzi ya vifaa hayakufuata sheria na kanuni za matumizi. Kufanya matumizi ambayo hayakuleta tija kwa taasisi husika, kutofanyika usuluhisho wa benki hali iliyopelekea kushindwa kupata usahihi wa bakaa ya fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha.

**Hati Mbaya**

Mhe. Spika, hati hii hutolewa pale ambapo ukaguzi umeshindwa kupata nyaraka na vielelezo vya kutosha wakati wa ukaguzo ili kuweza kutoa maoni ya ukaguzi kutokana upungufu yaliyojitokeza na kushindwa kugundua mambo ambayo yanaweza kusababisha madhara makubwa katika taasisi. Kwa hivyo Mhe. Spika, hayo ni baadhi tu ya majibu ambayio tumeyaleta lakini nataka niwashkuru wenye viti wa *LAAC* na *PAC* wametuamsha wamejitahidi kutusaidia na kinachofata mbele tutajitahidi kama hali itaruhusu kuandaa mafunzo maalum ili waweze waheshimiwa kuelewa zaidi huko tunakokwenda. Lakini pia sasa hivi kazi ikiyokuwa mbele yetu sasa hivi *PAC* na *LAAC* basi wazipitie ripoti hizi ili baadae waje na ripoti kamili hapa tuje tuzijadili kwa ukamilifu. Mhe. Spika naomba kuwasilisha.

**TAARIFA**

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Mhe. Spika, ahsante kwa kuniruhusu niweze kuweka taarifa na tuweke *hansard* sawa nadhani Mhe. Waziri katika majibu yake kuhusiana na swali kamati kwamba katika mahesabu yao au katika hayo mashirika ambayo tuliyataja kwa kipindi hicho ilikuwa bado taarifa zake hazijaletwa Barazani. Ndio maana kamati ilisema kwamba mwaka 2017/2018 taarifa hazikuja. Kwa hivyo, ndio maana tukasema kuwa hazijaja. Sasa maadam wamekubali kuwa watazileta lakini nyuma zilikuwa hazijaja, kwa hivyo nataka niweke *hansard* sawa.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, naomba tupokee hizo taarifa za serikali na baada ya hapo nadhani kazi zitafanywa wajumbe mtapata kuzichangia hizo ripoti siku za mbele kwa mujibu wa ule utaratibu ambao tumeuzoea. Waheshimiwa Wajumbe, naomba tukubaliane tu kuzipokea hamna haja ya kuhoji, tuyapokee haya majibu ya serikali na baadae tutayafanyia kazi. Suala hili lina changamoto kidogo lakini nafikiri maelezo mazuri yametoka kwa Mhe. Waziri wa Nchi

(OR) Fedha na na Mipango na yale ambayo yametoka kwenye majibu ya Mhe. Waziri mwenyewe ambaye anahusika. Baada ya hapo sasa naomba tuendelee na utaratibu wetu.

Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na majadiliano leo ni Ijumaa bila shaka tutamaliza saa sita kamili. Jana wakati naakhirisha shughuli za Baraza nilikuwa na wajumbe kama saba hivi ambao walikuwa wamebaki, lakini kwa kweli kwa sasa hivi kwa hao walioomba leo tu basi tutahitajika kuja kukamilisha kwa jioni tena baada ya saa 11:00 ingawa tutaanza mpaka saa sita. Kwa hivyo, kiasi cha wajumbe sita hivi wanaweza wakapata nafasi ya kuchangia mpaka saba kwa kutegemea na namna ambavyo watakuwa wamekwenda halafu baadae tena tutasitisha shughuli mpaka saa 11:00 za jioni ya leo ili kuweza kuja kukamilisha. Kwa maana hiyo, nawaomba waheshimiwa watatu wafuatao wajiandae, nao ni Mhe. Nassor Salim Ali ambaye atafuatiwa na Mhe. Zawadi Amour Nassor na Mhe. Mwanajuma Kassim Makame ajiandae.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia hutuba hii ya Mhe. Rais kwanza Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumshkuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima na kufika katika Baraza lako hili tukufu na kutekeleza wajibu wetu. Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwanza kwa kupata ushindi wa kishindo katika uchaguzi wa 2020 -2025 lakini vile vile nimpongeze kwa kazi kubwa ya kufanya kazi katika kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi yajayo ni neema tupu kweli.

Mhe. Spika, aidha pia nikupongeze wewe kwa kutuongoza tena katika baraza lako hili tukufu kwa kipindi chengine hichi cha 2025. Vile vile nimpongeze Mhe. Rais kwa kuwateua wasaidizi wake wawili lakini vile vile akiwemo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Hemed Suleiman Abdalla kijana mchapa kazi kwa kweli na nimtakie kila la kheri katika kumsaidia Rais katika majukumu yake haya. Nimpongeze pia mzee wetu Maalim Seif Sharif Hamad namtakia kila la kheri katika majukumu yake.

Mhe. Spika, nije katika sekta ya afya. Mhe. Spika, ukurasa wa 26 na 27 katika kitabu cha Mhe. Rais ameeleza hatua za kuendelea kuimarisha sekta ya afya kuna jambo jipya amelitaja ambalo wananchi wa Zanzibar walilipokea kwa hamasa kubwa sana. Mhe. Spika, jambo hili ni kuhusiana na bima ya afya kwa kweli sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa jumla wamelipokea hili na tunaliunga mkono ili wananchi wetu waweze kupata matibabu yaliyo bora na wale ambao wenye uwezo waweze kutumia hii bima ya afya.

Mhe. Spika, katika hatua hii haya yote ni katika mapinduzi makubwa katika kuendeleza hii sekta ya afya. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nitoe ushauri kwa Waziri wa Afya kusimamia maelezo aliyosema Mhe. Rais wa Zanzibar katika hutuba hiyo.

Pili, nije katika sekta ya sanaa, burudani na michezo, ukurasa wa 34 na 35 nimefarajika sana na maelezo ya Mhe. Rais katika mipango ya kuinua michezo na kimaendeleo ya kiuchumi hasa katika kupitia katika masuala ya sekta hii ya michezo. Naomba hatua za kuinua michezo kwanza ipewe kipaumbele zaidi na nimuombe Mhe. Waziri ili kuweza kumsadia Mhe. Rais na kufikia lile lengo lake. Katika mikakati ya kurejesha msisimko wa Ligi Kuu ya Zanzibar imedorora na imekuwa haina mvuto kutokana na changamoto ambazo za udhamini wa Ligi Kuu ya Zanzibar. Kwa hivyo, niombe sana serikali ya Dkt. Hussein Ali Mwinyi kuhakikisha wanaweza kuwasaidia

*ZFF* kuweza kupata wadhamini ili ligi hii iwe na mvuto wa aina yake na kuinua vipaji vya vijana wetu.

Lakini jengine Mhe. Spika, kufanya mikakati ya kuzifufua zile timu za zamani Zanzibar. Zamani *football* yetu ilikuwa na mvuto wa aina yake na Wazanzibari wanapenda michezo hususan mchezo huu wa mpira wa miguu. Lakini mchezo huu umekuwa ukidorora siku hadi siku ni kutokana pengine na vile vilabu vya zamani kuweza kufa na vikawa havipo katika ulimwengu huu wa soka kama vile vilabu vya Small Simba, Kikwajuni, Ujamaa, Mwembeladu, Kubwa Lijalo pamoja na Malindi ambayo inaenda enda katika kusuasua. Kwa hivyo, niombe serikali na waziri husika wa sekta hii aweze kuhakikisha anavishajihisha na anakutana na wadau.

Mhe. Spika, mimi nishauri kwa sababu mpira wa miguu una wadau wengi mbali na wapenzi na mashabiki lakini kuna wadau ambao wamecheza mchezo huu wa mpira wa miguu kuna wachezaji wa zamani kama Shem Frank, Ali Bushir, Moh’d Tashi na wengine sasa nadhani ipo haja Mhe. Waziri kukutana na wachezaji wale wa zamani ili kuweza kupata mawili matatu kupata ufanisi zaidi katika kuinua soka letu la Zanzibar. Mhe. Spika, mpira wetu umekufa.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo limeuwa soka letu la Zanzibar ni kuondokana na kuondoa katika *league* ya Muungano. Kwa hivyo, mimi niishauri serikali kwamba katika kudumisha Muungano wetu ni kurejesha league ile ya Muungano hata pengine katika sheria za Muungano, ili kutafuta timu mbili au tatu za Tanzania Bara na tatu za Zanzibar kucheza katika mashindano ya Muungano ambayo yatakuwa *Muungano Cup.* Hii italeta mvuto wa aina yake katika kurejesha soka letu la Zanzibar.

Jengine Mhe. Spika, Zanzibar miaka mingi hatujaandaa mashindano ya kimataifa. Mashindano yaliopo sasa ni mashindano ya *Mapinduzi Cup*, mashindani haya kwa bahati nzuri mimi ni mmoja wa waanzilishi wa mashindano haya wakati ule nikiwa Katibu wa Chama cha Mpira wa Miguu Wilaya ya Mjini, tukishirikiana na wenzangu tulianzisha mashindano haya kwa kuyaenzi Mapinduzi matukufu ya Zanzibar na tulikuwa tunazialika timu mbali mbali za Afrika ya Mashariki. Kama Kenya na Uganda, ili kuja kushirikiana na timu zetu za Tanzania Bara, nadhani katika kuendeleza mashindano ambayo yamekuwa ni mvuto mkubwa sana ni mashindano makubwa sana katika Ukanda huu wa Afrika ya Mashariki.

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Rais kwa kumteuwa ndugu yangu Naibu Katibu Mkuu Khamis ambaye baada ya kuondoka mimi kachukua hatamu na anayaendeleza mashindano haya ya *Mapinduzi Cup.*

Kwa hivyo, niombe serikali ifanye mikakati mikubwa ili kuhakikisha inaalika timu zile za Afrika ya Mashariki na Kati ili kuweza kuleta msisimko zaidi. Vile vile kuandaa mashindano kama yale ya *Challenge Cup*, Klabu Bingwa zile za Afrika Mashariki na Kati ambazo zilikuwa zinaitwa *Kagame Cup*. Mimi nadhani Zanzibar tunao uwezo wa kuandaa mashindano haya, ili vijana wetu wapate hamasa ya kuona wachezaji mbali mbali ili kuweza kuinua vipaji vyao.

Jengine Mhe. Spika, kuna Academy ambazo zimeanzishwa ndani ya Zanzibar. Nimpongeze sana ndugu yangu mchezaji wa zamani *Tanzania One* Ali Bushir, kwa kuanzisha *Academy*, ambapo *Academy* hii inaitwa *Youth Football Development Academy.*

Mhe. Spika, Ali Bushir ana vijana takriban 100, vijana wadogo tu wa kuanzia miaka 10 mpaka 15, wakati *final* za mashindano ya *Mapinduzi Cup*, nadhani sote ni mashuhuda tuliwaona vijana wale katika Uwanja wa Amani. Walikuwa wanatumia nguvu nyingi, ana mipango mizuri katika kuinua vipaji vya vijana wale. Kwa hivyo, nimuombe Mhe.Waziri na serikali kwa jumla ili kuweza kumuunga mkono Ali Bushir. Kwa kweli tumpongeze sana ndugu yetu Ali Bushir.

Mhe. Spika, katika masuala ya burudani, mambo ya sanaa. Zamani kulikuwa na taarabu zile za zamani kina Akhwan Safaa, Malindi na mzee wangu yule Mzee Gogo wa kule Kangagani, walikuwa wanatoa nyimbo za kimafunzo na burudani ambazo kwa kweli zilikuwa zinawasisimua mashabiki wa taarabu katika visiwa vyetu vya Zanzibar. Mimi nadhani iko haja ya kuunga mkono kwa sababu tuko katika hali ya kuinua maendeleo ya michezo, vile vile kutumia fursa hii kudumisha utamaduni wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nimuombe sana Mhe. Waziri ili kuhakikisha kwamba kina Mzee Gogo basi wanarudi katika hadhi yao ya zamani.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nilikuwa nataka nilizungumze katika hotuba ya Mhe. Rais katika ukurasa wa 19 na 20. Mhe. Spika, tunaingia katika uchumi wa buluu na nimpongeze sana Mhe. Rais pamoja na waziri katika kufanyakazi katika kuelekea kwenye lengo ambalo alikuwa amelikusudia Mhe. Rais, kwa faida ya Wazanzibari na Watanzania,

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, naomba uhitimishe muda wako umemalizika.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Namalizia Mhe. Spika, katika kitabu chake hiki ukurasa wa 19 amesema kuwa, “kwa upande wa Pemba tutazijenga kwa kiwango cha lami barabara za Chake Chake, Wete, Mkoani na kadhalika. Lakini vile vile tutazitengeneza barabara za ndani za Unguja na Pemba. Kwa hivyo, niiombe serikali kwa upande wa uchumi wa buluu.

Mhe. Spika, katika barabara ya Mtambile Kengeja, kwa sababu Kengeja na Mwambe ni sehemu ambayo huo uchumi wa buluu upo na wanatoka samaki wengi sana. Lakini barabara ya Mtambile Kengeja mheshimiwa ni mbovu sana. Kwa hivyo, Mhe. Spika, niombe sana barabara hii ikaweza kujengwa.

La mwisho Mhe. Spika, barabara yangu ya Jimbo la Kikwajuni ambayo ni Msikiti Makuti hadi Gongoni. Pia niiombe serikali kuweza kuiangalia barabara hii.

Mhe. Spika, baada ya kusema haya niunge mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii ya Mhe. Rais na ninamtakia kila la heri katika majukumu yake. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Zawadi Amour Nassor, ambaye atafuatiwa na Mhe. Mwanajuma Kassim Makame na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa ajiandae.

**Mhe. Zawadi Amour Nassor:** Ahsante sana Mhe. Spika, naungana na wajumbe wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na afya njema siku ya leo. Pia naomba niipongeze hotuba ya Mhe. Rais pamoja na kumpongeza yeye mwenyewe kwa ujasiri wake,

juhudi na imani kubwa aliyoionesha kwa Wazanzibari na ndio maana wakamchagua kwa kura nyingi na kumpatia ushindi, na leo akawa ndio Rais wetu wa Zanzibar. *(Makofi)*

Pia kwa fursa hii nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa kumuona Rais wetu huyu ni shujaa na ni shupavu na anaweza kuipeperusha bendera ya CCM. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pongezi nyengine ziende kwa Mhe. Makamu wote wawili waliochaguliwa hususan Makamu wa Pili ambaye anaonesha ujasiri wake wa kushirikiana na Mhe. Rais katika kutekeleza kazi zao za kila siku.

Mhe. Spika, naomba niwapongeze wananchi wa Jimbo langu la Konde kwa kunichagua kuwawakilisha. Lakini moja kwa moja niende kwenye hotuba ya Mhe. Rais katika ukurasa wa 34, ambapo hotuba yake nzuri inaonesha utekelezaji wa hotuba hii itakuwa ndio dira na muarubaini wa Wazanzibari. Ukurasa wa 34 Mhe. Rais aligusia sana kuhusiana na vitendo vya udhalilishaji ambapo vimekuwa ni kero kwa jamii yetu na kuipunguzia haiba na sifa nchi yetu ya Zanzibar. Kutokana na hili naomba niseme kwamba ifikapo miaka 10 mbele wanawake tutashindwa hata na wanaume wa kuwaowa watoto wetu, lakini pia serikali itakosa nguvu kazi, kwani udhalilishaji unaofanywa hususan kwa vijana wa kiume hupelekea vijana hawa kukosa nguvu kazi za miili yao na mwisho wake kazi yao kuwa wanayoiweza ni kupamba harusi, kutia piko na hina. Kwa hivyo, kwa hapa kama serikali yetu haijakuwa makini tukamsaidia Mhe. Rais katika kupunguza hili, basi baada ya miaka 10 taifa hili sijui nani atakuwa Rais na nani atakuwa mwakilishi.

Mhe. Spika, katika hili naomba niishauri serikali haya yafuatayo. Serikali iunde tume au kamati maalum ya kuchunguza na kubaini huu mtandao wa udhalilishaji. Je, ni kweli kuna mtandao, kwani kuna maneno mengi tu hata Mhe. Rais alipokuwa na wadau wa kupinga vitendo vya udhalilishaji, ilionekana kana kwamba kuna mtandao fulani wa kuhamasisha, mwisho wa siku Wazanzibari wote sijui wawe mashoga au sijui waweje.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, labda kungekuwa na tume maalum ya kuchunguza kama ni kweli huu mtandao upo, nani anayehusika na iweje labda baadae, ili serikali iweze kupambana nao na kuondosha kabisa.

Jengine Mhe. Spika, naomba nishauri uwepo wa Mahakama maaalum ya udhalilishaji ambayo nasikia kwa sasa tayari imeshaanzishwa na ipo. Naomba hii mahakama iwepo Pemba na Unguja, kwani na Pemba nako yapo yaliyo Unguja na Pemba yapo. Pia katika hizo mahakama kuwe na Mahakimu waadilifu ambao watazingatia kweli sheria na uwajibikaji. Uzoefu ni kwamba tunajuana kwenye utendaji. Kwa hivyo, naishauri wizara husika iangalie ni nani Hakimu wa kumuweka kwenye hizi taasisi, kwa vile lengo letu ni kupunguza hivi vitendo vya udhalilishaji.

Mhe. Spika, jengine ni kuwepo kwa marekebisho ya sheria. Kwa mfano, sheria ya ushahidi, sheria inayomlinda mwari na mjane na sheria ya elimu. Sheria hizi kwa kiasi fulani zinaonekana ndani yake kuna michangio kuna miyanya ya kuchangia udhalilishaji. Pia kuwe na utaratibu maalum wa kupatiwa wale wahanga nauli.

Kwa mfano, muhanga anataka akatowe ushahidi mahakamani, tujalie kwa sisi Pemba anatakiwa aende Wete akatowe ushahidi mwenyewe anakaa Makangale, hawezi kwenda kule kutokana na umbali na nauli nyumbani hakuna. Kwa hivyo, kunapelekea hapa kupotea kwa ushahidi na wale wafanyaji wakaona tayari ni fursa yao ya kuendelea kutukandamiza.

Jengine Mhe. Spika, kuwe na nyumba maalum ya kuwaweka hawa wahanga, kwa sababu watoto wadogo wanapofanyiwa udhalilishaji na baadae wakarudi kwenye familia zao, basi huko kwenye familia huwa kuna vishawishi na vitisho ambavyo hupelekea watoto wale kuwa wagumu wa kutoa ushahidi pale ambapo watapelekwa mahakamani kutoa ushahidi. Kwa hivyo, kuwe na stara na hifadhi mpaka pale atakapo kwenda kutoa ushahidi. Hapa napendekeza kwamba ikiwa tayari mtoto keshadhibitisha kwamba leo amefanyiwa udhalilishaji, basi kesho yake apelekwe kutoa ushahidi ili kwenye hii nyumba isijekuwa kuna gharama kubwa za kumlisha na mtu wa kukaa naye ili siku ya pili arejee nyumba.

Mhe. Spika, suala hili kwa vile Mhe. Rais alionesha nia ya kuliondoa, napenda niseme kwamba vituo vyetu vya *One Stop Center* na Dawati vina changamoto. Hakuna wataalamu hasa wa kukamilisha ushahidi katika hili na ndio maana hutumia zaidi macho na mikono katika kufanya ushahidi na siku nyengine kuna uwezekano wa kupoteza ushahidi kwa sababu vifaa vya kufanyia hili hamna.

Kwa mfano, dawati zetu nyingi za polisi unaweza kwenda na tayari mtoto ameshafanyiwa udhalilishaji, ukifika unaambiwa gari hakuna, gari haina mafuta, sijui hakuna karatasi za kuandikia. Kwa hivyo katika kwenda sambamba na hili ni lazima tuboreshe vituo vyetu vya dawati na vituo vyetu vya mkono kwa mkono. Sambamba na hilo kuwapa taaluma hawa watendaji askari wa dawati na hawa watendaji wa mkono kwa mkono. Uzoefu huu umeonesha tokea mwaka 2018 ilipoanzishwa sheria miaka 30 ni mtu mmoja tu aliyetiwa hatiani miaka 30 kwa kule Pemba, sijui leo kama aliongezeka.

Kwa hivyo, hii ni ishara kwamba tujiulize maswali huu udhalilishaji hamna au ni kipi kilichokosekana. Kwa hivyo, tunategemea kwa serikali hii ama udhalilishaji utakoma au utaondoka kabisa. Kwa hivyo, tumuungeni mkono Mhe. Rais katika azma yake hii ya kuhakikisha kwamba maendeleo ya nchi hii yatajengwa na Wazanzibari wenyewe, kinyume chake pakiwa na udhalilishaji hapo hakuna maendeleo.

Mhe. Spika, mwisho napenda nishauri kwamba hizi wizara tatu zikae pamoja zishirikiane na Mhe. Rais katika kuondoa hili, Wizara ya Afya, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Hizi ni wizara ambazo ni wadau wakubwa katika kuchangia na kupeleka msukumo wa kuondoa tatizo la udhalilishaji.

Mhe. Spika, baada hayo napenda niongelee kipengele kilichoongelewa katika ukurasa wa 19 na 20 hotuba ya Mhe. Rais suala la barabara za ndani. Napenda niishauri serikali kwamba katika hili la utengenezaji wa barabara za ndani hasa ukizingatia waziri mara nyingi anapokwenda anasema tukipata bajeti, tukipata bajeti. Napenda niseme kwamba basi kuwe na vipaumbele ili ziangaliwe sasa ni barabara zipi kulingana na mahitaji na kipaumbele kwa maslahi ya jamii, taifa na serikali basi hiyo barabara ndio ipewe kipaumbele iwe ndio ya mwanzo kutengenezwa.

Mhe. Spika, kwa mfano, barabara inayotoka Konde kuelekea Makangale, barabara hii inaelekea kwenye maeneo ya wawekezaji ambapo kuna hoteli takribani tano zinafanyakazi na zinaingiza mapato zaidi ya milioni 40 kwa mwaka, lakini ni barabara hii ambayo sasa hivi ukienda sio wakati wa mvua wala wa jua hiyo barabara haipitiki, barabara hii imepitiwa na Msitu wa Ngezi ipo katikati ya Msitu wa Ngezi. Kwa hivyo, pia lile wazo la kuongeza idadi ya watalii inapungua, kwani ni watalii wengi ambao wanaghairi njiani, akifika tu mwanzo wa msitu akitaka kuingia kati pale akiiona barabara anamwambia dereva (hapa mjumbe aliigiza sauti ya mzungu) "siendi tena samahani" anarudi. Kwa hivyo, pale serikali tumeshaikosesha mapato ya nchi. *(Makofi/Vicheko)*

Jengine Mhe. Spika, ni kwamba barabara hiyo hiyo kuna fukwe huko ambayo pia hawa watalii wanapenda. Kuna hicho kijumba ambacho kinaingiza mamilioni ya shilingi. Siku moja ni ukweli usio pingika kwamba kuna mtalii alikodi kukaa kwenye hoteli hiyo iliyokuwa na hicho kijumba kwa muda wa wiki moja na alilipa pesa zote. Alipofika na alipoiona barabara ilivyo, aliwauliza maswali mengi tu. Alipofika akasema (hapa mjumbe aliigiza sauti ya mzungu)"nitalala leo kesho nitaondoka". *(Makofi/Vicheko)*

Kwa hivyo, mwekezaji huyo alilala leo na kesho yake akaondoka na hapo alipoondoka hakupitia tena barabara ile, alihiyari apitie kwenye maji. Kwa hivyo, alipita baharini akatokea Wete, lakini ile barabara alisema haiwezekani nikiumwa, nikipata tatizo nitarudi vipi. Kwa hivyo, hata ile hali ya usalama wao kutokana na barabara wanahofu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hivyo napenda kuwe na vipaumbele, *target* yetu ni nini zaidi, tuangalie zaidi mahitaji.

**Mhe. Spika:** Naomba uhitimishe Mhe. Mjumbe.

**Mhe. Zawadi Amour Nassor:** Muda umekwisha. Toba wee! *(Vicheko)*

**Mhe. Spika:** Eee. Naomba uhitimishe Mhe. Mjumbe muda wako.

**Mhe. Zawadi Amour Nassor:** Mhe. Spika, kwa hivyo pamoja na yote hayo, naunga mkono hoja ya Mhe. Rais ni nzuri sana kwa asilimia mia moja. Mwenyezi Mungu ibariki Zanzibar, Mwenyezi Mungu mbariki Rais wetu, Mwenyezi Mungu ijaalie nchi yetu ipate pesa ya kutekeleza ahadi zote.

**Mhe. Spika:** Mhe. Zawadi Amour Nassor ni Mwakilishi wa Jimbo la Konde. UWAWAZA na serikali nadhani mmeshaona kilichopo mbele yenu, tujiandaeni. Ahsante sana Mhe. Mjumbe kwa mchango wako. *(Makofi)*

Sasa naomba nimwite Mhe. Mwanajuma Kassim Makame, ambaye atafuatiwa na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na Mhe. Hamza Hassan Juma ajiandae.

**Mhe. Mwanajuma Kassim Makame:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa furas hii adhimu kwa upande wangu, kwa sababu ni mara ya kwanza.

Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa yote kwa kutujaalia sote tukawa wazima wa afya na akatubakisha na pumzi zake mpaka hivi sasa tukawa tumekutana hapa.
Pia Nawashukuru na wanawake wote wa Mkoa wa Kaskazini ambao wamenichagua kuja kuwawakilisha katika kuwaondolea matatizo yao na kutoa ushauri katika Serikali yetu ya Mapinduzi ndani ya Baraza.

Mhe. Spika, namshukuru Rais wetu wa Zanzibar kwa ujasiri alionao, umahiri, imani, upeo wa mbali, utendaji bora, mwema na mzuri katika kuleta maendeleo makubwa ndani ya nchi yetu kwa muda mfupi mno.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia sehemu ya uwezeshaji kiuchumi katika ukurasa wa 28, katika maeneo ya ujasiriamali. Kwa kuwa dhamira na nia ya Mhe. Rais imelenga kuwawezesha wananchi kiuchumi, wakiwemo wajasiriamali kuhusiana na mitaji, mikopo, vifaa, utafutaji wa masoko, na kupewa taaluma mbali mbali. Basi mimi nashauri kwamba taaluma hii au utekelezaji huu au mipango hii itakapokuwa tayari kutekelezeka, basi waonekane wanawake zaidi wa vijijini. Kwa sababu wanawake wa vijijini bado hawajawa na fursa nzuri au hawajapata huduma nzuri kupitia mikopo na mitaji na elimu yao bado ni ndogo.

Mhe. Spika, ninachoomba ni kwamba wizara husika iwe inatoa fursa zaidi kwa wanawake wa vijijini ambao wako mbali na wako nyuma ili waweze kujikwamua kiuchumi. Naomba wizara husika iangalie fursa kwa wote, kwani fursa nyingi zinapokuwa zinatokea zinakuwa zinafika zaidi mjini na karibu na wizara ile husika.

Mhe. Spika, mwisho namalizia kwa kumshukuru sana Mhe. Rais na ninamuombea dua pamoja na sisi wenyewe tuliopo hapa, ili aweze kuiendeleza serikali yetu tuweze kufikia pahala ambapo tumekusudia.

Mhe. Spika, mimi sitochukua muda mwingi kwa sababu bado ni mwanafunzi, lakini pia naiunga mkono hotuba ya Mhe. Rais aliyoitoa tarehe 11/11/2020 hadi leo kuwa inaendelea vizuri na hapa tupo tunaijadili. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwanajuma Kassim Makame, naomba sasa nimwite Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa atafuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Mgeni Hassan Juma ajiandae.

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa:**Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Mhe. Rais Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sasa hivi tukiwa wazima wa afya katika Baraza hili na tukaweza kutekeleza majukumu yetu. Pia nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa dhamira yake njema ya kutaka kutuletea maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, niwashukuru Wanawake wa Mkoa wa Magharibi kwa kuniamini tena na kunileta katika Baraza hili ili kuja kuwatetea na nawaahidi tutashirikiana kwa pamoja kuleta maendeleo katika Mkoa wa Magharibi. Mhe. Spika, kwa kwa kweli hotuba hii ya Mhe. Rais ni dira katika serikali yetu kuelekea maeandeleo. Ni dhahiri kwamba hotuba hiii imelenga sekta zote katika serikali yetu inakwenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2021-2025.

Mhe. Spika, mimi nitakwenda moja kwa moja katika Sekta ya Afya. Kwa upande wa Sekta ya Afya serikali inaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa huko Binguni Wilaya ya Kati kwa kweli jambo hili ni jema serikali inalolifanya kwa kuwaletea wananchi wa Wilaya ya Kati Hopitali ya Rufaa katika maeneo yao ya karibu na kupata huduma nzuri katika hospitali yetu hii ya Rufaa. Pamoja na ujenzi huo nilikuwa naomba niende sambamba na fensi katika hospitali hiyo ili hospitali itakapomaliza na ujenzi wa fensi uende sambamba watakapoanza kazi zao, ili wafanye kazi zao vizuri na kwa uhakika na kwa makini bila ya kupata zogo katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, pia niipongeze serikali kwa kuimarisha hospitali zetu za rufaa Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na Hospitali za Wilaya, Hospitali ya Makunduchi pamoja na Kivunge kusema kweli jambo hili ni dhahiri serikali inawajali wananchi wake kwa kuona inataka kuwaletea huduma bora ya afya.

Mhe. Spika, katika Hospitali yetu ya Rufaa Mnazi Mmoja tayari tumeona huduma zinapatikana vizuri lakini bado kuna changamoto kidogo zinasumbua kama walivyoanza kuchangia Waheshimiwa na mimi naungana nao katika suala la kutafuta kwenda kupima vipimo unaweza ukamuona daktari akakuandikia lakini vipimo ukatakiwa ukafanye nje ya Hospitali yetu ya Rufaa. Mhe. Spika, suala hili ni tatizo kwa sababu kuna wananchi wanao uwezo wana bima wanaweza kupata huduma hii kwa urahisi. Lakini kuna wananchi hawana uwezo na kule kwenye vipimo unatakiwa ulipie. Kwa hivyo, hili naiomba serikali iliangalie vizuri tena kuona katika Hospitali yetu hii katika kuiboresha basi na vipimo hivyo vilikuwepo.

Mhe. Spika, niende katika suala la mama na mtoto tunashukuru Hospitali yetu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja inatoa huduma vizuri kina mama kusema kweli tunahudumiwa vizuri lakini pamoja na huduma hizo bado kuna changamoto ndogo pale ambapo mzazi ameshajifungua lakini anasubiri muda wa kupewa ruhusa ili aruhusiwe kwenda nyumbani wakati anasubiri katika yale masaa saba ambayo yupo katika uangalizi vitanda bado kidogo katika jengo letu la Dodoma, unapokwenda katika chumba cha kupumzikia kwa kusubiri kupata ruhusa unakuta kitanda kimoja wamekaa wazazi wanne wanaambiwa waweke mtoto mama akae asusubiri hayo masaa saba yafike apewe ruhusa na wengine wapo chini wanasubiri aondoke kwenye kitanda ili yule wa chini apande juu. Kwa hivyo, bado hilo liangaliwe tatizo hilo kutokana na sisi wanawake jinsi tulivyokuwa wengi na tunajitahidi *Alhamdulillah*.

Mhe. Spika, pia katika eneo hilo kuna tatizo la kipimo cha watoto wachanga ambao baada ya kuzaliwa kuna wengine wanapata matatizo lakini katika matatizo hayo kuna tatizo la kuwa na njano. Lakini tatizo hilo mtoto yule anapotaka kupimwa damu pia kipimo pale hapana unatakiwa uende Al- Rahma na kule unapimwa kwa shilingi 20,000 nakumbuka ndio unakuja kurejesha majibu ili daktari aweze kuja anaendeleaje. Kwa hivyo, hili ni tatizo kwa sababu watoto wetu

pale sasa hivi tukizingatia wale njiti ndio tatizo hilo linawapata basi kile kipimo inamaana ili daktari apate usahihi wa yule mtoto kipimo atoke nje akapime Al- Rahma arejeshe hospitali.

Kwa hivyo, naiomba serikali na hili iliangalie katika umuhimu wake kuhusu kipimo hicho cha kupima damu kuhusu watoto kupata umanjano.
Mhe. Spika, nikiendelea niende katika maji safi na salama ni kweli katika hotuba ya Mhe. Rais imezungumza kwamba upatikanaji wa huduma ya maji bado ni changamoto katika baadhi ya maeneo ya Mjini na Vijijini. Mhe. Spika, suala hili kusema kweli mtihani kidogo lakini tunawashukuru kwamba hatua ambazo zimechukuliwa katika Mamlaka hii ya Maji safi na salama *ZURA*, tunaona jitihada wanazochukua lakini ninachokisema na Waheshimiwa wengi wanakilalamikia kwamba tatizo maji na maji tayari utaratibu umeanza kufuatiliwa lakini bado maji mengi yanapotea kwa hiyo, waangalie tena kuhusu mabomba waharakishe kwa sababu hotuba alivyoitoa Mhe. Rais katika Baraza letu hili suala hili kaliona kwa hivyo, naiomba mamlaka husika wajitahidi.

Waheshimiwa wengi katika majimbo wanalalamikiwa na wananchi wao tatizo la maji, bado mafundi wanatengeneza eneo moja lakini eneo la pili bado hawajalifikia maana kufungua maji tayari yale mabomba pamoja na Mhe. Waziri alitujibu kwamba wapo katika mpango huo wakutengeneza plan hiyo ya kutoa mabomba ya zamani na kuweka mapya lakini naomba iharakishe tukizingatia tumebakia kama mwezi mmoja na nusu tunaingia katika mwezi Mtukufu wa Ramadhan kwa hivyo basi wajitahidi tuone tatizo hilo angalau kidogo au zaidilifanikiwe…

**Mhe. Spika:** Anza kuhitimisha Mheshimiwa.

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa:** Mhe. Spika pamoja na hilo nilikuwa nataka nimalizie kwamba pia wazingatie katika maeneo yale ambayo yanahamiwa sasa asubuhi liliulizwa swali hapa kuhusu maeneo ambayo hakuna maji safi na salama na hili pia walizingatie kwa sababu katika maeneo hayo kuna wale ambao wanaweza wao wanachimba visima lakini kuna wananchi wetu waliokuwa hawana uwezo suala hili linakuwa kwao ni tatizo. Kwa hivyo, naiomba Mamlaka hisika pamoja na kutengeneza maeneo ya Mjini au Mkoa wa Mjini wa Magharibi iangalie na Mikoa mengine kule kwenye changamoto ya maji basi nako wafike kwa sababu bado hayajafika maji safi na salama.

Mhe. Spika, baada ya kusema haya kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Magharibi naunga mkono hoja hii asilimia mia.

**Mhe. Spika:** naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma atafuatiwa na Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Harusi Said Suleiman.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, na mimi kwa upande wangu nikushukuru kunipa hii nikaweza kuchangia hotuba hii adhimu sana ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipokuja kulihutubia na kulizindua Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya Mhe. Juma Ali Khatib hayupo lakini nilikuwa nataka nimpelekee salam kwamba jana alikuwa anafanya *birthday* ya timu yao ya Yanga. Lakini mimi nataka nimwambie siku hizi vijana wanakwambia namba sio tatizo, tatizo matendo yake kwa hiyo, ajue

kwamba pamoja kwamba wametimiza miaka 82 lakini Simba wamewabeba katika mashindano ya Kimataifa na mwaka huu vile vile wataendelea kuwabeba. Mhe. Spika, nadhani mwenyewe kasikia na meseji imeshamfika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwanza kwa hotuba yake ambayo aliyotutolea katika Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, hotuba yake imo katika kitabu hiki ukiangalia kina kurasa 37 lakini unaweza ukatunga vitabu vyengine kumi kupitia katika hotuba hii. Mhe. Spika, mimi nataka nimpongeze kama alivyotupongeza sisi kwa ushindi mzuri mkubwa sana lakini vile vile nataka niwapongeze wateule wake ambao amewatea. Mhe. Spika, mimi nawaombea kila la kheri na sisi kama *back benchers'* tutshirikiana nao na tutasaidiana nao kwa hali na mali ili kuhakikisha haya malengo ya Mhe. Rais wa Zanzibar tunayatekeleza kwa sote na tunafikia yale matumaini ya wananchi.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba hii Serikali ya Awamu ya Nane ni serikali ambayo *speed* yake mtu akifanya masihara anaweza akaachwa njiani na ukizingatia hata katika hotuba yake Mhe. Rais katika ukurasa wa saba alielezea karibu asilimia 93 ya kizazi kilichokuwepo sasa hivi basi kimezaliwa baada ya Mapinduzi ambao ndio akina sisi. Sasa kasi yetu hii mtu kama akifanya masihara tunaweza kumuacha njiani.

Mhe. Spika, mimi nataka nieleze katika lile eneo ambalo alielezea kwamba sasa hivi tunataka tutafsiri mapinduzi tusiwe tunasema  Mapinduzi Daima hapana tutafsiri nini maana ya mapinduzi na ndio hii hotuba yake aliyokuja nayo akasema sasa anaelekeza katika Mapinduzi ya kiuchumi. Mhe. Spika, katika maelezo ya Mhe.Rais katika hotuba yake ukiangalia katika ukurasa wa kumi ameanza kutafsiri ni namna gani malengo yake ya kutafsiri mapinduzi ya kiuchumi kwa kuanzisha wizara maalum, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

Mhe. Spika, wizara hii na mimi naiombea dua sana Mwenyezi Mungu awajaalie yale malengo yao yote ambayo waliyoyapanga waweze kufanikiwa. Mhe. Spika, katika wizara ambayo itatoa ajira nyingi sana italeta mapato mengi kwa serikali ni hii Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Mhe. Spika, ukiangalia hivi karibuni Mhe. Waziri tayari alikwishaanza kuwakutanisha baadhi ya benki na baadhi ya wavuvi kwa ajili ya kutafuta namna gani kuweza kuwawezesha wavuvi wale ambao aliyozungumza jana Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa kuwezesha sasa kwenda kuvua katika bahari ya mbali wasivue huku karibu karibu ambapo kwenye mazalia ya samaki. Sasa hili peke yake kwa upande wa wavuvi nafikiri itakuwa ni uokozi mkubwa sana.

Lakini tuje katika suala la mafuta na gesi kwa kweli Mhe. Spika, tunashukuru kwamba sasa hivi kuna dalili ya kupatikana gesi kwa asilimia kubw katika nchi yetu. Lakini vile vile, katika miradi ambayo Mhe. Rais ametia saini hivi karibuni suala la Bandari ya Mangapwani lakini vile vile eneo la Bandari ya Uvuvi.

Mhe. Spika, hapa tulikuwa na ombi maalum sasa hivi tunategemea nchi yetu itajengwa sana tunategemea makampuni makubwa yatakuja Zanzibar katika suala ujenzi, lakini vile vile na kuwekeza. Hasa hapa nilikuwa naombi hasa kupitia kwa Mwanasheria Mkuu hivi sasa ukiangalia wakandarasi wetu tunaweza tukafika pahala wakaja wakawa wao sasa ni mashuhuda wa kuona wakandasi wakubwa wanaokuja wanafanya kazi za uekezaji kujenga miradi mikubwa

lakini wao wakawa washindikizaji kwa macho. Kwa hiyo, kitu ambacho tunachotaka kuomba na Mhe. Rais katupa ruhusa tuangalie katika maeneo gani sheria tufanye marekebisho.

Basi katika haya makampuni yatakayokuja makubwa hasa kwa ajili ya ujenzi basi kuwe kuna kipengele kinachowalazimisha kuweka wale *contractor* ambao watakaokuwa ni *local* ili sasa kuweza ku-*transfer technology* kutoka katika makampuni makubwa kuyaleta katika makampuni madogo hii kwa kweli Mhe. Spika, ndio itaweza kutafsiri hasa huu uchumi unaingia nao katika *style* gani. Lakini vile vile, tuweze kutoa elimu na taaluma kwa wafanyabiashara tuna *Chamber of Commerce* hapa sasa hivi ukiangalia katika ile sheria tuliyoipitisha ya mafuta na gesi kuna suala la *local content* inavyotakiwa wale wajenzi au watu wa miradi wanapokuja vile vifaa vyao vyote asilimia kubwa viwe vinakuwa *supplied* na *local person*.

Kwa hiyo, hii na katika maeneo yale Mhe. Spika, katika suala ku-*supply* vifaa inataka taaluma maalum kwa sababu sio unakwenda tu kununua kifaa kuna vifaa ambavyo vinatakiwa viwe katika kiwango maalum hata ulishaji, kusambaza mayai na vitu vyengine hivi vinatakiwa *local person* waweze ku-*supply* kwa wale wawekezaji ili sasa ile neema inapokuja isiwe zile fedha zinakwenda nje ya nchi.

Lakini jengine Mhe. Spika, hotuba ya Mhe. Rais inatupekea ndani ya miaka mitano ijayo Zanzibar itaanz kubadilika na kuimarika kiuchumi. Lakini vile vile tunategemea viwanda vingi vitakuja na hasa hivi sasa hivi katika malengo yake kwamba ameiangalia zaidi mashirikiano baina ya Sekta binafsi na  Serikali na bila ya kushirikiana na Sekta Binafsi basi tutchelewa sana kufanya maendeleo. Serikali tunategemea iwe inatoa huduma zaidi bora kwa wananchi lakini yale mipango mengine Sekta Binafsi iweze ku-*play role* yake kwa sababu kwanza watakuwa na fedha nyingi lakini watakuwa na *technology* nyingi ambayo itaweza kuja kutusaidia.

Kwa hiyo, kitu muhimu hapa Mheshimiwa yaani tunazo hizi *vocational training* lakini Mhe. Spika, bado ukiangali mazingira ya Vyuo vyetu vya Amali hali yake sio nzuri hawana vifaa vya kutosha hawana walimu wakutosha kwa sababu hiyo miradi yote ianayokuja mfano kama kwa upande wa Uchumi wa Buluu kule kutahitajika wafanyakazi wengi ambao wengine watatakiwa wawe na elimu kubwa wengine elimu ndogo sasa hivi Vituo vyetu vya Elimu ya Amali vitatusaidia sana katika kuandaa vijana wetu katika kuingia katika soko la ajira.

Mhe. Spika, jengine tuna tatizo kidogo katika Elimu ya Juu, kwanza tunaishukuru sana serikali yetu kwa kutoa elimu bure au kusema elimu bila ya malipo maana ukisema bure mwananchi hata kiatu cha mtoto wake anasema tumeambiwa elimu bure. Lakini kutoa  elimu bila ya malipo kwa kweli tunaishukuru sana serikali lakini bado katika Elimu ya Juu kuna tatizo tunaomba hili Mhe. Spika, serikali yetu ilizingatie hasa katika hii maandalizi ya Bajeti inayokuja. Mhe. Spika, bado wananchi wetu wanajitahidi lakini wanyonge leo katika Elimu ya Juu kwa Vyuo vya ndani serikali yetu *Alhamdulillah* ina-*support hundred percent*. Lakini kwa wale wanafunzi ambao wanasoma vyuo vya nje ya nchi inabidi mwananchi achangie karibia asilimia 50. Kwa sababu wao wanachangia *tuition fee* lakini masuala ya *accomodation, transport* na vitu vyengine inabidi huyo mzazi achangie kutokana na hali ya watu wetu.

**Mhe. Spika:** Anza kuhitimisha Mhe. Hamza Hassan Juma.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** kutokana na hali yetu Mhe. Spika, wanakuja kutuvamia sisi. Sasa ukiangalia hali Mwakilishi, huku kuna vuja na huku kuna barabara mbovu halafu watoto uwasomeshe vyuo vikuu itakua shida kidogo. Kwa hiyo, hili nafikiria serikali imeshasikia.

Mhe. Spika, ingawa nina mengi lakini la mwisho kabisa ni suala la jimboni. Tumeona hapa Mhe. Rais ameeleza namna gani nia yake ya kuboresha barabara mbali mbali katika upande wa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 19 ameeleza ya kwamba ataboresha barabara kuu lakini vile vile na barabara za ndani. Mimi katika jimbo langu Mhe. Spika, kuna jambo ambalo linanipa dhiki na ninapata tabu sana hasa unapokaribia wakati wa uchaguzi nakuwa sipati usingizi. Barabara ya Mboriborini. Kwa kweli barabara hii Mhe. Spika, kuna ahadi ya Mhe. Rais wa Awamu ya Sita, Rais wa Awamu ya Saba rafiki yangu Mhe. Al-Hajj Haji Omar Kheri aliniahidi imo katika mpango, akanipa mpaka *engineer*, wakanipa mpaka makisio.

**Mhe. Spika:** Mhe. Hamza Hassan Juma muda wako wa kuchangia umekwisha.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Kwa hiyo Mhe. Spika, nilikuwa naomba Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ aliyekuwepo sasa hivi basi tushirikiane katika kukamilisha ile ahadi ya Waheshimiwa Marais Wastaafu ambao Mhe. Rais wa sasa ameiridhi. Mhe. Spika, naiunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana. Naomba nimwite Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Harusi Said Suleiman kama muda utakuwa unaruhusu nitampa ajiandae.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii adhimu kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema ambaye ametujaalia uhai na uzima na kuweza kufika hapa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ambayo tumepangiwa.

Mhe. Spika, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia na naamini kwamba kwa dakika ambazo zimebakia basi utanipa fursa nimalizie yale ambayo nimekusudia kuongea.

Mhe. Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushindi mkubwa wa kishindo ambao ameupata katika uchaguzi wetu mkuu wa 2020. Vile vile, nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuteuwa wasaidizi wake wawili akiwepo Makamu wa Pili wa Rais na Makamu wa kwanza wa Rais na tunaona kwamba kwa sasa kwa kasi ambayo Mhe. Rais mwenyewe anaitaka wanakwenda sambamba na wasaidizi wake.

Vile vile, nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kututeulia Mawaziri ambao ni nguvu mpya lakini pia ni mawaziri ambao tuna imani kwamba watatutoa hapa tulipo na kutufikisha mbele ambapo tumekusudia.

Mhe. Spika, napenda pia kukipongeza Chama changu cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa, nawapongeza wananchi wa Zanzibar kwa amani na utulivu. Lakini vile vile, nawapongeza sana

vyama vyengine ambavyo vimekubali kushirikiana katika kulijenga taifa letu. Baada ya pongezi sasa naomba sasa nichangie Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, ni mambo machache sana ambayo nitayazungumza zaidi na kama Mhe. Rais alivyosema nataka nirudie yale ambayo ameyasema kwa kuwa alikuwa na nia ya dhati kabisa ya kuleta Mapinduzi ya Kiuchumi.

Mhe. Spika, mzungumzaji ambae ametangulia kabla yangu alizungumzia suala hilo kwa kuona kwamba umuhimu mkubwa sasa hivi tunauelekeza katika uchumi na hiyo ndio faraja ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, katika Hotuba yake Mhe. Rais, amezungumzia sekta mbali mbali ambazo zitatusaidia katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.  Moja katika sekta ambayo nitaizungumzia ni Sekta ya Utalii. Mhe. Spika, naizungumza hii kwa sababu nina *interest* kubwa kwenye masuala haya ya utalii. Kwa ufupi kabla ya kuzungumzia sekta hii, nitazungumzia Uchumi wa Bluu ambao Mhe. Rais amekuwa akiusisitiza sana katika hotuba zake mbalimbali.

Mhe. Spika, Mhe. Rais anapozungumzia Uchumi wa Buluu anakusudia kwamba ni ile bahari imetuzunguka ambayo Mwenyezi Mungu katujaali kuwa nayo na kwasababu eneo la ardhi tulilokuwa nalo ni dogo, kwa hiyo tunaweza kutumia bahari tuliyonayo ili kuhakikisha kwamba maendeleo yetu ya kiuchumi yatakuwa ni maendeleo ya kasi kubwa.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu, wengi huwa wanasema kwamba Uchumi wa Buluu ni kitu kipya kwetu sisi, lakini mimi ninasema kuwa sio kitu kigeni kwa Zanzibar kwa sababu tayari tumekuwa na  rasilimali ya bahari kwa muda mrefu tangu enzi na dahari, wazee wetu wakiitumia kwa ajili ya kupata kipato mbalimbali ikiwemo, uvuvi.

Mhe. Spika, nasema hilo kwa sababu bahari yetu imegawanyika kwenye sehemu tatu. Bahari ya sasa hivi ambayo tunayoitumia kama fukwe ambayo inatumika sana kwa shughuli za Utalii, lakini kuna na bahari ya katikati ambayo ni kama maili 12 ambayo inashughulika zaidi na masuala ya uvuvi. Vile vile, kuna bahari kuu ambayo inajumuisha masuala ya uvuvi na masuala ya gesi asilia na mafuta. Kwa hiyo, hizo bahari zote ukubwa na upana huo wa Uchumi wa Buluu unatupa fursa kubwa sana ya kuweza kuona namna gani tutaweza kutumia bahari katika masuala mbalimbali ya kiuchumi.

Mhe. Spika, nianze na uvuvi ambao tunajua kwamba wananchi wengi wakawaida wanaoishi katika maeneo mbali mbali ambayo yapo karibu na bahari wanautumia uvuvi kama ni kipato chao cha kiuchumi na wananchi hawa bado wanataka *support* kubwa sana kutoka serikalini. Kwa kuwa tumeona kwamba vifaa vyao vingi ambavyo wanavitumia ni vifaa ambavyo vipo katika mazingira yale yale ambayo tumekua nayo lakini vile vile tumekuwa na taaluma ambayo bado inatumika ni ile ile ya kileo. Ningeomba sana serikali hii sasa itoe elimu lakini pamoja na vifaa vizuri vya kisasa vyenye teknolojia ya kisasa ambayo itawasaidia wananchi wanaoishi pembezoni mwa bahari kwa ajili ya kupata pa kuongeza kipato katika shughuli zao za uvuvi.

Mhe. Spika, mbali na hayo, Kwa kuwa Mhe. Rais wetu aliahidi fursa za ajira basi fursa nyingi zitatoka katika maeneo kama hayo. Kwa hiyo suala zima ambalo wamelizungumzia suala la viwanda, nadhani lipewe *first priority* na mtizamo maalum kuhakikisha kwamba katika shughuli hizi za uvuvi basi viwanda vinavyoshughulika na kusindika mazao ya baharini ni viwanda ambavyo ni muhimu sana kwa ajili ya kupatika ajira hizi.
Mhe. Spika, msemaji mwenzangu aliyetangulia amezungumzia suala zima la Vyuo vya Amali. Vyuo vya Amali tunavyo vingi lakini bado havijaweza kutoa elimu ya kutosha ya kuweza kuwafanya hawa ambao wanatoka katika vyuo vile wanaweza kufanya shughuli mbali mbali za kiuchumi katika maeneo yao. Kwanza vyuo vile havina walimu wa kutosha, lakini pia havina vifaa vya ufundishaji ambavyo vitatengeneza vijana wale warudi katika maeneo yao ya kuweza kufanya shughuli za kiuchumi.

Mhe. Spika, ningeomba sana kufanywe utafiti maalum. Utafiti huu usiwe wa ujumla wake, kwa sababu katika kila eneo kama tutagawa, maeneo kiuchumi tutaona kwamba kuna aina ya uvuvi fulani ambao unafanyika. Kwa mfano kuna maeneo mengine ambayo utakuta kwamba kuna uwezekano wa kupatikana majongoo mengi lakini kuna maeneo mengine uwezekano wa kilimo cha mwani na kuna maeneo mengine uwezekano wa kufanya uvuvi wa samaki wakubwa. Hivyo, katika kila eneo ambavyo vyuo hivi vya amali viliovyo mitaala yake ielekee huko baada ya kusema wanafanya mitaala kwa ujumla wake. Kwa hiyo, Mhe. Spika, naomba hilo tuliangalie vizuri sana.

Mhe. Spika, nikizungumzia kwa mfano, kina mama wengi wanafanya shughuli za mwani na kwa bahati nzuri sana kina mama hawa wanahangaika sana kuhakikisha kwamba shughuli ya mwani inafanyika na wanapata kipato kizuri lakini kuna suala zima la kuongeza ubora wa bidhaa. Mhe. Spika, kwa dakika ambazo zimebakia naomba uniachie niendeelee tu mpaka mwisho *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa…

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Spika, unanikumbusha lakini dakika nilizozitumia ni sita tu mpaka sasa hivi…

**Mhe. Spika:** Hapana Mhe. Mgeni Hassan Juma, bahati mbaya nina *time keeper* hapa, tunamtumia, naomba umalizie Mheshimiwa.

**Mhe. Mgeni Hassana Juma:** Mhe. Spika, nimeanza kuzungumza kasoro robo.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mgeni Hassan Juma nina *stop watch* hapa natumia.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Spika, naomba uniachie kidogo nimalizie. Mhe. Spika, suala zima ninalotaka kulizungumzia ni kuhusiana na mfumo wetu huu ambao tunatoa wa elimu. Hilo ni jambo muhimu kwa sasa kulitizama, kwa sababu tumesikia kwamba kuna mabadiliko ambayo yatafanyika. Lakini Mhe. Spika, mara nyingi tunatengeneza katika *academicians* katika mfumo wetu wa elimu, hawa watu wa katikati ambao wengi wana *drop* skuli wakiwa *form two* au *form four* hawa ndio wa kuingia kwenye hivyo vyuo na humo ndimo mna vipaji maalum.

Mhe. Spika, sasa hebu tuangalie tena mitaala kuhusiana na mwani ili tuwarithishe watoto wetu namna gani mwani unavuliwa na namna gani mwani unafanya kazi. Tumewaachia kina mama peke yao, tukiwapa mafunzo madogo madogo tuingize kwenye mitaala. Uvunaji wa majongoo halikadhalika.

Mhe. Spika, ninataka kusema sio kwa umuhimu wake lakini nitaka kuseme na naomba unipe muda nilizungumze hili ni kuhusiana na Utawala Bora na nidhamu. Mhe. Rais amelizungumzia sana suala la nidhamu. Mhe. Spika, naomba unipe dakika mbili tu ili niweze kumalizia.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mgeni Hassan Juma samahani

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Spika, nataka kuzungumzia…

**Mhe. Spika:** Subiri kidogo Mhe. Mgeni Hassan Juma

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Naam.

**Mhe. Spika:** Nitakuongeza huo muda yaani utakuwa ndio mchangiaji wa mwisho wala hakuna tatizo lakini labda nikumbushe kuwa Waheshimiwa hii sio bajeti. Mawazo haya mengi sana wakati wa bajeti yatawasaidia sana Mawaziri, hii ni Hotuba ya Mhe. Rais na tuna orodha kubwa sana ya watu ambao wangetaka kuchangia ambao bado wamebaki kwa ajili ya kuchangia. Nakuruhusu Mhe. Mgeni Hassana Juma kwa vile unasisitiza na ndio Msaidizi wangu Naibu Spika, kwa hiyo endelea *(Makofi)*

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Spika nakushukuru sana kwa busara na hekma zako ambazo umekuwa ukizitumia siku zote wakati ukituongoza. Mhe. Spika, nazungumzia suala zima la Utawala Bora. Nimezungumzia suala hili kwa sababu lina umuhimu wake mkubwa katika kusaidia kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika tuna *gap* kubwa sana kuhusiana na suala la Utawala Bora lakini zaidi ni kwamba tuna matatizo ya kutoa huduma katika maeneo yetu mbali mbali. Hilo ni tatizo na limekuwa sugu kwa Zanzibar. Mimi nimefanya kazi serikalini nalielewa vizuri na nadhani wengi wanaelewa kwa sababu sote ni sote ni jamii na tunapata huduma mbali mbali na tunaona namna gani watendaji wanashindwa kuwajibika. Sio tu kwa sababu kwamba uajibikaji wao unahusu jambo fulani ambalo haliwezekani lakini ni kwa sababu hawataki kuwajibika. Kwa hivyo, hilo ni suala ambalo naomba nilisisitize hasa katika serikali hii na hasa katika viongozi kuhakikisha kwamba wanasimamia uajibikaji katika maeneo yao yanayohusika.

Jengine nilikuwa naomba na niliwahi kuomba nikaambiwa hili lipo nikazungumzia suala la *performance appraisal*. Mheshimiwa kumekuwa na tabia ya kuona watu wanapata vyeo au wanapata sifa kwa sababu labda anafahamiana au anajuana na fulani. Mheshimiwa mfumo huu kama utakuwepo *performance appraisal* kuona kwamba huyu kafanya na nini kakifanya, lazima tujaribu kuhesabu au kujua jambo gani ambalo limefanya na mtu fulani na ndio maana akapata nafasi hii. Mhe. Spika, nafikiri hilo ni jambo muhimu sana.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa niungane na wenzangu kwa kumuunga mkono Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapiduzi kwa hotuba yake nzuri kabisa na mwanana na kama alivyosema mwenzangu aliyetangulia kama ikiwa tunataka sasa kudadavua hotuba hii ambayo ameitoa Mhe. Rais basi tutaweza kuichambua na mambo mengi sana, na wewe umetwambia kwamba tuna nafasi nyengine nzuri ya kuweza kuzungumzia masuala ambayo Mhe. Rais ameyaelezea katika kitabu hiki.
Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa uvumilivu wako, nakushukuru kwa nafasi ambayo umenipa ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe muda uliobaki haumtoshi Mheshimiwa ambaye nilimtamka, lakini sasa atapata fursa ya mwanzo tutakapokuja jioni. Kwa hivyo, naomba niwataje watu watatu ili wajiandae wawepo karibu tutakapoanza.

Mhe. Harusi Said Suleiman ambapo atafuatiwa na Mhe. Kombo Mwinyi Shehe na Mhe. Mtumwa Peya Yussuf hao wajiandae ndio watakaokuwa watu wa mwanzo jioni. Baada ya maelezo hayo machache naomba sasa kuakhirisha Baraza mpaka saa 11 jioni.

*(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Mwongozo wa Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum

**MWONGOZO**

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, nimesimama kuomba mwongozo wako kwa kutumia kanuni ya kifungu cha 64(3) naomba kununukuu kidogo.

Kifungu cha 64(3) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi kinasema hivi;

> "Mjumbe anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna mjumbe mwengine anaezungumza na kuomba mwongozo wa Mhe. Spika, kuhusu jambo ambalo limetokea Barazani katika siku hiyo, ili Mhe. Spika atoe ufafanuzi kama jambo hili kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Baraza na majibu ya Mhe. Spika yatatolewa hapo hapo au baadae kadiri atakavyoona inafaa".

Mhe. Naibu Spika, jambo ambalo nataka kuomba muongozo wako kuhusiana na taarifa ambayo jana nilipokuwa nikichangia niligusia kuhusu mwenendo mzima wa benki yatu ya watu wa Zanzibar *PBZ* na tulimaliza. Lakini leo taarifa ambayo imekuwa *quoted* na vyombo vya habari baada ya mimi jana kumaliza baadae mchana Mhe. Rais amefanya maamuzi yake kuhusiana na yaani amebadilisha yaani ameteuwa Mkurugenzi Mtendaji mpya wa benki. Leo baadhi ya vyombo vya habari vikaunganisha maneno ambayo niliyozungumza jana na maamuzi ya Mhe. Rais.

Sasa naona jambo hilo nataka tu kupata muongozo wako au utaratibu ambao itabidi tuufate kuhusiana na jambo hilo kwamba wanaunganisha mazungumzo yangu au mchango wangu ambao nimeutoa jana lakini leo taarifa iliyotolewa wameunganisha ule mchango pamoja na hilo lililotokea, naomba muongozo wako Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, hoja yako ni kwamba yale yaliotolewa sio sahihi au hoja yako inaelekea wapi.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Mhe. Naibu Spika, hoja yangu ni kwamba muunganisho ambao umetolewa na vyombo vya habari leo sio sahihi. Mimi nimechangia na nimechangia kwa mujibu nilivyokuwa naona Mhe. Rais amefanya maamuzi na anayo haki ya kufanya maamuzi muda wowote ambao yeye anahisi unafaa. Bahati mbaya hata hao walionukuu wamesahau kuona barua ile ambayo Mhe. Rais ameitoa ilikuwa imetoka tarehe 10/02/2021 wakati mimi nimechangia jana tarehe 11/02/2021 kwa hiyo naomba muongozo wako utaratibu ambao inabidi tuufate kuhusiana na tukio kama hilo lisije likajitokeza tena, ahsante.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Mjumbe, kwa kifungu hicho hicho ambacho umekielezea kifungu 64(3) tunamabano (2) inasema “Spika anaweza ama hapo hapo kutoa maamuzi juu ya jambo hilo na utaratibu wake au wakati tutakapokhairisha kikao tutaweza kulijadili hilo” kwa hiyo nadhani ni bora zaidi tukaingia zaidi katika jambo hili ili kuweza kutoa maamuzi baada ya kuwa tumepata hasa usahihi wa jambo lenyewe. Nashukuru sana, tunaendelea.

Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea na mchangiaji wetu wa mwanzo ni Mhe. Harusi Said Suleiman ajitayarishe Mhe. Kombo Mwinyi Shehe na atafuata Mhe. Mtumwa Peya Yussuf. Mhe. Harusi Said Suleiman karibu.

**Mhe. Harusi Said Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nichukuwe nafasi hii kumshukuru Allah *(S.W)* na kumtakia rehma Mtume wetu Muhammad *(S.A.W)* kwa kutuwezesha kukuwepo hapa kutekeleza majukumu yetu ya matakwa katiba. Ni dhahiri kwamba tunapaswa kumshukuru kwa sababu wapo wenzetu ambao walitamani na wengine walithubutu lakini hawakujaaliwa kuingia. Mhe. Naibu Spika, pili nakupongeza wewe binafsi pamoja na Mhe. Spika kwa kuchaguliwa katika nafasi zenu za kutuongoza kwa kura za asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Bazara la Mapinduzi kwa ushindi mkubwa alioupata pamoja na tabia yake ya kumtanguliza Mwenyezi Mungu. Tabia ambayo imemjenga ujasiri na kujiamini katika kutuongoza. Mhe.

Naibu Spika, sasa niende kwenye lengo nililokusudia nalo ni kuipongeza hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliyoitoa wakati wa uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi kwa ufupi hotuba hii imeonesha dira na dhamira ya uongozi halisi kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, hotuba hii imerudisha matumaini kwa wale ambao walikata tamaa kwa baadhi ya mambo na kuwajenga ujasiri kuweza kusimama kupambana na kuendelea kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Mhe. Naibu Spika, hotuba hii ambayo leo tunaijadili kwa kweli imeshajadiliwa sana wananchi katika maeneo yao mbali mbali, kuanzia siku ya tarehe 11 Novemba, 2020 Mhe. Rais alipoiwasilisha. Mhe. Naibu Spika, wanamichezo, wafanyabiashara mbali mbali, wafanyabiashara wa masokoni, watu wa dini mbali mbali, wafanyakazi, wachukuzi, hata wananchi wakiwa kwenye usafiri yaani madaladala walitumia nafasi yao kuzungumzia hotuba ya Mhe. Rais na kuonesha kuwa wanayo matumaini makubwa ya uongozi wake katika kuendeleza ukuaji wa uchumi wetu, kuimarika kwa utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi na nakadhalika.

Mhe. Naibu Spika, hotuba hii pia imeelekeza sekta zote ambapo ukurasa wa kumi na tisa ilizungumzia ujenzi wa barabara mbali mbali ikiwemo barabara ya Wete Chake. Mhe. Naibu Spika, barabara hii kwa kweli ni mbovu na ni barabara muhimu sana kwa wananchi wa Pemba. Mhe. Naibu Spika, wakwezi na wakulima hutumia barabara hii kupitisha bidhaa kutoka sehemu moja na kuingiza sokoni eidha iwe soko la Chake Chake au soko la Wete. Hali hii husababisha usumbufu mkubwa na kupelekea kutumia pesa nyingi katika usafirishaji wa bidhaa zao. Mhe. Naibu Spika, kutokana na usumbufu huu unaopata wananchi na ukizingatia dhamira njema ya serikali yetu ya kuendelea kuwawezesha wananchi kuondokana na umaskini basi naiomba wizara inayohusika kutoa kipao mbele kwa barabara hii ya Wete Chake kuwa ya awali kati ya barabara zitakazojengwa kupitia ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi nah ii hotuba ya Mhe. Rais ya tarehe 11 Novemba 2020.

Mhe. Naibu Spika, katika dhamira njema ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuendelea kuinuwa uchumi wa Zanzibar ni vyema lengo la kujenga na kuimarisha bandari zetu na viwanja vya ndege litekelezwe haraka na kwa viwango vinavyofaa. Naipongeza saana hotuba ya Mhe. Rais kwa kuiona bandari ya Wete kuwa ni moja kati ya bandari zinazohitaji kujengwa.

Mhe. Naibu Spika, bandari ya Wete ni kilio kikubwa na cha mda mrefu kwa wananchi wa Pemba hususani wananchi wa Mkoa wa Kaskazini. Bandari ya Wete ina uwezo wa kuegesha, kuondosha na kupokea vyombo vingi kwa wakati mmoja kutokana na uhalisia wake na kusababisha mapato ya serikali kuongezeka. Hivyo basi naiomba serikali kupitia wizara husika kutoa nafasi ya mwanzo kwa bandari ya Wete kati ya bandari zitakazopata nafasi ya kujengwa ili tatizo la bandari ya Wete liweze kutatuka na serikali iweze kupata mapato kupitia bandari ya Wete.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wa jimbo la Wete wanampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Bazara la Mapinduzi kwa ujasiri aliyouonesha kwa kuonana na wananchi wa makundi mbali mbali ya kijamii yakiwemo makundi ya viongozi wa dini, makundi ya wafanyabiashara, makundi ya walimu wa madrasa, makundi ya wafanyakazi na wafanyakazi wa gereji, wajasiriamali, wavuvi, wajane nakadhalika, pamoja na kufungua Mahakama ya

Udhalilisha na kuiamuru kufanya kazi mara moja. Kwa kweli, wananchi wa jimbo la Wete wamekiri kwamba huu aliyouonesha Mhe. Rais ni ujasiri mkubwa na wanamtakia kila la kheri katika uongozi wake.

Mhe. Naibu Spika, mwisho na sio kwa umuhimu bali ni kwa kujali muda nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais kwa uteuzi aliyoufanya wa viongozi wetu wakiwemo Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Mwenyezi Mungu amrudishie afya yake *In sha Allah*, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, Mawaziri wetu majasiri pamoja na watendaji wote walioteuliwa.

Namalizia mchango wangu huu kwa kuwashuru wananchi wote wa Zanzibar kwa kuendelea kukiamini Chama cha Mapinduzi kwa kumpa kura nyingi na za ushindi mgombea alieletwa na Chama cha Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi na kusababisha kura zao na upendo wao kwake leo ni kuwa ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwa kweli, imani hii waliionesha wananchi kwa Mhe. mgombea kupitia Chama cha Mapinduzi ni imani kubwa na tunawaomba waendelee kumpa mashirikiano kwa yale yote ambayo anayafanya katika uongozi wake. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na nawashukuru pia wananchi wa jimbo langu la Wete kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa mwakilishi wa jimbo la Wete na nawaomba waendelee kunipa mashirikiano kwa manufaa ya jimbo letu la Wete. *(Makofi)*

Namalizia kwa kuipongeza sana familia yangu akiwemo mama yangu mzazi, mume wangu, wake wenzangu pamoja na watoto wangu. Wamenionesha upendo mkubwa na mashirikiano makubwa hadi kufanikiwa kupata kuingia katika Baraza lako tukufu. Nachukua nafasi hii adhimu kuunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Harusi Said, mchangiaje anaefuata ni Mhe. Kombo Mwinyi Shehe anafuata ni Mhe. Mtumwa Peya kwa bahati mbaya nimepata taarifa kwamba amepata dharura jimboni kwake na nitampa nafasi Mhe. Abdalla Abasi Wadi. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe karibu.

**Mhe. Kombo Mwinyi Shehe:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu ambae ametujaalia jioni hii kuwepo hapa tukiwa wenye afya kwa wingi wa shukurani nisema *alhamdulillahi.* Nitakuwa mkosefu wa fadhila endapo nitaacha kukishukuru chama changu cha ACT Wazalendo kupitia kiongozi wake mkuu ndugu Zitto Zubeir Kabwe na Mwenyekiti wetu Maalim seif Sharif Hamad kwa kunipa imani na kuniteuwa kupeperusha bendera kupitia chama changu cha ACT katika jimbo la Wingwi. Halikdhalika niwashukuru wana Wingwi wote kwa heshima hii walionita kwa kuniamini kuja kuwatumikia katika eneo hili muhimu sana miwaahidi kuwa nitatenda lile ambalo kuwa wamenituma na katu sitowaangusha.

Mhe. Naibu Spika, niende moja moja kwenye kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais kwa kuzingatia maeneo yafuatayo. Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kusema ni kweli na ni wazi kabisa kuwa serikali ya awamu ya nane ina dhamira thabiti ya kuwatumikia wazanzibari na naamini kwamba

imekusudia kuwaonyesha wazanzibar matunda ya Mapinduzi na sio simulizi za Mapinduzi na Muungano.

Mhe. Naibu Spika, nayasema haya kwa sababu zifuatazo. Naomba niseme hivi, wakati serikali ina dhamira ya kwenda kutekeleza haya yote ambayo ameyagusa Mhe. Rais kuna haja ya serikali kuangalia ni changamoto gani zilijitokeza kupitia serikali ya awamu iliopita, ili twende sambamba kuzifanyia kazi sambamba na serikali hii ya awamu ya nane, nina maana gani. Kwa mfano waswahili wanasema tunajifunza kutokana na makosa.

Mhe. Naibu Spika, naomba niendelee kwenye mchango wenye ukurasa wa kumi na moja eneo la utalii. Mhe. Naibu Spika, kwa muono wangu ninavyoona katika eneo hili ziko changamoto na naiomba serikali izifanyie kazi changamoto hizi kama ifuatavyo. Ni imani yangu kuwa eneo la utalii ni eneo ambalo kuwa linaweza kuiongezea serikali mapato kwa hali ya juu ila ziko changamoto kama ifuatavyo.

Mara nyingi wawekezaji wetu wanapokuja kuwekeza katika maeneo kama haya ya kitalii, serikali ama inashindwa kuwapa taaluma ya kutosha katika kutumia yale maeneo wanayotaka kuwekeza na jambo hili mara nyingi linaweza kuleta migogoro sana katika maeneo ya vijiji kama vile ama jamii inashindwa kupewa taaluma juu ya namna gani ya uwepo wa mwekezaji yule katika eneo lile. Tukiangalia *reference* huko nyuma katika maeneo haya ya kitalii maeneo mengi kunatokezea migogoro niiombe serikali wakati tunaendelea kulifanyia kazi zoezi hili la sekta ya utalii tujaribu kuziangalia changamoto hizi na nyengine kuwa ambazo nadhani mimi sijazitaja ili zifanyiwe kazi kabla ya kueleka huko.

Sambamba na hilo naomba nielekeze mchango wangu kwenye ukurasa namba kumi na sita eneo la biashara na viwanda. Mhe. Naibu Spika, biashara ni eneo pia ambalo lina wadau wengi ndani ya nchi yetu hii mfano hai angalia Darajani kuna vijana wetu wengi wamewekeza katika eneo hili. Ushauri wangu kwa Serikali hebu tujaribuni kuwapunguzia kodi wafanyabiashara, kwa sababu unapompunguzia mfanyabiashara kodi, nina imani atafanya kazi katika mazingira rasmi na kipato kitapatikana na wakati huo huo watapata nafasi ya kulipa kodi kama kawaida.

Kwa mnasamba huo, mtu huyu endapo kama utampunguzia kodi nina imani na mwengine atakuja kuongeza kufanya biashara ile, ninaamini haba na haba hujaza kibaba kwa mujibu wa muono na maelezo ya Mhe. Rais wetu anasema yeye ni muumini sana wa kodi ndogo. Kutokana na hali hiyo, naomba tu kweli kodi ni eneo moja ambalo tunalitegemea sana, lakini pia tukipunguza kodi watu wetu wataweza kufanya biashara kwa wingi na serikali itapata mapato kwa wingi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwa upande wa eneo la viwanda hili ni eneo muhimu sana katika serikali yetu hii nina imani kama litafanyiwa kazi litaweza kuongeza ajira kwa vijana wetu,. Kwa hivyo, naiomba serikali pale anapotokezea muwekezaji kwa eneo kama hili la viwanda basi ni vyema wahusika wa eneo lile nao wapewe taaluma lakini pia na wahusika wa eneo lile wasikoseshwe ajira. Tunaona na tuna mifano mingi kuna viwanda vinajengwa katika meeneo mbali mbali lakini ajira zinakuwa ni shida kwa wale watu ambao wanazunguruka eneo la kiwanda, naomba sana serikali katika kuzingatia utekelezaji wa masuala haya na hilo pia waliangalie.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye ukurasa wa 25 inazungumzia sekta ya elimu nakumbuka serikali ya awamu ya saba ilijenga Skuli za Sekondari kwa kila Wilaya kwa dhamira ya kukusanya wanafunzi wa michipuo kupitia skuli zile zilizomo ndani ya wilaya, lakini niseme kwa bahati mbaya skuli hizi hazikuwahi kujengewa madakhalia jambo ambalo limepelekea zile skuli mpaka leo kuweza kutumika kwa lengo lililokusudiwa. Kwa mfano hai niseme katika skuli yangu ya Chwaka/Tumbe iliyomo kwenye jimbo la Wingwi skuli hii uwepo wake umelazimisha kuua skuli ya Sekondari ya Sizini jambo ambalo nikuombe sana Mhe. Waziri wa Elimu wana Sizini wanataka skuli yao, Skuli ya Sizini ilichukuliwa kinyemela na kupelekwa Chwaka/Tumbe wenyewe watu wa Sizini wanataka skuli yao kwa maana wameijenga kwa jasho lao wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu baada ya hayo machache niliyoyazungumza nikushukuru na niunge mkono hoja mia juu ya mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Mjumbe kwa mchango wako na anayefuata ni Mhe. Abdalla Abass Wadi na ajitayarishe Mhe. Suleiman Makame Ali.

**Mhe. Abdalla Abass Wadi:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru wewe pamoja na Mhe. Naibu Spika, lakini kwa heshima kubwa kabisa nampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Nungwi, hasa kwa ushindi mkubwa sana aliotupatia katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Pia Mhe. Naibu Spika mimi binafsi pamoja na wapiga kura wangu nakwambia kwamba hatuna mashaka na yeye na serikali yake pamoja na wale wote aliowateua, kwa hivyo wote kwa pamoja nawapongeza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja niende katika ukurasa wa kumi na moja ambao unazungumzia suala la utalii, suala hili Mhe. Naibu Spika, katika Jimbo langu la Nungwi ndio liliko hasa ukilinganisha Zanzibar nzima basi Nungwi linafanyika zaidi, kwa sababu mtu muwache atoke anakotoka kokote kule Ulaya, Asia wapi lakini akiigusa Zanzibar kama hajaigusa Nungwi basi anajiona bado hajaja kufanya utalii katika nchi yetu hii.

Kwa maana hiyo, basi namuomba Mhe. Waziri anayehusika na sekta hii ya utalii aiangalie sana Nungwi kwa hali yake ilivyo hivi sasa hasa katika ujenzi wa barabara za ndani ambao zimetoka katika barabara kuu zikaelekea mahoteli, zile barabara kusema kweli ni mbaya sana kwa hivyo tunamuomba Waziri mwenye zamana aje kule Nungwi aziangalie barabara zile na kama itawezekana basi kama alivyotambia Mhe. Rais katika kitabu chake hichi basi zishughulikiwe haraka sana.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nizungumzie kidogo kuhusu suala la elimu mimi mwenyewe kwa kuwa nilikuwa mwalimu lakini sasa hivi nimeshastaafu nalijua sana suala hili, pale petu pale kuna skuli wananchi wamezijenga na hivi sasa zinasubiri kuezekwa kwa ushirikano mkubwa sana wananchi wamekaa pamoja kwa kushirikiana na viongozi wao wa jimbo, wadi na hata matawi kwa kuzijenga skuli zile mwaka sasa hivi lakini bado hazijaezekwa. Kwa hivyo, vile vile namuomba Mhe. Waziri wa Elimu kwa kushirikiana na serikali kuu basi skuli zile waje kuziezeka tushirikiane pamoja na sisi viongozi wa jimbo tuziezeke, kwa sababu hivi sasa sisi viongozi wa jimbo mimi na Mbunge na Madiwani tumo katika harakati hizo za kuziezeka lakini

nguvu zetu ni chache, kwa hivyo tunaiomba serikali ije kuungana na sisi ili tupate kuziezeka skuli zile.

Mhe. Naibu Spike, nije katika upande wa afya vile vile katika Jimbo langu la Nungwi tunavyo vituo vya afya ambavyo havina uzio na vituo vile kila siku tunaripotiwa tukiamka tu kwamba leo umefanyika uharibifu na watu wasioitakia mema nchi hii. Kwa hivyo, tunaiomba serikali pamoja na Wizara ya Afya ije kuvishughulikia vituo vile kwa kuvijengea uzio, kwa mfano kama kituo cha Nungwi, Tazari na Kidoti hivi ni vituo ambavyo kila siku wanakwenda waharibifu wanaviharibu.

Mhe. Naibu Spika, halafu nije kwa upande wa michezo hii ni sekta muhimu sana kwa upande wa nchi yetu kwani tumeshuhudia mnamo miaka ya 1970 na 1980 ilikuwa Zanzibar haikamatiki kwa michezo ya *football* na riadha, lakini hivi sasa michezo ile imepotea kabisa kabisa. Kwa hivyo, natoa ushauri kwa Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo basi atupitie kule Nungwi tufanye mikutano kwa pamoja angalau kidogo apate kuonana na wale wadau wa michezo, ili tulizungumze suala hili, huenda Mwenyezi Mungu labda atatujaalia tukarudi kama miaka ya 1970 na 1980. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi ni mwanamichezo mkubwa sana na katika taaluma yangu basi nimefanya Diploma ya michezo kwa hivyo hii shughuli naijua vizuri sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anitumie kwa shughuli hizi za michezo na nitamsaidia pamoja na serikali bila ya shaka yoyote ile. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Michezo nakuomba sana pale atakaponafasika basi anitumie mimi ni mtaalam kidogo wa michezo. *(Kicheko/Makofi)*

Halafu kwa jumla tukiizungumzia hotuba hii basi ni hotuba iliyojaa busara na mwenendo mzuri wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi.

Kwa hivyo, kwa upande wa hotuba hii basi sina matatizo nayo kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Nungwi tunampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa huu muda mfupi tu wa siku mia tumeona maendeleo yake makubwa sana aliyofanya na tunampongeza.

Hivyo kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii mia kwa mia ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Abdalla Abasi Wadi, anayefuatia ni Mhe. Suleiman Makame Ali ajitayarishe Mhe. Panya Ali Abdalla, bada ya hapo atafuata Mhe. Huzaima Mbarouk Tahir.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais. Lakini, kabla ya kuchangia kwanza nishukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kutupa afya njema kuweza kusimama hapa mbele ya Baraza lako hili na kuweza kutoa michango yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar lakini vile vile akamteua Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais kwa kuona kwamba hao ni viongozi wa kuweza kumsaidia kazi katika serikali yetu hii, pamoja na mawaziri wote.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa kumi na moja kuhusu masuala ya ufugaji wa samaki kwenye uchumi wa buluu, hapa Mhe. Rais alieleza mambo mengi sana katika kitabu chake hichi cha hotuba mazuri na ya kufanyiwa kazi ya kimaendeleo yenye kuleta maslahi katika Zanzibar yetu.

Lakini katika suala hili la ufugaji wa samaki wale wanaotaka kufuga samaki kule vijijini vizuri wapewe taaluma ya kuhakikisha kwamba wanafuga samaki wale wanaofugika. Kwa kweli, sababu kuna mabwawa mengi yameanzishwa kwa wafugaji samaki lakini hawana taaluma hawajui ule utaratibu wa ufugaji wa samaki na hawajui samaki gani anaweza kuishi katika bwawa mwisho wake hawafanikiwi katika masuala ya miradi hii.

Vile vile serikali inatoa vifaranga vya samaki vifikavyo milioni kumi kuwapa wafugaji hawa, hapa ndio pale pale kwenye suala la taaluma serikali itajikita katika kutoa vifaranga hivi, lakini wale wanaokwenda kupewa basi waweze kuwa na taaluma ya kuweza kuwafuga samaki hawa kujua kwamba samaki huyu anafugwa katika maeneo gani.

Mhe. Naibu Spika, kwenye suala la ufugaji wa kaa, kamba na pweza nalo hili lizingatiwe, ili kuhakikisha kwamba tunapata uchumi katika sekta ya ufugaji wa mazao ya baharini. Kwa kweli, jana Mhe. Mussa Foum Mussa alisema hapa kwamba bahari Zanzibar bado nzima haijaguswa ni kweli, bahari ya Zanzibar bado hatujaitumia ipasavyo. Kwa hiyo, kama tutakumbuka katika kipindi cha serikali iliyopita ya awamu ya saba Mhe. Hamad Rashid alipokuwa Waziri wa Kilimo na Uvuvi alitwambia Zanzibar kuna vijana wamekwenda kupata mafunzo kwa ajili ya masuala ya uvuvi wa bahari kuu, na pia akapata kutuonesha zile boti za uvuvi zilizonunuliwa na serikali, lakini pia wawekezaji ambao kwamba wanataka kuwekeza katika sekta hii ya uvuvi hususan uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Naibu Spika, suala la uvuvi wa bahari kuu ni suala linaliweza kutupatia mapato Zanzibar kuhakikisha kwamba tunakula samaki na panakuwa na viwanda vya Samaki Zanzibar na kuona kwamba uchumi wetu unakuwa na vijana wanapata ajira kupitia sekta hii ya uvuvi wa bahari kuu. Hapa Zanzibar kuna uvuvi huu wa *long line* hata haujaanza bado, kwa hivyo mimi nina imani kwamba serikali hii ya awamu ya nane inayoongozwa na Mhe. Rais makini na shupavu Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, basi wananchi wafurahie yaliyo mengi mazuri kwa wale wavuvi wenzangu wanaotoka maeneo ya Tumbatu na maeneo ya Ndagoni kule kwa Mhe. Haji Omar Kheri tuhakikishe kwamba wavuvi wetu hawa wakae mkao wa kula mambo mazuri yanakuja.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye masuala ya mafuta na gesi suala hili la mafuta na gesi kwetu sisi Zanzibar itakuwa ni jipya, ili kuondoa migogoro hii isije ikatufika kama ilivyofika kwa nchi nyengine kwa sababu popote pale ambapo pana jambo la matumaini la kujenga uchumi katika nchi kwenye masuala haya ya mafuta kuna wengine wanatizama kwa jicho la husda.

Sasa Mhe. Naibu Spika, naomba kwenye sekta hii ya mafuta na gesi katika masuala yale ya kutafuta na uchimbaji wa mafuta wale wananchi wanaoathirika kwenye masuala ya makazi vilimo na mambo mengine basi wazingatiwe, kuhakikisha kwamba wanapewa zile fidia zao, ili waridhike na serikali iweze kufanya shughuli hii bila ya kuja kuingia mtu au kidudu mtu akaweka maneno kwa wananchi na tukapata vurugu kwenye masuala haya ya mafuta na gesi. Naiomba sana serikali kulizingatia hili walisimamie kwenye suala la fidia za wananchi.

Mhe. Naibu Spika, limefanyika zoezi hili la utafutaji wa uchimbaji wa mafuta kwenye maeneo ya Pemba huko sijui hapa Unguja iko vipi, lakini Pemba hadi leo hakuna mwananchi aliyelipwa fidia hata mmoja. Kwa hivyo, naiomba sana serikali kuhakikisha suala hili ili kuja kuondoa wale mahusda na vidudu mtu kuhakikisha kwamba wale wanaostahiki kulipwa fidia walioathirika kwenye nyumba zao na sehemu za kilimo waweze kupewa fidia zao, ili watoe ushirikiano katika masuala haya ya uchimbaji wa mafuta.

Lakini Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa wa kumi na saba kuhusu masuala ya kodi, bila ya kodi hatuwezi kwenda popote nchi yoyote inaendeshwa na kodi. Lakini kodi hizi ziangaliwe upya utitiri wa kodi kwa wafanyabiashara inafikia hadi wafanyabiashara wengine wanakimbia nchi kutokana na matatizo ya kodi. Kwa mfano hai, kule Pemba nadhani Mhe. Makamu wa Pili atafahamu nikizungumza kwamba kuna *Feasal Hardware* pale Chake Chake alipata hasara mpaka kufika kuondoka na kwenda nchi nyengine kuwekeza kutokana na masuala ya usumbufu anaoupata. Mhe. Makamu wa Pili nakuomba kwamba suala hili la kodi na suala la wafanyabiashara Pemba hususan kuhusu mizigo lifikiriwe, ili kuondokana wananchi wa Pemba wanaochukua makontena na kuyashushia Mombasa waweze kupata urahisi na biashara zao ziweze kufika kwa wakati kama walivyokusudia wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, mfuko mmoja wa saruji Pemba ni shilingi elfu kumi na saba hapa Unguja na shilingi elfu kumi na tatu na mia tano au elfu kumi na nne Pemba inakuwa mara mbili zaidi ya bei hiyo, mwananchi wa kawaida ikimfikia inakuwa ni tatu hata kupata hiyo saruji yenyewe na kuweza kujenga hiyo nyumba na hata akikaa hiyo nyumba ni taabani.

Kwa hivyo, naomba sana Mheshimiwa lakini suala hili Mhe. Rais alilizungumza katika mikutano ya hadhara mbali mbali alivyokuwa anaomba ridhaa kuondosha utitiri huu wa kodi. Naomba sana Mhe. Makamu wa Pili na viongozi wote wa serikali tumsaidieni Mhe. Rais kwenye hili kuhakikisha kwamba masuala haya ya kodi yanakwenda sawa na yanakaa sambamba, ili kuhakikisha wafanya biashara na wale watumiaji ambao kwamba ni wanunuzi wa kawaida tuweze kupata faida kwa kile tunachokinunua.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye sekta binafsi, sekta binafsi nazo zikishirikishwa katika masuala haya ya uwekezaji na masuala ya kiuchumi tutafikia mbali. Kwa mfano, Mhe. Mazurui alikuwa Rais wangu wa *Chamber of Commerce* nadhani labda atakuwa kanisahau Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima *Zanzibar Chamber of Commerce* ikishirikishwa ipasavyo katika masuala haya ya uwekezaji, nina imani tutafikia mbali Zanzibar na hawa watatusaidia au wataisaidia serikali kutafuta wawekezaji na kuweza kuwaweka hapa kuhakikisha kwamba tunapata viwanda na mambo mengine mbali mbali, lakini na sekta binafi nyengine ambazo kwamba zina nia njema ya kuweza kuisadia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Nabu Spika, nikitoka hapo niende kwenye ukurasa wa kumi na tisa suala la barabara hili limezungumzwa na wengi, Mhe. Rais amelitizama eneo la Pemba kama ni eneo la uwekezaji lakini huwezi kuwekeza kama hakuna umeme wa uhakika, huwezi kuwekeza kama hakuna miundombinu ya barabara Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Ndagoni unakujua ndiko ulikotoka umeme kutoka Tanga, ndiko kwenye kitovu cha umeme kwa Pemba lakini miundombinu ya barabara ya Ndagoni kilomita 8. 9 kutoka Wesha mpaka Mkumbuu sio zuri.

Kwa kweli, barabara ile Mhe. Naibu Spika ikinyesha mvua hata punda hafiki na kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu kanijaalia nimerudi tena kipindi chote cha miaka mitani nilikuwa nazungumza suala la barabara ya Ndagoni. Sasa kwa vile tunakwenda Pemba ni maeneo ya uwekezaji na kuekeza lazima tupate umeme na kule Ndagoni ndiko kwenye kitovu cha umeme ikianguka nguzo ya umeme kule Ndagoni kiza Pemba nzima hata viwanda vyenyewe hazitaweza kufanya kazi. Mhe. Naibu Spika, kuna siku ilikwenda trekta nayo pia ikakwama ile trekta ilikwenda kukwamua gari ambayo ni ya Shirika la Umeme ilikwama pia.

Kwa hiyo, naomba sana serikali kwenye suala hili tunapotaka kuekeza masuala ya viwanda, ili tuhakikishe kwamba tuna umeme wa uhakika na mambo mengine kuhakikisha kwamba miundombinu suala la barabara ili kuhakikisha kwamba miundombinu ya umeme iko salama kule Ndagoni, basi iweze kutengenezwa ile barabara kuona kwamba tunafikia pahali pazuri tujue kwamba wale wawekezaji nao wakitizama kwamba Ndagoni au maeneo ya umeme nayo yako salama waweze kuwekeza masuala ya viwanda na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, vile vile eneo lile la Ndagoni lina maeneo mengi ambayo watu wameshanunua tayari kwa kuekeza mahoteli. Mpaka leo hii wamesimamisha zile *beckon* tu hakuna yeyote aliyepeleka jiwe hata gari moja na Mhe. Nadir shahidi nilimpeleka kwenda kukagua maeneo yale mpaka leo hii kutokana na miundombunu ya barabara ilivyo. Kwa hiyo, naomba sana serikali ihakikishe kwamba barabara hii inafikiriwa na nina imani tu kwamba kwa kipindi hichi cha miaka mitano inayokuja na tunayokwenda nao na Rais wetu huyu ambaye tunae basi huenda barabara ile nayo ikaonekana.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye uwezeshaji wananchi kiuchumi. Mhe. Naibu Spika, suala la uwezeshaji wananchi ni suala mbalo kwamba nalo linahitaji kutizamwa kwa macho mawili Mhe. Rais amesema kwamba atatoa vitambulisho kwa wajasiriamali. Hili ni jambo jema na wajasiriamali wanamshukuru sana Mhe. Rais isipokuwa tu sasa wanasubiri vile vitambulisho, ili waweze kufanyakazi kama vile ambavyo Mhe. Rais kawaahidi.

Mhe. Naibu Spika, mjasiriamali wa kawaida analipia kodi au tozo ile anayotoa ya Halmashauri na sehemu nyengine kwa mwezi inafika shilingi elfu sitini hadi laki moja. Lakini kikiwekwa kitambulisho nina imani hata wakiambiwa watoe shilingi elfu hamsini kwa mwaka mzima anaweza kuitoa kuona kwamba mjasiriamali huyu na yeye anaweza kukua. Mhe. Naibu Spika, wajasiriamali wengi hawataki utajiri wanataka kile chakula chao cha siku moja na watoto.

Kwa hiyo, naomba sana serikali suala hili wale viongozi wote walioteuliwa na Mhe. Rais tuweze kumkubusha Mhe. Rais kwenye suala hili la wajasiriamali la vitambulisho, ili kuhakikisha

kwamba wajasiriamali nao wananufaika na masuala ya vitambulisho na biashara zao ziende kama vile walivyopanga.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye ajira kwa vijana. Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mhe. Rais na hata kama kuna kijana hatompongeza Mhe. Raisa basi itakuwa sijui anataka nini huyu. Mhe. Rais hapa amesema hapa kwamba atawapatia mitaji vijana maana Mhe. Naibu Spika, mara nyingi tunazungumza kwamba vijana wajitegemee tunasema vijana wajiajiri wenyewe.

Lakini Mhe. Rais katika kitabu chake hichi amezugumza jinsi gani atawapa taaluma vijana atawapa na mitaji hapo sasa ndio ukweli tutaona kwamba vijana wanataka kuwezeshwa na sietaka kufanya kazi ni hiari yake mwenyewe. Mhe. Naibu Spika, unapomuwezesha ukampa mtaji hapo sasa utamwambia kwamba jiajiri mwenyewe, lakini Mhe. Naibu Spika tukiimba nyimbo kijana jiajiri wewe umekaa kwenye kiti unazunguka hivyo utakuwa unamuoenea. Lakini serikali ya awamu ya nane imepanga hilo kutoa mikopo kwa vijana wetu kuhakikisha kwamba mitaji hii itawasaidia vijana wetu hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye suala la maji. Mhe. Nibu Spika, suala la maji nalo litizamwe vizuri...

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe unazo dakika mbili za kumalizia.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Mhe. Naibu Spika, hizo dakika mbili zinanitosha lakini Mheshimiwa ukumbe kwamba ukiombwa utoe kwa sababu uliomba wewe hapa na ukapewa zile dakika kwa hiyo na sisi tukubalie. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Mjumbe kwa mchango wako. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Panya Ali Abdalla baada ya hapo atachangia Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir ajitayarisha Mhe. Rukia Omar Ramadhan. Mhe. Panya Ali Abdalla karibu.

**Mhe. Panya Ali Abdallah:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukuwe fursa hii kumshuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana hapa. Lakini pia tuchukuwe fursa hii kumuomba Mwenyezi Mungu awajaalie mwenzetu wenye kupata mtihani wa maradhi awepe tahafif ili wapone haraka na waweze kushughulika na yao, lakini na Mwenyezi Mungu aliowatanguliza mbele ya haki tunamuomba awarehemu kwa rehema njema awasamehe makosa yao na kuwafutilia madhambi yao pamoja na kuwachanganya katika kundi lake la waja wema.

Mhe. Naibu Spika, napenda niungane na wenzangu wote ambao wameshiriki katika kuchangia hotuba ya Mhe. Rais na walianza kwa kumpongeza sana Mhe. Rais na mimi napenda niungane nao. Mhe. Rais ameweza kutuonesha muelekeo mwema kabisa yale aliyoyaahidi maana yake anaendelea katika utekelezaji wake. Kwa hiyo, tunachukuwa fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais Dr. Hussein Ali Hassan Mwinyi lakini pia tunachukuwa fursa hii kumpongeza sana kwa uteuzi wa kumteua Makamu wa Kwanza wa Rais lakini na kumteuwa kijana shupavu, hodari,

jasiri, Makamu wetu wa Pili wa Rais ametuonesha kabisa mapambano yake na yuko vizuri katika kusimamia shughuli zake za kazi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia nichukuwe fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe pamoja na Mhe. Spika pamoja na wenyeviti wetu ambao tumewachangua hivi karibuni tu. Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri uongozi mwema *Inn Shaa Allah* mtuongeze vizuri.

Mhe. Naibu Spika, napenda niungane na wenzangu katika kukichangia kitabu hichi, wenzangu wamesema mengi na ni mengi mazuri kwa sababu hichi kitabu kila unavyoendelea kukisoma basi kinaleta muonekanao mzuri zaidi maana yake hakiishi hamu.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze katika ukurasa wa 21 Mhe. Rais ameizungumzia habari ya kilimo na mimi kupitia habari ya kilimo na ambayo hii nilikuwa nikiichangia muda mwingi hapa Barazani basi napenda niendelee kusisitiza.

Kwanza nichukuwe fursa hii kuipongeza awamu ya saba ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuonesha dhamira ya dhati kabisa katika kilimo na alianza na kilimo hichi cha umwagiliaji na ndicho kilimo ambacho tunakitegemea kama kitafanyiwa kazi kitaweza kutuzalishia chakula vizuri.

Sasa nampongeza Mhe. Rais kwamba na yeye amelichukuwa na anasema itaendeleza mipango na mikakati ya awamu ya saba. Kwa hiyo, hili tunajua jambo hili litawezwa kuendelezwa vizuri na Mhe. Naibu Spika, kwa nini tunasema tushughulikie mipango ya kilimo, ili iweze kwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kilimo ndio uti wa mgongo wetu lazima sisi tunategemea hatuwezi kuja hapa Barazani kama hatutajua mambo ya kula kula kule nyumbani yamekaa vizuri. Kwa hiyo, kuisimamia sekta hii ikaweza kufanya kazu zake vizuri na ikaweza kuleta uzalishaji mzuri tunaamini tunaweza kwenda vizuri.

Kwa kweli, nalizungumzia sana hii kwa sababu bado hatujawa na mpango wa kuweza kuwa na chakula cha kujiwekea akiba ya chakula na hili na jambo muhimu katika nchi lazima muweze kuishi kwa kuona chakula mna uhakika wa kukipata. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, mpango huu unaotaka kwenda kufanya *irrigation* naamini utaweza kutupeleka pazuri katika uzalishaji wa chakula.

Mhe. Naibu Spika, lakini pili niendelee kuishauri serikali katika kipindi cha nyuma tulikuwa na mpango au tulikuwa na utaratibu wa kugawa mbegu ilikuwa tukishamaliza mavuo ya mpunga serikali ilikuwa inatupa mbegu za kunde, mbegu za mahindi, ili tuweze kuzidisha uzalishaji. Kwa hiyo, bado naiomba au naishauri serikali mpango huu ukiendelea maana yake tunaendelea kuzidisha uzalishaji.

Kwa hiyo, hata pia ilikuwa na mpango wakuangalia ule wakati wa kiangazi tulikuwa tukuipatiwa mbegu ambazo zilikuwa na uwezo wa kustahamili ukame na tulikuwa tunalima, kwa ajili ya kupata manufaa. Kwa hiyo, bado tunaishauri serikali iendelee kutupatia ili tuweze na sisi

kujitegemea angalau kwa asilimia ya nusu ya chakula tunaweza kukilima sisi wenyewe hapa nchini petu.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 32 ambapo Mhe. Rais alizitaja Idara Maalum na mimi kwanza napenda nimpongeze Mhe. Rais lakini napenda pia nizipongeze Idara hizi Maalum kwa kazi kubwa na nzuri ambazo waweze kuzifanya kuweza kuisimamia nchi hii kubakia katika amani na utalivu. Jambo hili tunapongeza sana vikosi vyetu na kwa kuwa Mhe. Rais ameligusia basi naamini itakapokaa hali yetu katika hali nzuri basi Mheshimiwa ataweza kuwakumbuka hawa kwa kuwaongezea mishahara kwani waswahili wanasema "Mcheza kwao hutumzwa". *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa naamini lakini pia vikosi vyetu hivi vinavyoshiriki katika kilimo kuvipatia nyenzo za kisasa vikaweza kulima katika hatua nzuri ya kisasa, basi pia tunaweza kuongeza uzalishaji wa chakula katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nilitaka niende katika ukurasas wa 33 ambapo kunasema kuna "ustawi wa wazee wanawake pamoja na watoto".

Nampongeza Mhe. Rais kwa juhudi zake zote ambazo ameweza kuyashughulikia au kuyakushanya makundi mbali mbali ambayo ataka kuyaweka katika usaidizi. Hapa lipo katika wanawake na watoto, kwanza wazee nilikuwa naiomba serikaili iangalie wazee wetu katika mambo yale ya kijamii basi tuweze kuwapa vitambulisho maalum, ili wazee wale wanapoonekana katika huduma basi pia waweze kupatiwa fursa kama hospitali basi waweze kuhudumiwa kwa haraka wazee wetu, kwa sababu tunajua sisi bila ya wazee tusingeweza kufika hapa. Lakini kwa upande wa wanawake na watoto Mhe. Rais ameazimia kusaidia wanawake wajanae tunampongeza juu ya hilo.

Lakini napenda nitoe ushauri serikali juu ya hili tutoe elimu ya kutosha kuna wanawake watakuja kuona kuwa tayari serikali inataka kuwasaidia wakenda wakadai talaka kwa makusudi majumbani, wameshajua wao watasaidiwa basi wakaona ni kuzitupa familia zao na kwamba Mhe. Rais atatusaidia. Kwa hivyo, hapa elimu itolewe ili ile talaka iwe imetokea kwa bahati mbaya lakini ndipo mtu aweze kusaidiwa, lakini tusifanye juhudi ya kwenda kuzidai talaka tupate tushughulikiwe na serikali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lakini niende ukurasa wa 34 Mhe. Rais amelitaja kundi la watu wenye ulemavu. Kwa kweli, napenda nimpongeze Mhe. Rais kwa hili, kwa sababu Mhe. Rais wetu kama tulivyoelewa alifanya kampeni za kisayansi mwaka huu katika nchi yetu ameweza kuyagusa makundi mbali mbali kwa hiyo nao wamehamasika vizuri.

Sasa, katika kundi hili la watu wenye ulemavu nilikuwa naomba na kwa hapa Mhe. Rais amezungumzia ilivyo kama ilani kwamba ilani imewataja sana watu wenye ulemavu na kuweza kuopatia hati mbali mbali. Lakini serikali imesema itaweka kipaumbele, hivyo naomba sana serikali juu ya suala hili la watu wenye ulemavu iweze kweli kuweka kipaumbele katika majengo ambayo wenzetu wanafika pale yale majengo yawe rafiki na wao, ili waweze kupatiwa huduma zote wanazozihitaji lakini katika elimu Mhe. Naibu Spika, naiomba serikali kweli iwekeze katika watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, watu wenye ulemavu wanao uwezo mkubwa, kwa sababu Mwenyezi Mungu hakunyimi yote wana uwezo mkubwa wenzetu hawa, lakini pia wanazo changamoto kubwa. Changamoto waliyonayo watu wenye ulemavu ni kukosa vifaa vya kufundishiwa lakini pia kukosa walimu wenye taaluma hii ya kuwafunza wao. Kwa sababu tulienda kuwatembelea siku moja yenye watu wenye ulemavu tutakuta mtoto anasoma kidato cha nne lakini anasomeshwa na mwalimu wa skuli ya msingi, hili ni tatizo. Kutokana na hali hiyo, tunaomba sana ili hawa tuende nao sambamba basi ni kuweza kuwasaidia katika kuwapatia huduma zao mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika ukurasa huu huu wa 34 kuna maeneo mengine mtambuka ambayo yamegusa sanaa, burudani na michezo, wenzangu wengi wamegusia suala hili na mimi napenda nigusie suala hili.

Mhe. Naibu Spika, tunao vijana wengi wanao shughulikia sanaa, burudani na michezo. Lakini tunataka kuishauri serikali basi wenzetu wako katika sanaa basi waweze ile sanaa yao kuiweka katika utamaduni wa nchi yetu, kwa sababu kama tunavyoelewa utamaduni ni lulu katika nchi yetu, leo tunapotoka katika utamaduni wetu na tukaweza kufanya tu sanaa zetu za kuigiza katika nchi za wenzetu, kwa hiyo tunavunja ule utamaduni wa nchi yetu.

Lakini kupitia hapa naomba nimpongezee sana Mkuu wa Wilaya ya Mjini Mhe. Rashid Simai Msaraka, ambaye nilimuona ameanza kurejesha utamaduni wetu wa kushughulikia vijana lazima waendane na muelekeo mzuri. Wananchi wa Zanzibar ni wazuri wanao utamduni mzuri kwa hiyo ni lazima turudi katika tamaduni zetu ambazo tumezirithi katika wazazi wetu. *(Makofi)*

Kwa mfano, leo vijana unawakuta wanafuga manywele unamkuta mtu hata ukikutana nae huwezi kuamini kama ni mtu ana akili yake timamu akikuomba *lift* unaseme mmh! Huyu ana akili kweli si mwendawazimu, kwa sababu ya kuona vile alivyojiweka. Kwa hiyo, namshukuru na nmpongeza sana amenza vizuri na aendelee tuko pamoja na yeye, lakini hata mavazi katika nchi yetu hii, basi tuangalie tuendelee katika kuvaa katika mavazi yanayolingana na utamaduni wetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu ningependa kwa sababu Mhe. Rais ameelezea pia katika mapato au ukusanyaji wa kodi. Kwanza nampongeza sana Mhe. Rais kwa kuweze kufanikiwa kuyasimamia mapato yakaweze kupatikana bilioni mbili ambazo mwaka mzima kukuliwa kunakusanywa bilioni nne, lakini baada ya mwezi mmoja ameweza kukusanya bilioni mbili katika bandari hili ni jambo la kuwekwa kumbukumbu vizuri, kwa sababu ameweza kuyasimamia mapato na bila ya mapato maana yake hakuna hayo matumizi ambayo tunataka kuyatumia.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo niseme bado katika eneo la mapato bado...

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, tupunguze minong'ono tusikilize hoja.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Mhe. Rais aongeze juhudi zake bado mapato ya serikali bado yanavuja mengi hatuyapati kama inavyotakiwa, ukiangalia katika maduka risiti zinaendelea kuwa hazitolewi ukiendelea katika masheli risiti zinazotolewa labda kwa magari ya serikali,

lakini bado tunahitaji katika eneo hili liweze kukusanya mapato, ili serikali iweze kupata matumizi katika mipango yake mbali mbali ambayo imejipangia.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wenzangu wengi wamechangia na michango ni mizuri zaidi kwa hiyo naomba na mimi kwa kumalizia kuna wenzangu wengi hapa wapongeza, lakini na mimi naomba nichukuwe fursa hii kumpongeza sana mume wangu Bwana Pembe Juma Khamis mwanasiasa mkongwe lakini ni mwanasiasa mzalendo. Kwa hiyo, nachukuwa fusa hii kupongeza na kumtakia kila la kheri mwenyezi Mungu amjalie kheri ampe afya njema azidi kuendelea kunisaidia katika majukumu yangu haya. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema haya naomba niunge mkono hotuba hii ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja pia tukiendelea kumuombe dua Mhe. Rais wetu aendelee na kazi hii vizuri na sisi tunam-*support* kwa asilimia zote tutafanya naye kazi pamoja ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Panya Ali Abdalla kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe, inaruhusiwa unapongeza mume, mama, mke na mwengine ambaye unaona kwamba anastahiki kupongezwa mpongeze.

Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea naomba niseme kwamba bado naendelea kupokea majina ya wachangiaji. Kwa hiyo, yeyote yule ambaye anataka kuchangia nafasi ipo, sasa nimpe nafasi Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir na baada ya hapo atafuata Mhe. Rukia Omar Ramadhan.

**Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir:** Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi hii kuendelea kuchangia hotuba ya Mhe. Rais ambayo ni *Golden Speech*.

Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo uhai na uzima kushiriki na mimi hapa.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mhe. Rais wa awamu hii ya nane katika siku zake mia moja na kufanya vyema na kuwakosha Wazanzibar namna alivyopandisha uchumi wetu wa Zanzibar katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, lakini kwa upokee niwashukuru Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuniona ninafaa na kuja kuwakailisha hapa, lakini siwasahau walioniibua Wilaya ya Mjini Umoja wa Vijana niwashukuru kwa dhati. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika ukurasa wa 10 katika dhamira nzima ya uvuvi nimpongeze Mhe. Rais kwa kuendelea kuthamini uvuvi na kwenda kuandalia uchumi wake mahsusi na kuandaa ama kuja kununua vyombo vya kisasa ambavyo vinaendana na uvuvi wa bahari kuu.

Hivyo naiomba sana serikali kutokana na vifaa hivyo iendane sambamba na ujenzi bandari kuu, ili kuongeza ufanisi na ajira kwa vijana kwa zile meli ambazo zinakuja kufanya *discharging,* tuje kujua kiasi ambacho kilichovuliwa pamoja na kupata mapato. Kwa kweli, hapo itaongeza ajira kwa vijana kupitia Wizara hii ya Uchumi wa Buluu kuandaa mikakati madhubuti ya kuongeza

mafunzo katika vituo vya amali, skuli na vyuo vikuu kwa kuwafundisha, ili vijana tuje ku-*compete* katika soko hili la uchumi wa buluu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, na mimi niende katika ajira kwa vijana, nimpongeze sana Mhe. Rais kwa hotuba yake imeeleza mwelekeo wa Mapinduzi ya uchumi, lakini pia imekwenda kueleza namna gani vijana tunakwenda kuajiriwa.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kwenda kuitekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi zile ajira 300,000 za vijana. Mimi nadhani ni jambo jema na Mwenyezi Mungu amjaalie aweze kutekeleza hilo.

Vile vile nampongeze Mhe. Rais wa Awamu ya Saba, Dkt. Ali Mohamed Shein alituandalia mabaraza ya vijana na yalituwezesha katika miradi midogo midogo kupitia Shehia na Wilaya. Lakini namuomba sana Mhe. Rais kupitia waziri wake wa vijana kuendelea kuyaenzi na kuyatunza mabaraza ya vijana kwa kuyawezesha na kuipatia mikopo, ili tuendelee kutunza na kuendelea kuibua miradi mikubwa zaidi kupitia haya Mabaraza ya Vijana, Shehia na Wilaya katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niende moja kwa moja kwenye amani na utulivu, ukurasa wa 35. Nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi ameirithi vyema amani hii ya Zanzibar na utulivu kwa Dkt. Ali Mohamed Shein ndipo alipoirithi. Lakini na yeye anaendelea kuitunza na sisi vijana tunamwambia kama alivyohusia katika hotuba yake jukumu la amani hii, maana yake ni kila mmoja wetu kuilinda na kuidumisha sio vyombo vya ulinzi na usalama tu. Mhe. Naibu Spika, katika Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa sisi vijana tutakuwa walinzi watiifu, walinzi imara na tutakuwa macho muda wote kuiendeleza amani ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 28 uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Mhe. Naibu Spika, haya yalianza zamani kwenye Serikali ya Awamu ya Saba kwa kuandaa vitu tofauti tofauti, lakini tumshukuru maana yake pale alipoachiwa na yeye anapaendeleza Mhe. Rais wetu vijana anaendelea kuwawezesha lakini kwenye wananchi hao asilimia kubwa ni vijana na wajasiriamali wengi ni vijana. Kwa hiyo, tumshukuru lakini kutuongezea ile asilimia kidogo ya mikopo ili tuweze kujiajiri zaidi. Mhe. Naibu Spika, kubwa zaidi pale alipotufurahisha na nimpongeze na Mwenyezi Mungu amjaalie afanye haraka kuondosha kodi kama utitiri na kuja na mfumo mmoja tu kwani vijana itatusaidia mitaji yetu kukuwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini ku pitia Wizara ya Biashara tuseme kuna baba zetu, vijana wenzetu katika hizi biashara za boflo, basi na wao waandaliwe soko zuri na madhubuti kuona namna gani wanakwenda kuuza biashara hii katika sehemu nzuri, mazingira mazuri... *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Samahani Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe, naomba niseme hivi tunapogonga meza tunaharibu mfumo wa vipaza sauti na hilo nafikiri kwa wale ambao ni wajumbe wa zamani wanalifahamu hilo. Ningeomba sana wakati tunagonga meza tugonge kwa ustaarabu wa hali ya juu, tunafahamu kwamba tunapata mshawasha mkubwa katika maneno ambayo yanazungumzwa, lakini ifike pahala tuheshimu na mifumo yetu ambayo inatusaidia katika kufanya shughuli zetu. Ni hilo tu waheshimiwa, sijui nimeeleweka.

**Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir:** Mhe. Naibu Spika, ahsante lakini niwaambie tu biashara ya boflo ipo zamani wengine imetulea na wazee wetu wameianza zamani ni vyema kuiandalia utaratibu maalum ikawa *unique* maana yake inapatikana Zanzibar tu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 34 sanaa, burudani na michezo. Nimpongeze sana Mhe. Rais wa Awamu ya Nane kwa kuendelea kuyaenzi pamoja na kulea matamasha ya Sauti za Busara pamoja na *ZIFF*. Lakini kilio chetu kama vijana tuna wasanii ambao *Zanzibar Flava Units* ambao hawa wameji-*organize* lakini kuna vikundi asilia tamasha la maigizo kupewa nafasi zaidi ndani ya Zanzibar, ili na wao wajiongeze uwezo ama kumfikia Diamond pamoja na Ali Kiba, hawa nao wanahitaji matamasha, hawa nao wanahitaji vifaa vya kisasa. Dkt. Ali Mohamed Shein amewaandalia *studio* pale Rahaleo Studio Zanzibar, basi tunaomba na yeye atujali zaidi kama vijana wake ambavyo anavyotujali tunajua Rais wetu ana mapenzi na sisi, ana huruma na sisi nadhani vijana wake ndio walinzi wa nchi hii ya Zanzibar katika visiwa vya Unguja na Pemba. Tunaomba matamasha ambayo yataandaliwa na Wizara ya Vijana kutangaza wasanii wetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja ya Mhe. Rais wa Zanzibar, lakini zaidi niishukuru familia yangu hasa mama yangu kwa kuniunga mkono na mimi kutekeleza majukumu haya, na niwashukuru sana vijana wenzangu ndani ya Zanzibar nzima kwa kuniunga mkono na mimi nawaomba waendelee kuniunga mkono niweze kuwatetea ndani ya Baraza hili la kutunga sheria. Nashukuru Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir mchangiaji anayefuata ni Mhe. Rukia Omar Ramadhan na ajitayarishe Mhe. Anna Athanas Paul. Waheshimiwa manaochangia msiwe na wasi wasi sana na muda tulionao tuna muda wa kutosha kabisa. Kwa hiyo, unaweza ukajimwaga vizuri kama una la kuzungumza.

**Mhe. Rukia Omar Ramadhan:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ulionipa na mimi niungane na wenzangu kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa katika uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi, tarehe 11 Novemba, 2020.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na afya njema na kuweza kukutana katika kutekeleza wajibu wetu. Nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa hotuba yake iliyokidhi mahitaji ya wananchi wa Zanzibar wakiwemo wa Jimbo la Amani. Niwashukuru kwa upekee na mapenzi makubwa wana Jimbo la Amani kwa kunichagua kwa kura nyingi nije kwenye Baraza lako tukufu kuwakilisha na kuishauri serikali. Nawaomba waendelee kunipa mashirikano, ili tuweze kuitekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi kufikia yale mahitaji yao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nisiwe mchoyo wa fadhila napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru kwa dhati ya moyo wangu viongozi wa Jumuiya ya Wanawake hasa Mkoa wa Mjini kwa mashirikiano yao makubwa waliyonipa wakati wa kampeni. Wanawake hawa walinitia moyo na kuniongeza ujasiri wakati nikiwa naomba kura ndani ya Jimbo la Amani. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kuendelea kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika hatua ya kuimarisha ubora wa elimu Zanzibar katika ukurasa wa 25 ambapo ameenda kuigusa haki ya msingi kwa kila mwananchi. Mhe. Naibu Spika, katika hatua njema ya Mhe. Rais wa Zanzibar ya kulishughulikia suala hili la elimu mara tu baada ya kulihutubia Baraza hili amefanya mkutano mkubwa wa kukutana na wadau wa elimu ambapo sehemu kubwa walitoa changamoto na mafanikio. Changamoto hizo ambazo kwa pamoja tukishirikiana tutaweza kuisogeza mbele nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, moja kati ya changamoto za elimu ipo katika sera uandaaji wa walimu na usogezaji wa miundombinu pamoja na vifaa. Naendelea kuiomba serikali kuangalia maeneo hayo matatu.

Mhe. Naibu Spika, tufanye mapitio ya sera ya elimu ili yale maeneo yote yaliyokuwa na changamoto kuyapatia ufumbuzi wake kwa haraka. Lakini pia kukirejesha Chuo cha Ualimu Nkurumah, ili kuweza kuwaandaa walimu bora kama ilivyokuwa hapo awali, ambapo tulipata walimu wenye *ethics, content* na *methodology*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naendelea kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika hotuba yake amegusia suala zima la uboreshwaji wa maslahi ya walimu. Naiomba wizara husika isichelewe kuwapatia uimarishaji huu wa maslahi yao walimu hawa ili lengo lile la Mhe. Rais lifikiwe la kuwapa *motion* walimu wetu.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza Mhe. Rais kuona umuhimu wa kufanyiwa ukarabati skuli za zamani, kiukweli wananchi wa Jimbo la Amani wamefarijika sana kuona nalo limepewa umuhimu katika hotuba ama Serikali ya Awamuu hii ya Nane. Namuomba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wakati watakapofanya tathmini ya skuli zenye mahitaji ya ukarabati atuone na sisi Jimbo la Amani tuna skuli zetu nne za msingi. Skuli ya Kilimahewa "A", Kilimahewa "B", Kwamtipura na Nyerere zinahitaji ukarabati mkubwa, ili ziendane na hadhi ambayo maeneo zilipo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kwenda eneo jengine la maji safi na salama katika ukurasa wa 27. Naendelea kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuligusa eneo hili la maji safi na salama katika hotuba yake.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya maji kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji awe na ajenda maalum ya kufanya mapitio ya miundombinu ya maji katika maeneo tofauti yenye changamoto za maji. Kwa mfano, katika Shehia ya Kwawazee, Kilimahewa Juu, Kilimahewa Bondeni na Amani katika Jimbo la Amani, kwa sababu ya uchakavu wa miundombinu yake. Namuomba Mhe. Waziri kwa sababu wananchi walionichagua na wananisikiliza nakuomba mheshimiwa na Mamlaka ya Maji tufanye ziara ya haraka iwezekanavyo ili tuweze kutatua changamoto hii inayowakabili wananchi wa Jimbo la Amani.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende ukurasa wa 19 unaozungumzia barabara. Naomba niendelee kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa azma yake ya kuzitengeneza barabara zilizoainishwa katika ukurasa huu ambao zimeenda sambamba na ahadi zilizotolewa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020-2025.

Katika eneo hili la ujenzi wa barabara namuomba Mhe. Waziri na Wakala wa Utunzaji na Uendelezaji wa Barabara na Mhe. Waziri wa TAMISEMI kuzishughulikia barabara za ndani zilizoekewa ahadi na viongozi waliopita na ni ahadi za muda mrefu, kuzifanyia upembuzi yakinifu na kuzijenga ili wananchi waendelee kujenga imani ya serikali ya Chama Cha Mapnduzi waliokichagua kwa kura nyingi. Mfano wa barabara hizo katika Jimbo la Amani ni barabara ya Ziwatuwe mpaka Mboriborini na kutoka Kwawazee mpaka Kwanajim naendelea kutetea eneo la jimbo langu na eneo la Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango wa Jimbo la Magomeni naamini matengenezo haya yatafanywa kwa uharaka na yatapatikana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie katika eneo la ustawi wa wazee wanawake na watoto ukurasa wa 33. Naomba kupongeza hotuba ya Mhe. Rais kugusia eneo hili muhimu la wazee, wanawake na watoto katika maelezo ya eneo hili imegusa kuendeleza ustawi wa wazee, ustawi wa wajane na ustawi wa watoto. Naomba kwa sababu ya muda kumalizia kwa kuzungumzia suala la ustawi wa watoto ambao wamekumbwa na kadhia kubwa ya udhalilishaji.

Mhe. Naibu Spika, katika eneo hili naomba kumpongeza Mhe. Rais kwa kuanzisha Mahakama ya Udhalilishaji. Nawaomba viongozi wenzangu na wananchi kuunga mkono jitihada za Mhe. Rais za kupambana na udhalilishaji kwa gharama yoyote, ili kuweza kuondosha ubaya huu wanaofanyiwa watoto wetu. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Amani naiunga mkono hotuba hii asilimia moja. Ahsante sana na nakushukuru Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Rukia Omar Ramadhan, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Anna Athanas Paul ajitayarishe Mhe. Zaina Abdalla Salum.

**Mhe. Anna Athanas Paul:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa fursa hii ya kutaka na mimi nichangie ambayo nimeyaona ndani ya hotuba hii, hotuba ya dhahabu ya Mhe. Rais. Napenda kuompongeza Mhe. Rais kwa kuteuliwa kwa kishindo kwa ushindi mkubwa ambao haujawahi kutokea Zanzibar tokea vyama vingi vianzishwe. Pia nipende kumshukuru kwa kunichagua mimi kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, nataka kumwambia kwamba *I'm very greatfull* kwa hii nafasi ambayo amenipa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia nikupongeze wewe na Mhe. Spika kwa kuchaguliwa pia kwa kura nyingi, lakini pia nimpongeze Mhe. Makamu na Mhe. Makamu wa Pili kwa kuteuliwa kuweza kushika nafasi hizo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda kwenye kilimo napenda kumpongeza Mhe. Rais kwa kutilia mkazo suala hili la kilimo, hasa kilimo cha umwagiliaji maji. Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha jambo hili linafanikiwa tumeona miradi sasa imeanzishwa na inaendelea. Miradi mingi katika mabonde mbali mbali ya mpunga inaendelea na inafanya vizuri mpaka sasa. Lakini tumuombe Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo aisimamie miradi hii ambayo sasa inaendelea ili iweze kumalizika kwa wakati. Tokea ilipoanza sasa imeongezewa muda, huu muda uliongezwa basi miradi hii iwe imeshakamilika na sasa tuweze kuzalisha na tupate kuwa na uhakika wa chakula, si uhakika tu na pia tuwe na *stock* ambayo itabakia huko kwamba lolote litatokea iwe tuna chakula chetu cha kutosha cha kuweza kulisha Zanzibar nzima.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kuzungumzia kilimo cha mboga mboga ambapo mazao mengine Mhe. Rais ameyatilia mkazo na zaidi ametilia mkazo vijana na ametaka vijana wajengewe uwezo wa kupata vitalu na kuweza kuzalisha mboga mboga kwa wingi na kwa uhakika, kwa sababu kuzalisha ndani ya vitalu nyumba kunampa uhakika mkulima kwamba ataweza kulima kwa mwaka mzima bila ya kubughudhiwa na wadudu, bila ya kubughudhiwa na mvua muda wowote ataweza kulima.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kipindi cha mvua huwezi kulima mboga mboga, lakini kama tutakuwa na hizi nyumba vitalu mwaka mzima wakulima wataweza kulima mboga mboga na kuweza kuilisha nchi yetu bila ya kuwa na haja ya kuagiza mboga mboga hizo kutoka nje.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Kilimo kuweza kufufua kuna kitengo cha *Agro Process* cha usindikaji. Kitengo kile kiwepo sasa kwa sababu hizi mboga mboga ni *perishable goods*, sasa zikishakuwa nyingi ni bidhaa ambazo zinaharibika haraka, zinaweza zikaharibika huko sokoni na wakulima wetu vijana hawa wakapata hasara.

Sasa hii *food processing*, hii *department* iwepo ili mazao haya yaweze kusindikwa na kuyapatia thamani zaidi na hiyo bei yake itaongezeka na bei ikiongezeka wakulima watapata faida zaidi. Kwa kweli, kitengo hiki kipo kimejengwa pale Kizimbani nakijua, lakini sasa hakifanyi kazi kwa muda mrefu sijajua tatizo lake liko wapi, kifufuliwe basi na kiweze kuonesha faida yake.

Mhe. Naibu Spika, bila shaka jambo hili lihusishwe na kitengo cha *SMIDA* kwa sababu *SMIDA* ni kitengo ambacho kinashughulikia ukuzaji wa viwanda vidogo vidogo. Kwa hivyo, kishirikiane basi na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, ili kuwakuza hawa vijana wetu ambao watajihusisha katika kilimo cha matunda na mboga mboga waweze kufanya huu usindikaji na kuwa na viwanda vyao. Mwaka mzima tutaweza kula embe, mananasi pamoja na matunda mengine yaliyosindikwa, hatuna haja ya kukaa tukasema sasa embe hazipatikani, tutakuwa tuna embe za kutosha lakini zilizosindikwa na hii itatupatia hata soko la watalii kwa sababu watalii wanapenda sana hizo bidhaa na wameshazoea kula hivyo vitu vya kusindikwa.

Pia napenda kuzungumzia ufugaji. Mhe. Rais amegusia ufugaji na kusema kwamba sasa tunakwenda kwenye ufugaji wa kisasa zaidi. Sasa ufugaji wa kisasa zaidi unahitaji ng'ombe wa kisasa kwa sababu tunahitaji maziwa mengi, ng'ombe wa kizamani hawatoi lita nyingi za maziwa ila ng'ombe wa kisasa wanatoa lita nyingi za maziwa. Kwa hivyo, ufugaji wa kisasa unaelekea huko kwenye ng'ombe wa kisasa.

Mhe. Naibu Spika, ng'ombe wa kisasa kwa hapa kwetu hatuwezi kuwapata lakini tuna kitengo chetu cha *AI (Artificial Insemination*). Kitengo kile pana mtambo mkubwa wa kuzalisha gesi, nimuombe tu Mhe. Waziri wa Kilimo au aangalie kwa makini mtambo ule sasa aufufue, ili mbegu, madume yapo yanayozalisha mbegu pale, lakini mbegu hizo haziwezi kuhifadhiwa maana ile *liquid nitrogen* ambayo inazalishwa na mtambo ndio haipo mana mtambo umelala. Sasa kitengo cha *AI* kina haja ya kuboreshwa upya na kufufuliwa, ili tunapokwenda kwenye ufugaji wa kisasa tuwe na ng'ombe bora, tuwe na ng'ombe ambao watatupa lita nyingi za maziwa.

Sasa sijui Mhe. Waziri kitengo hiki kwa nini kinakufa siku zote na kuwaletea bughudha wafugaji wetu. Mbegu zinachukuliwa kutoka Arusha au sehemu nyengine Bara zinaletwa Zanzibar mfugaji anapelekewa anapandishiwa ng’ombe wake, lakini mbegu zile ambazo zinapandishiwa ng’ombe hashiki mimba kwa sababu mbegu ile imetoka Arusha mpaka imefika Zanzibar na ile inahifadhiwa kwenye hiyo *liquid nitrogen*.

*Liquid Nitrogen* mpaka ifike hapa inakuwa imeshapoteza ubora wake na hakuna tena ile gesi ya kuipa angalau ikawa na uhai, ikifika kwa mwananchi anapandishiwa na kupandishiwa ni shilingi 30,000 mara moja, mfugaji anapandishiwa zaidi ya mara tatu ng’ombe hajashika mimba. Kwa hivyo, hii inawapa hasara wafugaji wetu na kuwazidishia umasikini na sasa inapelekea kuwapandishia kwenye ng’ombe hawa wa kienyeji tu na kupunguza uzalishaji wa maziwa. *(Makofi)*

Jana msemaji mmoja alisema kwamba Said Salim Bakhresa anatumia maziwa ya unga kuzalisha yale maziwa, kwa sababu sasa hapa wafugaji wetu hawana maziwa ya kumpa yeye akaweza kuzalisha bidhaa hii ya maziwa ya maboksi.

Mhe. Naibu Spika, lakini gesi hii pia tungeweza kuizalisha na tukawauzia nchi nyengine, kwa sababu mtambo wetu ni mkubwa sana ungeweza kusambaza Tanzania nzima, Bara wangeweza kuja kununua kwetu kwa sababu wao hawana mtambo mkubwa kama huu tulionao sisi tungeweza pia kufanya biashara hiyo.

Vile vile, nizungumzie utunzani wa maziwa, usalama na ubora wa maziwa. Jana tumezungumzia kwamba watalii wanakataa bidhaa zetu hawazikubali lakini Wazungu wana *standard* zao, huwezi tu ukampelekea maziwa kwenye dumu la lita 20 halafu yeye akachukua, hawezi kuchukua maziwa kama hayo ataagiza *South Africa* ambako maziwa yamehifadhiwa. Kwanza yamepimwa kwa sababu yeye anaangalia yapo bora kwa kumpa mlaji, lakini cha pili yamehifadhiwa kwenye vyombo maalum vya kuhifadhi maziwa. Kwa kweli, mpaka sasa wafugaji wetu wanahifadhi maziwa yao kwenye madumu na chupa za *drop*, ambapo hali hiyo inashusha ubora wa maziwa. Kwa hivyo, hili liangaliwe tuwe tuna vituo vyetu vya upimaji wa maziwa.

Mhe. Naibu Spika, zamani nakumbuka mimi nilipokuwa mdogo kulikuwa kuna mideli ya *aluminium* makubwa kama ndoo pamoja na *packets* ndogo ndogo za maziwa yanahifadhiwa humo, tulikuwa tunakunywa maziwa humo hatutumii hizi chupa za *drop*. Sasa Mzungu ukimwambia anunue maziwa kwenye chupa tutapiga kelele sana lakini yeye hawezi kufanya hicho kitu. Kwa hivyo, ili ajira ziwe nyingi, vijana wetu wawe na ajira za uhakika na za staha basi tuboreshe hivi vitu tuweke hivi vitengo, ili vijana waweze kuvitumia na kuweza kujipatia tija katika uzalishaji wao.

Vile vile tuendeleze mashamba yetu ya malisho kwa sababu Zanzibar sasa mashamba mengi watu wamejenga katika mashamba hayo na zamani tulikuwa na *pasture* zetu tunapanda majani na ng’ombe wanakuwa na uhakika wa chakula. Kwa sababu uhakika wa chakula tusijiangalie sisi tu na wanyama nao wanatakiwa waangaliwe kwenye uhakika wao wa chakula ili waweze kutupa tija. Ng’ombe usipomlisha hawezi kukupa maziwa, ng’ombe unapomlisha ndivyo anavyotoa maziwa zaidi akiwa na njaa hawezi utamkamua povu tu hawezi kutoa maziwa.

Kwa hivyo, haya mashamba, hizi *pasture* zilizokuwepo Kizimbani zifufuliwe tuna sehemu kule za kupanda hayo majani ya ng'ombe zifufuliwe basi ili yakaushwe majani wakulima wanakwenda pale wananunua kwa bei nafuu wanaweza kuwalisha ng'ombe wao na hapo uzalishaji wa maziwa utapanda.

Mhe. Naibu Spika, kuna hizi *hub integration* za kila wilaya ambapo wakulima sasa baada ya kuzalisha maana wakisha kuzalisha sasa tumewawezesha wamezalisha watapeleka wapi maziwa yao, tuwe na hizo *hub integration* ambazo wakulima watapeleka huko na zitahifadhiwa hapo kutakuwa kuna wataalamu, shughuli zao zote zile wafugaji wa wilaya ile, vikundi vile vitakuwa vinafika hapo vinapatiwa hata taaluma, lakini maziwa yao wanapeleka hapo wanauziwa. Kwa hivyo, huyo mnunuaji mkubwa ambaye ana kiwanda sasa yeye ndio anakuja pale haendi kumpitia mkulima mmoja mmoja akaanza kununua, hiyo kwake itakuwa inampa ugumu. Lakini ana kituo kimoja anakwenda hapa anajua nikienda Wilaya ya Kati nakwenda sehemu fulani, nikienda Wilaya ya Kusini nakwenda sehemu fulani hivyo tu. Hizo *hub integration* ziboreshwe ziweze kutumiwa na hao wafugaji wetu.

Pia, napenda kuzungumzia wafugaji wa kuku. Vijana wetu wengi walikuwa wamejikita katika kufuga kuku hapa Zanzibar, lakini sasa ufugaji huu vijana wengi wamerudi nyuma kwa sababu kuna kuku wa peduu wanaingizwa kwa wingi na sasa mabanda ya vijana yamekuwa matupu wanakaa panya tu humo ndani, hamna kuku kwa sababu hawawezi kushindana na peduu. Peduu anauzwa shilingi 4,000 yeye kuku mpaka amfuge, amlishe, akue shilingi 6,000 au 7,000. Sasa hali yenyewe ya kimaisha ndio hii uchumi wa katikati hapa tupo mtu atakwenda kwenye shilingi 4,000 ataacha shilingi 7,000. Wapo ambao wataweza kidogo maisha yao yapo juu, lakini hawa wengi ambao maisha yao yako katikati wao wata-*opt* huko kwenye kuku wa peduu.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia tuombe haya machinjio, naona katika lengo kipaumbele kutakuwa kuna machinjio yatajengwa sasa sijajua machinjio hayo ni ya ng'ombe au kuku. Machinjio ya kuku bado Zanzibar hayajakuwepo ya kisasa, tuwe na machinjio ya kisasa kuku waweze kufanyiwa *packaging* wakishafanyiwa ukiwapeleka sokoni basi wanauzika mara moja, lakini kuku tu kachinjwa ovyo ovyo kapelekwa huko yaani hujui vile viwango vyake vikoje, hawana *label* kama wamepitia watu wa vyakula hawezi mtalii kumnunua kuku wa aina hiyo atanunua tu peduu wake ambae amepekiwa vizuri wametoka Brazil atalisha humo hotelini mwake.

Sasa vijana wetu wanakosa ajira na Mhe. Rais lengo lake ajira laki tatu ajira hizo zitatoka humo kwenye ufugaji, ukiachia gesi na mafuta hizi nyengine ndio zina watu wengi zaidi kuliko hizo gesi na mafuta tunavyofikiria. Kwa kweli, kwenye ufugaji wa kuku, ng'ombe pamoja na kilimo cha umwagiliaji maji.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nizungumzie ufugaji wa nyuki. Nyuki ni ufugaji mzuri sana kwa sababu hauna *stress* ufugaji wake, ukiweka mzinga wako hapo unasubiri kuvuna asali yako. Sasa naomba ufugaji huu wa nyuki nao utiliwe mkazo kwa sababu zao la asali lina bei kubwa zaidi hapa Tanzania, lakini nje ya Tanzania bado asali inapendwa na bado inatakiwa kwa sababu watu wengi sasa wanaacha kula sukari na wana-*opt* kutumia asali kwa sababu za kiafya.

Kwa hivyo, tuliangalie basi na huu ufugaji wa nyuki kwa vijana wetu kwa kuwapatia mizinga ya kisasa mana kuna mizinga inazalisha mpaka lita 20, lakini mtu ana mzinga unazalisha lita tano yaani ya kizamani, tuwe na mizinga ya kisasa tuwape vijana waweze kujipatia hizo ajira kupitia ufugaji huu wa nyuki ambao una pesa nyingi, robo lita tu ya asali ile iliyokuwa safi haijachakachuliwa inauzwa pengine shilingi 50,000 lakini ile asali ya kikweli kweli. Kwa hivyo, asali ni zao ambalo linatuletea pesa na litatuletea pesa za kigeni pia na litatuletea pesa za hapa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nichangie kuhusu barabara zetu. Nimeona katika hotuba yake Mhe. Rais anasema kuna ujenzi wa barabara. Mimi napenda kuitilia mkazo barabara ya Kizimbani – Kiboje, barabara hii kwa kweli mimi siku zote ilikuwa inanihuzunisha, nilikuwa napita nikienda kazini naona ile barabara inazalisha sana kwa sababu Wazungu wanakuja kwenye *spice tour* kila siku. Lakini pia kuna vitu vikubwa kuna Chuo cha Kilimo, kuna *Institute* ya *research*, kuna *laboratory* ya mbegu, kuna mambo makubwa katika ile barabara, lakini inawekewa fusi tu ikinyesha mvua ndio hivyo linaparaganyika, kila siku ni hivyo mabonde mabonde.

Naomba na hii katika vipaumbele basi itizamwe kwa ukaribu na haina kilomita nyingi ni kilomita saba tu na *point* kidogo, ifanyiwe basi uharaka ijengwe jamani ili iweze kuzalisha zaidi. Kwa sababu isijekuwa kama wale Wazungu wa Mhe. Zawadi Amour Nassor wakasema *no*, siendi tena. Sasa barabara hii inapitisha Wazungu wengi naomba itiliwe maanani. *(Kicheko/Makofi)*

Vile vile nizungumzie *road decoration*, kuna hizi *decoration* za barabarani. Barabara zetu zina ukosefu wa hizi *road decoration,* kuna sehemu nyingi hizi *zebra* zikifutika tena hapo itakaa miaka sita au saba haijachorwa tena. Kuna hizi nyengine za kuonesha watu wenye mahitaji maalum kwa sababu wanapata tabu sana katika kukata, wenye miguu yao kamili wanapata tabu sikwambii sasa ambao wana mahitaji maalum. *Road decoration* zikiwekwa na zikipewa heshima basi itafanya urahisi kwa watu kuvuka barabara.

Kwa hivyo, naomba hizi barabara za kisasa ambazo zitajengwa pia zizingatie hizo *decoration* za barabarani, lakini pia zizingatie *decoration* za watu wenye mahitaji maalum zioneshe kama sehemu hii kuna watu wasiyoona wanakatisha, watu wasiosikia wanakatisha, ziwemo zile zioneshe na hizi barabara ndio zitakuwa za kisasa na za kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nizungumzie zile *shade* za watu wanazokaa wakasubiri daladala. Vituo vyetu havina *shade* yaani utakwenda vituo vingi Zanzibar ndio ukute kile cha kusubiria kile cha kujikinga na jua au mvua. Watu wanakuwa wamekaa ovyo ovyo tu wanaumia na jua, kwa hivyo katika ujenzi wa barabara na hili walizingatie la kuweka hizo *shade* na sehemu nyengine zote.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii na naunga mkono hotuba ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante kwa mchango wako. Mheshimiwa anyefuata sasa hivi ni Mhe. Zaina Abdalla Salum baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Sabiha Filfil Thani.

**Mhe. Zaina Abdalla Salum:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, nataka nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha sote tukiwa wazima na salama na kuja kuungana pamoja kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba katika Baraza hili la Kumi kwa kikao hiki cha leo cha tatu.

Mhe. Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu kutoa pongezi zangu katika wale wenzangu waliotangulia ambao wametoa pongezi nyingi sana kwa Mhe. Rais wetu, lakini pia wametoa pongezi nyingi sana kwa uteuzi wake kwa wasaidizi wake wawili ambao ni Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais, kwani wao ni wasaidizi wa Mhe. Rais kwa hivyo, tunaomba waungane pamoja kumsaidia kazi zake pale ambapo panahitajika basi wawe pamoja na yeye. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nimshukuru sana Mhe. Rais kwa pale ambapo ametoa hotuba hii katika uzinduzi wa Baraza hili tarehe 11 Novemba, 2020, alizungumza maneno mazuri sana ambayo ni ya utekelezaji mkubwa na hasa ikionesha kuwa hotuba hii ni ya mwendo wa kasi. Kwa hivyo, kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kweli ikiwa kama mtu atakuwa kidogo mzito, basi tutamuacha njiani na hii tunategemea tutawaacha njiani kwa sababu mimi sitokubaliana nao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niwapongeze wanawake wa Mkoa wa Magharibi kwa kupitia Jumuiya ya Wanawake UWT Mkoa wa Magharibi kwa Chama changu Cha Mapinduzi, basi niwapongeze sana kwa kuweza kuniamini kwa kupitia Chama changu pia cha Watu Wenye Ulemavu wakaweza kunichagua ili niweze kuwa mwakilishi wa kuja kuwawakilisha katika nafasi hii kwa kupitia Mkoa wangu wa Magharibi.

Pia Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mhe. Rais kwa ushindi wake mkubwa alioupata kwa kura nyingi ambazo wanachama wa Chama Cha Mapinduzi wamemuonesha imani kubwa ya kuona kwamba mwendo wake wa kasi basi utaweza kuwasaidia katika ujenzi wa nchi yetu. Lakini pia sasa niingie katika hiki kitabu ambacho ametuletea hapa mbele yetu tukaweza kukijadili.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kutoa pongezi katika kuchangia kwangu kwa sababu nitakuwa ni mkosefu wa shukurani ambapo Mhe. Rais alipoanza kuitekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuona kwamba kuwawezesha watu wenye ulemavu ambapo katika mazingira yake hii ni moja tu katika uteuzi wake ambao ameufanya, basi katika nafasi zake kumi katuletea mtu mwenye ulemavu ambapo sasa hivi tumekuwa watu watatu Mhe. Anna Athanas Paul pale. Kwa hivyo, hii ni moja ya kuwa kiongozi wetu ni mahiri wa kuona kwamba watu wenye ulemavu anawajali kiasi gani. Sasa niombe tu kwamba na hawa wasaidizi wake ambao amewateuwa wakiwemo miongoni mwa mawaziri basi na wao waungane nao pamoja kuona kuwa watu wenye ulemavu wanafikia malengo yao kwa yale yanayowakwaza.

Mhe. Naibu Spika, pia nitakuja katika uwezeshaji wa kiuchumi. Uwezeshaji wa kiuchumi Mheshimiwa hii imekuwa ni changamoto kubwa kwa watu wenye ulemavu kwa sababu hii ilivyoandaliwa uwezeshaji wa kiuchumi, watu wenye ulemavu awamu iliyopita basi tukiiangalia ni kama watu kumi katika miaka mitano ambao waliopewa mikopo hii.

Kwa hiyo, naomba sana waziri aliyokuwa ana dhamana hii ahakikishe kuwa watu wenye ulemavu wanapatiwa mikopo hii ili na wao waweze kujiwezesha kiuchumi kwa kuona kwamba katika maelezeo haya aliyoyaeleza Mhe. Rais kuwa atawawezesha kiuchumi na kuwapatia elimu pamoja na mtaji wa kujiwezesha kiuchumi pamoja na kuwapatia haki zao.

Mhe. Naibu Spika, pia suala zima la elimu alishalizungumza Mhe. Panya Ali Abdalla lakini kanisaidia sana sana, mimi nisisitize tu. Mhe. Naibu Spika, kweli watu wenye ulemavu wanakosa haki yao ya msingi kuhusiana na upatikanaji wa elimu, kwa sababu watu hawa kwa kupitia ulemavu wao, wanakuwa hawana vifaa vya kuyapata masomo yale. Pia walimu wanakuwa na changamoto kubwa kuwa vifaa vya ufundishaji wa walemavu havipo, lakini pia miundombinu ya ufundishaji kwa kupitia watu wenye ulemavu wasiosikia pia havipo. Kwa hivyo, tukiangalia bajeti nyingi zinakuwa zinapita basi vifaa hivi vinakuwa havipatikani.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana Mhe. Waziri mwenye dhamana hii kipindi sasa kimefika cha mwendokasi, tunakwenda kasi. Kwa hiyo, niombe sana vifaa hivi viweze kujadiliwa au viweze kupatikana. Vile vile, kuhusiana na mamabo ya mitaala kama alivyozungumza kwamba wataipitia upya, basi pia mitaala nayo iangaliwe kuhusiana na watu wenye ulemavu, waone kwamba na watu wenye ulemavu wanaipata hii haki yao ya msingi kiufasaha zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia nije katika suala la ustwai wa jamii, wazee, wanawake na watoto. Kuna suala zima la Pencheni Jamii kwa watu wenye umri wa miaka 70. Mhe. Naibu Spika, tukiangalia sana hili jambo kalianzisha Mhe. Rais Awamu ya Saba tumpongeze sana kwa kuwathamini wazee wetu na pia Mhe. Rais wetu kalithamini anaamua kuwa aliendeleze. Lakini namuomba Mhe. Waziri pia mwenye dhamana hii apitishe uhakiki mwengine upya, ili kuwatambua vyema wazee ambao wanaokuwa na uhakika wa kupata pencheni hii.
Vile vile, ahakiki upya kuhusiana na wale wazee mpaka hivi sasa kuna wazee wengine hawaipati ile haki yao ya kimsingi, wameainishwa tu lakini kuipata hawaipati, lakini vile vile kuipata kwao kuna mwengine anapata elfu tano, mwengine elfu kumi na mwengine anapata elfu ishirini. Kwa hiyo, haki yao hasa ya kimsingi ambao waliyoanishiwa hawaipati na haiwafikii, kwa hiyo nimuombe sana Mhe. Waziri ambaye mwenye dhamana hii alifanyie jambo hilo ili ahakikishe kuwa inawafikia wenyewe walengwa ambao waliokusudiwa.

Lakini pia tuseme kwamba katika suala la amani na utulivu, hii ni jukumu letu sote ili kuona kwamba amani na utulivu katika nchi yetu inakuwepo, kwa sababu amani na utulivu bila ya kuwepo amani na utulivu tunaoumia sana ni wanawake na watoto pamoja na watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, niombe sana tuidumishe amani na utulivu ili tuone kwamba mambo yetu tunapata kuyafanya kwa ufasaha zaidi. *(Makofi)*

Kwa haya machache Mhe. Naibu Spika, niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia. Ahsante.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Zaina Abdalla Salum. Sasa nimpe nafasi, nimekwama kidogo kwa sababu wanaohusika wote wawili walikuwepo lakini naona sasa siwaoni, ambao wanatakiwa naye ni Mhe. Sabiha Filfil Thani na Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma. Sasa nitampa nafasi Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma na baada ya hapo atachangia Mhe. Sabiha Filfil Thani. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma karibu.

**Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia jioni hii ya leo kufika hapa na nikiwa ni miongoni wa wachangiaji wa hotuba hii ya Mhe. Rais aliyokuja kutufungulia baraza letu Novemba 2020.

Mhe. Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu wote kwa kuanza kumpomgeza Mhe. Rais kwa ushindi ambao ameupata wa kishindo kupitia Chama Cha Mapinduzi, ushindi huo ni ushindi wa kisulisuli haujapata kutokea tangu tumeanza mfumo wa vyama vingi, lakini Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze Mhe. Makamu wetu wa Kwanza wa Rais na tuzidi kumuombea kwa Mwenyezi Mungu afya yake iimarike, ili tuweze kujumuika katika majukumu yetu ya kikatiba lakini vile vile nimpomgeze Mhe. Makamu wetu wa Pili wa Rais kwa uteuzi ambao ameupata tukiamini kwamba uteuzi wake utakuwa ni wa mfano kwa kulinganisha na umri aliokuwa nao na kasi ya Mhe. Rais. *(Makofi)*

Vile vile, niwapongeze mawaziri wote kwa uteuzi, niseme kama Mwakilishi wa Vijana nimefurahishwa na uteuzi huu ambapo meza yote ya mbele inafurahishwa na nyuso za vijana zimeanza kutanda kulia mpaka kushoto. Kwa hilo, tunamshukuru Mhe. Rais na kupitia wao naamini mambo yatakwenda vizuri na hatutomuangusha tutafanya kazi na itaonekana na matunda yake yatazidi kuimarika.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kutoa shukurani zangu za dhati kwa chama changu Chama cha Mapinduzi, kwa kuendelea kunifunza, kunielekeza na kunikoka kupitia Jumuiya ya Vijana na leo hii kunipa ridhaa tena ya kurudi kuja kuwatetea vijana wenzangu. Mhe. Naibu Spika, hii ni heshima ya pekee kwa kijana kama mimi kupata nafasi kwa awamu mbili kuja kuwasemea vijana wenzangu na leo hii nasimama kwa mara nyengine tena kujua kutetea hoja hizi kama Mwakilishi wa Vijana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niendelee kuwapongeza na kuwashukuru Umoja wangu wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi ukiongozwa na Mwenyekiti wangu Kheri Denis James na Makamu wangu Mwenyekiti ambaye ni Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo akiwa ndiye waziri mwenye dhamana ya vijana wote wa Zanzibar na Mwenyezi Mungu amsaidie kupitia vijana sisi aipeperushe bendera hii vyema pale ambapo inahitajika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, lakini kipekee kabisa niipongeze na kushukuru Baraza langu la Umoja wa Vijana Mkoa wa Kusini kwa kuniridhia na kuniona natosha naweza kuvivaa viatu hivi vya kuweza kuwawakilisha vizuri na hatimaye leo nasimama tena kwenda kusema maneno kwa ajili ya vijana hawa. Mhe. Naibu Spika, pongezi nyengine nitazimalizia mwisho lakini kubwa kabisa naomba niende kwenye ajenda.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niseme na niungane na kauli ya Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa kusema kwamba hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni miongoni wa *golden speech* ambayo imeelekeza na imetoa mwanga kwa nchi yetu wapi tunatoka, wapi tunakwenda na nini mwelekeo kwenye taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, nianze na kesi nzima ya Uchumi wa Buluu, kiukweli niseme kwamba, ajenda hii kwetu sisi Wazanzibari ni mpya lakini mpya kwa maana tukianagalia hali halisi ya utekelezaji wake ni tayari tumeshaanza kuutekeleza lakini ukiangalia kiundani kabisa dhana hii imekuja kwa ajili ya kutukomboa wananchi wa Zanzibar lakini kuja kutukomboa vijana wa Zanzibar. Kwa kweli, naomba sana kama vile limeekewa kipaumbele kwenye maeneo yetu yote ukiangalia Dira ya Maendeleo, lakini hata kwenye Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi imeoneshwa wazi kwamba hii ndio itakuwa dira yetu kama ni sehemu ya utekelezaji wa ilani yetu.

Kwa kweli, naiomba serikali kupitia maeneo yote halisi ikiwemo maeneo ya bandari, uchimbaji wa mafuta, uwekezaji, lakini kuna maeneo ya kuimarisha ukiyaangalia hasa katika maeneo ya bahari ikiwemo uvuvi wa mwani na michezo ya bahari na maeneo mengine. Mimi niiombe serikali kupitia wenzangu hasa vijana ukiangalia ndio wanaonufaika wakubwa kwenye maeneo haya tuangalie miradi hii namna ya kutekelezwa iende moja kwa moja ikawaguse makundi maalum ambayo hayo ndio yatakuwa manufaa makubwa wakiwemo vijana, wanawake na hata watu wenye ulemavu kwenye miradi hiyo. Ukizingatia makundi haya yote kikawaida kwenye miradi mingi wanakuwa hawazingatiwi kutokana pengine na sababu za kijamii au kimaumbile. Kwa hiyo, mara hii na kwenye utekelezaji wa miradi hii izingatie namna bora ya kuwashirikisha ipasavyo ili tuweze kuwasaidia na tuende sambamba na sera hii.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ajenda nyengine inayohusiana na utalii kwa wote. Mhe. Naibu Spika, niseme kwenye hotuba hii ya Mhe. Rais amegusia dhana nzima ya utalii kwa wote, tunatambua kwamba utalii ndio tunaotegemea kwenye uchumi wa nchi yetu, lakini hii kauli haipo kuwa ngeni imeshakuwa inatekelezwa na imekuwa inazoeleka kwenye masikio ya watu. Kwa kweli, naiomba wizara husika na bahati njema Mhe.Waziri husika hapa hayupo lakini serikali ipo iangalie dhana hii kwa upana wake na kwa maana yake. Maana yake ni kwamba, kama ni utalii kwa wote basi uende ukawanufaishe wananchi wote, wale wanaohusika na maeneo ya utalii lakini na hawa wawekezaji wenyewe waliokuja kuekeza kwenye nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nishauri kwamba kwenye maeneo yetu ya utalii ukiangalia kanda zote za pwani, wananchi hali halisi ya maisha yao ni magumu kutokana na kupanda kwa bei baadhi ya bidhaa ambazo wanazihitaji kwenye maeneo yao. Kwa hiyo, naiomba serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale iende ikawaelimishe wananchi wetu, ili waone kwamba huu utalii umekuwa ni mkombozi kwenye maisha yao na sio sehemu ya kupotosha utamaduni wao, lakini isiwe sehemu pia ya kupoteza muda wao na maeneo yao ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa utalii.

Kwa maana hiyo ushauri wangu kwa serikali ishirikiane na sekta nyengine ambazo zinahusiana na utalii ikiwemo uvuvi, na hata Sekta ya Uchumi, ili kuona yale masoko ambayo yanapatikana kwenye kanda za utalii yaweze kutumika vizuri kwenye maeneo ya utalii hata ikiwezekana zile bidhaa ambazo wanazalisha hawa wajasiriamali waliokuwepo kwenye kanda zila za pwani waweze kuziuza katika soko hilo la utalii.

Nikiendelea na mchango wangu nataka kulipongeza kwenye hotuba hii kwenye ukurasa namba 30 Mhe. Rais amegusia dhana nzima ya kupambana na rushwa, ubadhirifu, uzembe sambamba na kuzuia mianya ya ufujaji wa mapato. Mhe. Naibu Spika, nadhani sote tutakuwa mashahidi Mhe. Rais tumeona juuhudi ambayo anaichukua kwenye kupambana na rushwa na hasa kwenye

kuhujumu uchumui na tumeona ziara yake ya *ZAECA* na matunda ambayo yametoka kwenye ziara ile kila mmoja Mzanzibari mwenye hisia na uchungu wa nchi hii ameridhika nayo.

Kwa hivyo, kubwa zaidi tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu aweze kupambana na vitendo hivi kwa nguvu zake zote na wala asirudi nyuma, tukiamini kwamba na sisi tulikuwemo humu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia kwenye kamati zetu za sekta hata kwenye maeneo yetu mengine ya kazi tutamsaidia hatua kwa hatua, ili kuona mambo haya yanakwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC* na nadhani kuna Kamati ya hapa ya *LAAC* pia inahusiana na uchunguzi wa fedha za serikali, lakini kuna kamati nyengine ya bajeti ambayo inahusiana na mambo yote ya fedha za serikali. Kwa hiyo, kwa umoja wetu hata na wajumbe wengine ambao wamo kwenye kamati zengine za sekta kwa umoja wetu tumuunge mkono Mhe. Rais kwa namna ambavyo anaweza kupambana na hili kwa nguvu zake zote. Kwa hivyo, naomba niseme kwamba kuptia wajumbe wenzangu tumuunge mkono Mhe. Rais tumpe nguvu ya pamoja ili tuweze kufikia yale malengo yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichangie kitu chengine kinachohusiana na ushirikishwaji wa Sekta Binafsi. Mhe. Naibu Spika, ili nchi yoyote iendelee inahitaji ushIrikishwaji wa *Private Sector* na bahati nzuri sera hii imekuwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na kwa bahati njema Mhe. Rais ameichanganua kwenye ukurasa wake wa 17 kwenye hotuba hii ametuambia kwa uwazi kabisa atashirikiana na *Private Sector* kuona nchi yetu inapiga maendeleo na inapiga hatua kupitia sekta hizi binafsi.

Kwa maana hiyo Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumuomba Mhe. Mwakilishi na Mhe. Waziri anayehusiana na mambo ya uwekezaji milango yake iwe wazi kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu, lakini milango yake iwe wazi kwa ajili ya maslahi ya uwekezaji, iwe wazi kwa ajli ya kuandaa miuondombinu ya uwekezaji ili wawekezaji wetu wawe rahisi kufika kwenye nchi yetu na kuja kuwekeza na kuja kuzitumia tunu zetu.

Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukiona wawekezaji wengi kama alivyosema Mhe. Zawadi Amour Nassor leo asubuhi wanakuwa wanakwama kutokana na miundombinu ambayo ipo katika maeneo yetu. Kwa maana hiyo serikali ipo mbele, tunaiomba serikali kwa umoja wenu muweze kushirikiana muweke *infrastructure* nzuri ili wawekezaji hawa wasiwe na ukakasi pale wanapobidi kuja kuwekeza kwenye nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna kitu chengine ambacho kimezungumzwa na bahati nzuri mimi nikiwa Mwakilishi wa Vijana naomba nichukue fursa hii kushukru na kumpongeza Mhe. Rais kwa kuona ule utekelezaji ameanza kwa nguvu zake zote, na utekelezaji wake huo ni ile ajenda ya kusema kwamba kuna ajira laki tatu kwa ajili ya vijana wa Zanzibar. Hili niseme limeanza kwa sababu hivi juzi tumeona Mhe. Rais wakisaini mkataba unaohusiana na ujenzi wa bandari, bandari hizo mimi naamini utekelezaji wake utakapokamilika itakuwa ni faida kubwa sana kwa vijana, lakini tuna ajenda hii ya Uchumi wa Buluu ikitekelezwa ipasavyo mimi naamini tunaweza kuzalisha zaidi ya ajira laki tatu kwa ajili ya vijana wetu na sisi kama vijana hatuna budi kuungana na juhudi hizi. Tutaunga mkono bega kwa bega, tuone ajenda hizi na lengo la Chama Cha Mapinduzi kama ilivyosemwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inatekelezwa kwa asilimia mia na hata ikizidi itatufurahisha zaidi.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo naweza kulizungumzia kwenye hii hotuba ya Mhe. Rais ni eneo la uvuvi. Mhe. Naibu Spika, naomba nishauri kwenye kesi ya uvuvi, maeneo mengi ya uvuvi hususan katika ukanda wetu wa Mkoa wa Kusini, maeneo ya Paje, Bwejuu, Michamvi na maeneo mengine yamekuwa yakikabiliwa na changamoto nyingi hususan uvuvi wa dhana zaifu ambazo zimekuwa zikizoeleka.

Kutokana na hali hii, namuomba Mhe. Waziri husika na bahati njema Mhe. Waziri ambaye anashughulika na uvuvi huyu ni mtu wa bahari na mtu wa pwani zaidi. Kwa hiyo, tumuombe ashirikiane na wale wananchi wanaohusika na changamoto hii au kadhia hii waweze kuwasaidia. Mhe. Suleiman Makame Ali wa jimbo la Ziwani amekuwa akitoa changamoto nyingi sana za uvuvi, kwa hiyo tuombe na Mhe. Hassan Hamad Omar wa Kojani na yeye alikuwa akisemea sana changamoto za uvuvi, tuwaombe Waheshimiwa Mawaziri watafute wataalamu wakae nao ili waone changamoto hizi na matatizo haya yanayowakabili wavuvi wetu yaweze kutatuka vizuri.

Lakini sasa hivi tumeelekeza nguvu zetu kwenye uvuvi mkubwa, nini *target* yetu kwenye uvuvi mkubwa. *Target* yetu ni kwamba, tuweze kuyafikia yale maeneo ambayo bado hayajafikiwa, vipi tumejipanga serikali ili tuone maeneo haya tunayafikia kwa wakati. Mhe. Waziri naamini wizara yako hii imeundwa kwa lengo la kuwasaidia wavuvi lakini imeundwa kwa ajili ya kuwasaidia Wazanzibari, pia imeundwa kwa ajili ya kusaidia uchumi wa Zanzibar ili uweze kusonga vizuri. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri vifaa hivi vinapogawia vifaa vya uvuvi wajitahidi wazingatie yale maeneo athirika na maeneo tajwa ambayo yapo wazi na yanafahamika.

Mhe. Naibu Spika, nikiongelea suala zima la bandari nadhani hapa nitakuwa nimegusia vitu vingi lakini naenda kwenye sekta nzima ya biashara na viwanda. Mhe. Naibu Spika, tuseme ukweli kwenye Sekta ya Viwanda tunakwenda moja kwa moja kuwagusa wakina mama, vijana lakini tunakwenda moja kwa moja kuwagusa wananchi wa Zanzibar na wananchi wa Tanzania kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukiona mafanikio makubwa ambayo yanatoka kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajenda ya kuimarisha sera yao ya viwanda na sisi bahati njema tumeiweka kama ni ajenda yetu Zanzibar. Naamini maeneo ya viwanda yapo mengi, juzi tu Mhe. Rais aliyepita Dkt. Ali Mohamed Shein alikwenda kuzindua maeneo ya viwanda pale Chamanangwe imani yangu kwamba maeneo yale tutayatumia vizuri lakini kuna maeneo mengine kwenye Jimbo la Dimani eneo la Shakani eneo lile ni la viwanda na limetelekezwa niiombe Mhe. Waziri wa wizara hii warudi tena kwenye maeneo yale ya viwanda.

Kwa mfano, kuna kiwanda kimoja kinaitwa kiwanda cha mbao kipo eneo kubwa sana kimetelekezwa, naomba sana Mhe. Waziri ambaye anayehusika kwenye wizara hii ingawa hayupo lakini yupo ambaye anakaimu naomba mtafute timu ya wataalamu, ambao watakwenda kuangalia yale maeneo, kuna nini na maeneo hayo tayari sasa hivi yameshavamiwa na yanajengwa na wananchi bila ya ridhaa ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba sekta hii ya viwanda ikitekelezwa, wafaidika wakubwa ni sisi vijana. Vijana tayari tumeshawaahidi kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, lakini

tumeshawaahidi kwenye Dira yetu ya Maendeleo kwamba tuna ajira zaidi ya laki tatu, ajira hizi zitatoka wapi tusipoitekeleza ajenda hii vizuri. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Mawaziri waliopewa dhamana hizi, watumie dhamana zao vizuri ili kuona mafanikio yanapatikana vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwenye kesi nzima ya makusanyo ya kodi. Tumekuwa tukiona kwamba changamoto kubwa ambayo inaitawala nchi yetu ni uvujaji wa mapato. Mapato mengi yanapotea na sijui yanapotea kwa namna gani. Leo hii Mhe. Waziri wa Fedha yupo pale ni kijana, tunaamini *system* nzima ya ukusanyaji wa kodi utakuwa mzuri zaidi, hatuna mashaka na ukusanyaji wa kodi. Lakini shida yetu kwa nini mapato haya hayaongezeki kwa kiwango ambacho tunahisi sisi tutaridhika kama wananchi wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, kitu chengine, nimpongeze Mhe. Rais kwa kuona amemteuwa Mkurugenzi mpya wa Bodi ya *ZRB* jana. Nadhani hii itakuwa ni mwanzo wa safari nzuri ya lile lengo ambalo tunalikusudia kwa kuona fedha hii ya serikali inaongezeka kwa kiwango na kwa *speed* ile ambayo tunaitaka sisi.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa ninukuu Kauli ya Mhe. Rais inayosema kwamba "kote nilikopita wakati nikiomba kura, nikiomba ridhaa kwa wananchi wa Zanzibar, nimekutana na ari, shauku, utayari wa hali ya juu kwa waume na wanawake, vijana kwa wazee, wakulima kwa wavuvi, wafanyabiashara kwa wafanyakazi na makundi yote ya kupokea mapinduzi mapya ya kiyuchumi, kuna kujenga uchumi mpaya wa Zanzibar. Wanachi wetu wamechoshwa na siasa za uhasama, kuhubiri chuki na visasi ambavyo havibadilishi hali halisi ya maisha yao kuwa bora zaidi, wanataka matunda ya mapinduzi na si simulizi za mapinduzi na muungano" Mwisho wa kunukuu. Mhe. Naibu Spika, hili nimependa niliseme kutokana na hali halisi ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, tukizungumza uhalisia tulokuwanao huko mitaani, sote tunaishi kwenye mitaa yetu na kwa bahati njema kuna mheshimiwa mmoja jana aligusia, lakini mi naomba leo nigusie kidogo kwa upande mwengine. Mhe. Naibu Spika, bei za bidhaa zetu tunazohudumia wananchi wetu bado zipo juu. Naamini tukifanya na tukitekeleza vizuri haya maagizo na *speech* hii ya Mhe. Rais ambayo ameisema hapa, lakini na ile ambayo tumeiahidi kwenye Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi, naamini tutafungua mianya ya kuwawezesha wananchi wetu kuondokana na huu ugumu na ukakasi wa maisha.

Mhe. Naibu Spika, tunatambua bidhaa hazishuki bei, zinapanda bei lakini tuwatafutie namna ya kuweze kuitafuta fedha na kuweza kuipata fedha, ili wakidhi mahitaji yao haya ambayo wameyakusudia.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa, niseme na niendelee kushukuru na kupongeza familia, wapenzi, ndugu lakini na wazazi wetu kwa dua njema ambazo wanatuombe watoto wao na sisi tunazidi kuwaambia waendelee kutuvumilia, waendelee kutuombe, sisi watoto wao tumejitoa kwa ajili ya nchi yetu na kwa ajili ya maslahi ya taifa letu. Naunga mkono hotuba kwa asilimia mia. (*Kicheko/Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante, Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma kuna jambo walikuwa wanalisubiri ndio maana wamecheka sana. Tunaendelea, Waheshimiwa Wajumbe, sasa

mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mhe. Sabiha Filfil Thani na baada ya hapo basi kama tutakuwa na nafasi watachangia mawaziri pamoja na Makamu wa Pili wa Rais.

**Mhe. Sabiha Filfil Thani:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kupata fursa ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kutujaalia siku ya leo tumeamka tukiwa wazima na wenye afya njema kuweza kuhudhuria hapa katika kikao hichi cha Baraza la Wawakilishi.

Kwa vile mimi ni kikao changu cha kwanza, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza Kuu la Wazazi Taifa, Wajumbe wa Baraza la Wazazi la Mkoa wa kusini Unguja, Kamati Kuu ya Chama changu ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuridhia kulirejesha jina langu kuwa Mwakilishi wa Umoja wa Wazazi katika nafasi hizi za wanawake.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuwashukuru, napenda kumshukuru Mhe. Rais kwa uteuzi wake wa Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa pili wa Rais, sambamba na Mwanasheria Mkuu. Napenda kumshukuru Mhe. Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa kupata kura kwa asilimia mia moja, hii inaonesha imani ya wawakilishi juu yao. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, shukurani za pekee zimuendee Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, kwa kupata kura za kishindo haijapata kutokea toka tumeingia katika mfumo huu wa vyama vingi. Katika hili naomba niungane na wenzangu kuipongeza hotuba hii, imetoa dira ya muelekeo wa mapinduzi ya kiuchumi ya kuijenga Zanzibar mpya na ndio matarajio ya wananchi anaowaongoza.

Mhe. Naibu Spika, ili kufikia hapa inatupasa tuwe tuwajibika kila mmoja kwa nafasi yake, tuna usimamizi kila mmoja kwa nafasi yake, tusimamie na tupige vita ufisadi, wizi wa mali ya umma na la mwisho ni amani na utulivu. Tukiweza kuyasimamia haya tutafikia lengo la Mhe. Rais alilolikusudia.

Naanza kwenda moja kwa moja katika suala hili la udhalilishaji. Nataka kuchangia hapo, namshukuru Mhe. Rais kwa kuona ipo haja ya kuanzisha mahkama hii inayoshughulikia kesi za udhalilishaji, tunampongeza sana. Tunaloliomba itakapofika wakati wa kufanya kazi, hukumu zitakazotolewa zitangazwe kwenye vyombo vya habari. Kwa kipindi kikubwa huwa tunasikia kwenye mawio wakati wa tukio tu, lakini wakati wa hukumu huwa ni kimnya au adhabu zinazotolewa halizilingani na uzito wa kesi zenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, jengine nnalotaka kuchangia, nimeka nikafikiria suala hili la udhalilishaji litamalizika hadi lini. Naomba kila mmoja turudi katika imani ya dini zetu, wakiristo kwa upande wao na waislamu kwa upande wetu. Suala hili la imani tunaanzia katika mifumo ya vyuo vya madrasa ambavyo wamo walimu ambao wanasomesha ambao tumewakabidhi dhamana za watoto wetu.

Kwa kweli, hapo nyuma vyuo vya madrasa vilikuwa vina mwalimu Mkuu halafu ndio hao vina hawa mabarobaro. Kwa hivi sasa walimu wale hawapo, waliobakia ni vijana tu. Hawa vijana muda mkubwa wanakuwa faragha, faragha inapopatikana, ndivyo hivyo vitendo vya udhalilishaji

vijavyojitokeza na wala sio wote lakini baadhi ya hawa maustadhi. Jamani kazi hii ina thawabu kubwa sana, lakini inataka imani ya dhati ya mtu ndani ya nafsi yake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tusione pesa wanazotoa wazazi ni kidogo, wafikirie fungu wanalolipata kwa Mwenyezi Mungu. Tunaomba sana walimu wa Vyuoni watusaidie ulezi katika suala hili la malezi ya watoto wetu. Tumewaamini sana, tunawapenda sana, tuko pamoja nao, tunachangia kwa kila michango ambayo inahitajika katika vyuo hivi, wazazi tunajitolea. Lakini na wao watupe faraja ya wazazi ya kuona watoto wetu wapokuwa nao, wanakuwa katika mikono salama.

Jengine ambalo nataka kuchangia suala la wawekezaji. Katika eneo hili kuna tatizo, kuna baadhi ya wawekezaji wamepewa maeneo kwa ajili ya uwekezaji, lakini wanachokifanya wanazungusha makuta, uwekezaji hauonekani. Umeshafika wakati Mhe. Waziri wa Uwekezaji na Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi waone jinsi gani ya kuweza kumsaidia Mhe. Rais. Kutokana na hali hiyo, naomba ufanyike utafiti wa kina kuhusu maeneno yote waliopewa kibali cha uwekezaji na wakashindwa kuyaendeleza kwa zaidi ya miaka mitano, basi maeneo hayo yarudi serikali, ili waweze kupewa wawekezaji wengine waweze kuyaendeleza. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo napenda kuishukuru familia yangu, wafanyakazi wenzangu kwa kuniunga mkono katika kipindi chote cha uchaguzi hadi hivi sasa. Baada ya hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana, nashkuru Mhe. Sabiha Filfil Thani, Waheshimiwa Wajumbe bado tunaendelea kuchangia hotuba ya Mhe Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Wachangiaji niliowabakisha ni Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara mbali mbali. Nimeombwa na Mawaziri kwa sababu kuna hoja nyengine ambazo wao watakuwa na uwezo wa kuzijibu vizuri tukijaaliwa Jumatatu. Kwa maana hiyo, basi naomba mniruhusu niakhirishe kikao hiki kwa muda huu ili Jumaatatu Mawaziri ambao watataka kuchangia, akiwemo Makamu wa Pili wa Rais, waweze kuja na majibu pamoja na mambo mengine ambayo yatahusiana na hotuba hii. *(Makofi)*

Kwa mstakbali huo nimuombe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, eeh! Samahani. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuakhirisha kikao chetu kwa mujibu wa kanuni za muda wa kikao, ili tuweze kuakhirisha. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

## KUAKHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwa vile shughuli za leo zimemalizaika kabla ya muda kumalizika, ili kutoa fursa kwa Waheshimiwa Mawaziri kuja kutoa ufafanuzi wa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe siku ya Jumaatatu. Naomba kutoa hoja ya kutengea Kanuni ya 23, ili tuweze kumaliza mijadala ya leo kabla ya kufika muda wake. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:** Mhe. Naibu Spika, naafiki.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Waheshimiwa, Mhe. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ametoa hoja, wanaokubaliana na hoja hiyo, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa utulivu wenu leo hii, lakini labla ya kuakhirisha nna tangazo linalohusiana na semina ya kesho ambayo itafanyika katika jengo la *ZURA*, kuanzia saa 3:00 asubuhi. Waheshimiwa Wajumbe mnahimizwa kufika kwa wakati.

Baada ya tangazo hili, naomba sasa kuakhirisha kikao hadi Jumaatatu saa 3:00 asubuhi. Ahsanteni sana.

*(Saa 1:14 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 15/02/2021 saa 3:00 asubuhi)*